# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Sita – Tarehe 13 Aprili, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali. Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 68

**Hitaji la majengo ya Kituo cha Afya Nguruka – Kigoma Kusini**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga majengo katika Kituo cha Afya Nguruka kilichopandishwa hadhi ya kuwa Hospitali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Nguruka kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza Mkoani Kigoma kinahudumia wakazi wapatao 135,546. Kituo kinatoa huduma kwa ngazi ya kituo cha afya kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza imekwisha jenga hospitali mpya ambayo imeanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, kituo hiki kina uhitaji wa majengo mbalimbali ya kutolea huduma ikiwa ni pamoja na wodi mbili

za kulaza wagonjwa, kliniki ya mama na mtoto, jengo la kuhifadhia maiti na jengo la kufulia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 kituo hicho kimetengewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo itakayowezesha kutoa huduma kwa ngazi ya kituo cha afya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bidyanguze swali la nyongeza.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niishukuru Serikali kwa majibu mazuri pamoja na kwamba wananchi walitegemea iwe ni hospitali lakini kwa sababu kwa kuwa Halmashauri imeshakuwa na hospitali haiwezekani kupata hospitali nyingine ya Wilaya.

Je, ni lini fedha hizi ambazo zimetengwa zitakwenda kwa ajili ya utekelezaji kwa sababu mwaka wenyewe ndiyo unaelekea mwisho maana Juni ndiyo mwisho.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, naomba Mheshimiwa Waziri aweze kuongozana nami kipindi hiki ambacho Bunge linaendelea aweze kwenda kuona kituo chenyewe cha afya ambacho tunakizungumzia kwa sababu kina hali mbaya sana. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bidyanguze hilo swali nilikuwa najiuliza akiongozana na wewe nani atajibu maswali huku nyuma kipindi hiki ambacho Bunge linaendelea. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Jimbo la Kigoma kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Sera ya Afya kwa sasa Halmashauri moja inakuwa na hospitali moja na ndiyo maana Serikali ilileta fedha imejenga Hospitali ya Halmashauri, kwa hiyo, hiki lazima kiendelee kama kituo cha afya. Fedha hizi zitapelekwa ndani ya mwaka wa fedha huu wa 2022/2023 Serikali inatafuta fedha ili kupeleka fedha kwa ajili ya mpango huo wa kukamilisha kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, niko tayari kuongozana nae na ningeomba uridhie tuongozane baada ya kuahirisha Bunge hili ili tukapate muda wa kutosha, tufanye ziara hiyo na kufanya majukumu hayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, aliyekuwa Waziri wa TAMISEMI alituahidi mwaka jana kwamba angetupatia kituo cha afya kwenye Kata ile ya Kirua Vunjo Kusini kwenye Kijiji cha Kohesa. Sijui mtaanza lini kujenga hospitali hiyo kwa sababu tulipata mbadala wa kupata Hospitali ya Wilaya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, Mbunge wa Jimbo la Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi ya Serikali itatekelezwa, ni suala la muda tu kwa hiyo Serikali inatafuta fedha ili kwenda kutekeleza ahadi hiyo kupeleka Kituo cha Afya katika Kata aliyoitaja, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL S. BARAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa, Kituo cha Afya cha Gallapo kinahudumia Tarafa nzima ya Babati ikiwemo Kata za Endakiso, Mamire, Qash na Gallapo. Je, ni lini Serikali itajenga nyumba ya Mama na Mtoto na chumba cha kuhifadhia maiti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nilifanya ziara Babati Vijijini, tulishirikiana sana na Mheshimiwa Mbunge tulifika Kituo cha Afya cha Gallapo, ni kweli kinahitaji muindombinu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali imeweka mpango wa kutafuta fedha kupeleka Gallapo ili kianze ujenzi wa majengo ya Mama na Mtoto na majengo ambayo yanapungua, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kata ya Kimala ipo pembezoni sana mwa Wilaya ya Kilolo na hakuna Kituo cha Afya, katika ile Kata barabara hazipitiki wananchi wanaenda katika Kituo cha Afya cha Dabaga.

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuwajengea Kituo cha Afya katika Kata hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata hii ya Kimala ambayo iko pembezoni tulishaelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo kufanya tathmini na kuwasilisha Kata za kipaumbele za kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa vituo cha afya. Kwa hiyo, nitoe rai kwa Mkurugenzi kufanya hayo maelekezo ya Serikali na kutuletea, ikiwa ni kipaumbele cha Halmashauri hiyo basi Serikali itaona namna ya kutafuta fedha kushirikiana na mapato ya ndani lakini pia fedha za Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yawe mafupi nenda moja kwa moja kwenye swali unalotaka kujibiwa bila maelezo ambayo hayahusiani na swali husika. Mheshimiwa Asia Halamga swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kata ya Endago ya Wilaya ya Hanang ina wakazi zaidi ya 5,600 lakini haijawahi kuwa na Kituo cha Afya wala Zahanati. Je, ni lini Serikali itapeleka huduma ya afya katika Kata hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la

nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kata hii ina idadi kubwa ya wananchi zaidi ya 5,000 lakini haina zahanati. Nimhakikishie kwamba tunaweka mpango wa kutafuta fedha kwenda kujenga zahanati katika eneo lile, ikibidi tunaweza tukaona uwezekano wa kujenga Kituo cha Afya baada ya tathmini kuona inakidhi vigezo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Idd Mpakate swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kituo cha Afya Mtina kilichopo katika Jimbo la Tunduru Kusini kilitegewa shilingi milioni 250 katika bajeti hii ambayo ipo 2022/2023. Je, ni lini Serikali itapeleka pesa hii kwa ajili ya kuboresha huduma ya Mama na Watoto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba kwa sababu ipo kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha, naamini kwamba ifikapo Juni 30, fedha zitakuwa zimepelekwa kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wilaya ya Kilindi ina Tarafa Nne, Tarafa Tatu zina vituo

vya afya. Je, ni lini Serikali itajenga kituo afya Tarafa ya Kimbe, Kijiji cha Ndegerwa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Omari Kigua Mbunge wa Jimbo la Kilindi kama ifiatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tarafa hii ya Kimbe ambayo haina kituo cha afya tayari ilishawekwa kwenye mpango wa Tarafa za kimkakati, sasa fedha tu inatafutwa ikishapatikana itakwenda kujenga kituo cha afya kwa ajili ya kusogeza huduma kwa wananchi. Ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo swali la nyongeza. Mheshimiwa Boniphace Butondo swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kituo cha Afya cha Negezi na Mwang'alanga ni moja kati ya vituo vya afya ambavyo vimeanza kufanya kazi katika kipindi hiki lakini bado vina mapungufu ya wodi za kawaida za wagonjwa, mapungufu ya mochwari na *walk ways*. Ni lini Serikali itakwenda kukamilisha vituo hivi vianze kufanya kazi ipasavyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniphace Butondo, Mbunge wa Jimbo la Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Negezi na hivyo vingine ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja ni miongoni mwa vituo ambavyo Serikali imeweka mpango wa kuhakikisha vinakamilishwa kwanza kabla ya kuanza vituo vingine vipya, ndiyo maana katika mwaka uliopita wa fedha na mwaka huu hatujajenga vituo vingi sana vya afya vipya kwa sababu lengo ni kukamilisha kwanza vituo ambavyo vimeanza kwa sehemu ili vitoe huduma kwa upana wake na baadae tuende kwenye vituo vingine.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ipo kwenye kipaumbele. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA**: Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 69

**Ukosefu wa barabara za mchepuko katika Mji wa Tunduma**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya mchepuko kwa kiwango cha lami kutoka Mpemba kupitia Chapwa Mwakakati katika Mji wa Tunduma kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa sasa Mji wa Tunduma umekuwa ukikumbwa na msongamano mkubwa wa magari kuanzia Mpemba hadi Forodhani *(Boarder)* hali

inayosababisha usumbufu kwa watumiaji wa barabara ya ndani ya Tunduma na wanaokwenda uelekeo wa barabara ya Tunduma - Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza adha hiyo, Serikali itatenga kiasi cha shilingi bilioni 1.5 katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Sogea - *Transformer* yenye urefu wa kilometa 2.0 kwa kiwango cha lami ili iwe njia mbadala kwa watumiaji wa barabara za Mji wa Tunduma.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya barabara ya mchepuko inayoanzia Mpemba – Chapwa - Makambini kadri ya upatikanaji wa fedha ili kuondoa msongamano mkubwa wa magari. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninashukuru kwa majibu mazuri lakini kuna changamoto ambayo ipo.

Mheshimiwa Spika, hii barabara tunayoiongelea hapa ni barabara ambayo ni ahadi ya Hayati Mheshimiwa Rais Magufuli na pia kumekuwa na barabara nyingine ya Chapwa, Chindi, Msangano ambayo hii ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja Songwe tarehe 06 Julai, 2020. Ninataka kufahamu kwa nini ahadi za Viongozi hazitekelezeki kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto nyingine ambayo ipo ya ujenzi hafifu wa barabara za lami kwa *TARURA*. Ninataka kufahamu ni kwa nini barabara zao haziwi na ubora, mfano mzuri uko katika Jiji lako la Mbeya utaona barabara ya Kabwe – Isanga, barabara ya Mafiati - Airport,

barabara ile ya kutoka njiapanda ya Ilonda kwenda Isyesye ni barabara zinazoharibika kabla ya muda.

Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu ni kwa nini barabara zao zinakuwa hazina ubora? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa ya Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi zote za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ni kipaumbele katika utekelezaji wake na Serikali imekuwa ikitekeleza ahadi za viongozi kwa awamu kwa sababu ziko nyingi, kwa hiyo kadri ya fedha zinavyopatikana ahadi zile zinatekelezwa. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba ahadi hii ya Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kipaumbele na Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji. Ndiyo maana katika bajeti ijayo itatenga Bilioni Moja na Milioni Mia Tano kwa ajili ya kuanza utekelezaji huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara za lami za *TARURA* barabara zetu za lami za kipindi cha nyuma kabla ya 2022 zilikuwa zinajengwa kwa maana ya kubeba uzito wa chini ya tani 10 hadi 15, baada ya kuona siyo rahisi ku-*control* magari yenye uzito mkubwa Serikali kupitia *TARURA* tumeborsha sasa tunakwenda tani 30 na kuendelea. Kwa hiyo sababu ya kuonekana barabara zile zilikuwa ni dhaifu ni kwa sababu zilikuwa zinajengwa kwa kiwango cha tani 10 lakini magari mazito zaidi yaliweza kupita, tunaamini sasa hatutakuwa na changamoto hiyo kwa sababu tumeboresha mfumo huo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Jimboni kwako Mheshimiwa Waziri Wanging'ombe kuelekea Lupira, kwa maana Kipengere - Lupila na barabara ya Esaprano. Barabara hizi ni za kiuchumi lakini zimekuwa zikisumbua kwa muda mrefu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Richard Sanga Mbunge wa Jimbo la Makete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mbunge jirani yangu amekumbusha suala la msingi na tayari nimhakikishie kwamba kwenye bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI suala hilo ni kipaumbele kujenga barabara kutoka kipengere kuelekea kule Lupila na itatekelezwa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, sasa aulize swali lake.

Na. 70

**Kuwa na Chuo cha *VETA* katika kila Jimbo**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuwa na Chuo cha *VETA* katika kila Jimbo ili kuwakomboa vijana na tatizo la ajira?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa elimu sayansi na teknolojia Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Jimbo la Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, azma ya Serikali ni kujenga Chuo cha Ufundi Stadi *(VETA)* katika kila Mkoa na Wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vyuo vya *VETA* katika Wilaya 63 ambazo hazina vyuo hivyo. Kiasi hiki pia kitatumika katika ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Songwe ambao hauna chuo cha ngazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, Serikali inaendelea kutekeleza azma hiyo na ikishakamilisha ujenzi wa *VETA* katika kila Wilaya itaangalia uwezekano wa kuanza kujenga vyuo hivyo katika Majimbo kulingana na uhitaji na upatikanaji wa fedha. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Majimbo ya Vijijini yana maeneo makubwa sana ya kiutawala lakini yana mahitaji makubwa ya elimu ya *VETA*.

Je, Serikali haioni sababu ya kuowandolea adha wananchi wa vijijini kutafuta elimu hii kwa umbali mrefu?

Mheshimiwa Spika, kutokana na hoja za swali nililouliza hapo juu, Serikali ni lini itajenga chuo cha *VETA* angalau kimoja kwenye Jimbo la Lulindi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Mchungahela kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo la ujenzi wa vyuo hivi katika ngazi za Wilaya ni kusogeza huduma hizi karibu kule Wilaya. Tunafahamu kweli zipo Wilaya ambazo zina maeneo makubwa ya kiutawala, lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati tunajenga vyuo hivi, tunaweka vilevile na huduma ya mabweni. Lengo la huduma za mabweni ni kuhakikisha wanafunzi wote ambao wanatoka mbali kuweza kukaa pale pale chuoni na kuweza kupata huduma hii kwa karibu zaidi. Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi, bado tunaweza tukawahudumia wale ambao wametoka mbali kwa sababu watakuwa wanakaa pale pale chuoni.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, anazungumzia suala la ujenzi kama nilivyoeleza kwenye majibu yangu ya swali la msingi, kwamba kwa sasa tunakamilisha kwanza ujenzi wa vyuo hivi katika wilaya hizi, halafu tutaangalia sasa yale majimbo yenye changamoto ikiwemo labda na jimbo lake pamoja na Jimbo la Nanyamba kule nako kuna malalamiko makubwa sana. Hii itategemea sasa vile vile na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru. Serikali mwaka 2021 iliahidi kujenga Chuo cha *VETA* katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara Kata ya Kisawasawa. Sasa hivi tunapewa taarifa kwamba chuo hakitajengwa katika Halmashauri hiyo kwa sababu kuna Chuo cha Ufundi cha *FDC*. Chuo kinaenda kujengwa katika Halmasahuri ya Mlimba:-

Mheshimiwa Spika, nataka kujua: Je, kuwepo kwa Chuo cha Ufundi cha *FDC* ni sababu ya kukosa vyuo vya *VETA*? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Asenga, Mbunge wa Ifakara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu ya swali la msingi, vyuo hivi tunajenga katika ngazi ya Wilaya, havijengwi katika ngazi ya Halmashari. Ni jukumu la Wilaya kuangalia kwamba vinakwenda kujengwa wapi? Kwa zile Wilaya ambazo zina Halmashauri zaidi ya moja, ni lazima wakae chini Wakuu wa Wilaya pamoja na Wakurugenzi ili waweze kuamua wapi chuo hiki kinakwenda kujengwa? Kwa hiyo, sisi jukumu letu ni kwenda kujenga Chuo cha *VETA* lakini majukumu au wajibu wa kuchagua eneo gani la kwenda kujenga linabakia katika Wilaya husika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa *VETA* Wilaya 63

na Wilaya ya Nyang'hwale tayari upembuzi yakinifu umeshafanyika; je, katika Wilaya 63 na Nyang'hwale ikiwemo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Hussein Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwamba vyuo hivi vinaenda kujengwa kwenye Wilaya na kama tayari tumeshafanya upembuzi yakinifu, tafsiri yake ni kwamba tumeshakuja kufanya *Geotechnical Survey, Topographical Survey* pamoja na *Environmental and Social Impact Assessment*. Kama shughuli zozote zimeshafanyika kwenye eneo lako, *is likely* kwamba chuo hicho kinakuja kujengwa kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tena, nenda moja kwa moja kwenye swali ili utoe fursa kwa Mbunge mwenzako kuuliza swali pia.

Mheshimiwa Mohamed Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ujenzi wa Chuo cha *VETA* Chemba umekamilika, nataka kujua ni lini sasa kitafunguliwa ili kidahili wanafunzi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la

nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Monni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli ujenzi wa vyuo 25 vile vya Wilaya awamu ya kwanza pamoja na vinne vya Mikoa, tayari ujenzi umekamilika. Jukumu letu tulilonalo sasa hivi ni utafutaji wa vifaa na kuajiri walimu kwa ajili ya kwenda kufundisha kwenye maeneo hayo. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mwaka ujao wa fedha kuanzia mwezi Julai tutaanza kutoa kozi za muda mfupi lakini kuanzia Mwezi wa Kumi tutafanya usahili sasa kwa ajili ya kozi za muda mrefu sambamba na upelekaji wa vifaa vya kufundishia kwenye maeneo hayo kwa sababu samani tayari tumeshapeleka.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Liwale iliahidiwa kujengewa Chuo cha *VETA* kwenye bajeti hii inayotekelezwa sasa. Mpaka leo hii imebakia miezi miwili bajeti inakwenda kwisha: Je, lini tutapewa fedha hizi tuweze kujenga chuo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari tumeshapeleka fedha za awali kwa ajili ya *mobilization* na zile kazi za mwanzo; na kazi nyingine za *Geotechnical Survey, Topographical* pamoja na *ESIA (Environmental and Social Impact Assessment)* tayari zimeshafanyika. Kwa hiyo, hivi sasa tunachokamilisha ni

kupata matokeo ya tafiti hizi tulizokwenda kufanya. Baada ya matokeo hayo, tayari tutapeleka fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa maeneo yote yale 63 tuliyoyataja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Halmashauri yangu ya Nanyumbu imepokea fedha za ujenzi wa Chuo cha *VETA,* lakini cha kushangaza fedha hizi zimekabidhiwa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ambayo ipo kilometa 90 kutoka wilayani kwangu: Kwa nini fedha hizi zimepelekwa Masasi wakati Nanyumbu yupo mdhibiti ubora ambaye angesimamia fedha hizi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Yahya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli fedha tumepeleka katika *FDC* ya Masasi na hatukupeleka kwenye Wilaya ya Nanyumbu moja kwa moja kwa sababu *FDC* Masasi ndipo ambapo fedha tutazipitishia pale. Tumeona ni muhimu kupitishia hizo pesa pale baada ya kufanya *study* ile ya ujenzi awamu ya kwanza; Vyuo vyote vya *FDC* wamesimamia vizuri zaidi vile vyuo vya *VETA* kuliko zile ofisi zetu za wadhibiti ubora. Kwa hiyo, tumepitisha kule kwa sababu ya kupata usimamizi makini kwa chuo chetu kile na matumizi ya fedha yaweze kuwa sahihi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kama alivyozungumza kwenye majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri kwa suala la *FDC* na *VETA*, kwamba lengo ni kupeleka katika kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri haona sasa wakati umefika wa ku-*engage* TAMISEMI katika mlolongo huu wa kwenda kusimamia ili hivi vyuo kuwa endelevu? Serikali haioni wakati umefika wa kumshirikisha TAMISEMI katika usimamizi wa hivi vyuo vya ufundi? Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ametoa ushauri wa kwamba tushirikiane, lakini tumekuwa tukishirikiana kwenye eneo hili la utoaji wa elimu kuanzia shule hizi za msingi, sekondari mpaka vyuo. Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi kwamba ushirikiano upo, lakini kwa vile ametoa ushauri, ushauri huo tumeuchukua tunaenda kuufanyia kazi. Kwa maana ya ushirikiano, bado tunaendelea kushirikiana na TAMISEMI kwa sababu vyuo hivi viko kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nyongo, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Swali langu kwa Mheshimiwa Waziri ni moja tu kwamba: Kwa kuwa mnakwenda kujenga sasa vyuo kwa wilaya zote, ina maana

ya mahitaji ya walimu wa ufundi yanakwenda kuongezeka: Mna mpango gani maalum kama Wizara wa kuzalisha walimu wa kwenda kufundisha elimu ya ufundi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Nyongo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli ujenzi wa vyuo hivi; vile 25 na hivi 63 na hivi vya mikoa unakwenda kuongeza uhitaji wa walimu kwenye eneo hili. Naomba nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, kwanza tuna chuo chetu ambacho kinafundisha walimu wa masuala haya atakayekwenda kufundisha maeneo haya ya vyuo vya ufundi pale Morogoro. Vile vile, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Nyongo, tunakwenda kufanya maboresho ya mitaala pamoja na sera yetu ya elimu. Tutakwenda ku-*convert* vyuo vyetu vile vya ualimu tulivyokunavyo zaidi ya 35 ili tuingize *component* au kada ya ufundi mle ndani ili tuweze kupata hiyo *supply* ya walimu kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie vile vile Mheshimiwa Nyongo kwamba, Mheshimiwa Rais tayari alishatoa kibali cha kuajiri watumishi au walimu zaidi ya 571, ambao tunaendelea na mchakato na mpaka kufika sasa walimu 171 tayari tumeshaajiri kwa ajili kuanza kutoa mafunzo kwenye vyuo 25 ambavyo ujenzi wake umekamilika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 71

**Kukamilisha utekelezaji wa sera ya kupeleka umeme vijijini**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha utekelezaji wa Sera ya kupeleka umeme Vijijini kupitia Mpango wa *REA III* Mzunguko wa Pili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa kusambaza umeme vijijini, awamu ya tatu mzunguko wa pili unaosambaza umeme vijijini vikiwemo vijiji vya Kilwa Kusini vyote, unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Desemba, 2023. Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan imeongeza wigo wa mradi toka kilomita moja kwa kila kijiji na kufikia kilomita tatu (1+2) katika usambazaji wa umeme katika vijiji ili kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, awamu hii ya *REA III Round II* itakapokamilika hakuna kijiji ambacho kitabaki bila umeme.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali yanayotia moyo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza. Kilwa Kisiwani kwa sababu ni kisiwa utaratibu wake ni wa kipekee. Je, na yenyewe nayo imo katika mpango huu na awamu hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Kata za Nanjirinji, Narikalage pamoja na vijiji vyake vya Nainokwe, Liwiti pamoja na Narikilage yenyewe inapitiwa na msitu wa hifadhi na kulikuwa na mgogoro kati ya *REA* na *TFS*: Je, mgogoro huo umekwisha na Serikali sasa iko tayari kusambaza umeme katika kata hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikianza na swali la kwanza, tunafahamu kwamba kuna vijiji katika Jimbo la Kilwa Kusini ambavyo vipo katika visiwa na upo mradi unaitwa *RBF (Result Based Financing)* awamu ya pili ambao utafikisha umeme katika visiwa hivyo pamoja na visiwa vingine Tanzania Bara 36 katika awamu hii. Kwa hiyo, pamoja na visiwa hivyo viwili, viko visiwa vya maeneo mengine vya maeneo mengine ambavyo pia vitafikishiwa umeme katika miradi hii ambapo tunatafuta sasa wakandarasi wa kupeleka mradi wa umeme katika maeneo hayo. Kwa upane wa Kilwa amepatikana Mkandarasi anaitwa *Greenl Leaf* ambaye anakamilisha taratibu za kupeleka umeme katika maeneo hayo ya visiwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la pili, ni kweli tulikuwa na changamoto ya mawasiliano katika ya Wizara ya Nishati na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitisha miundombinu ya umeme katika mapori ya *TFS,* lakini tatizo hilo sasa limekuwa *solved,* na sasa tunazungumza lugha moja. Kwa hiyo, sasa kunapokuwa na mradi unaohitaji kupita katika maeneo hayo, vibali vinatolewa na mradi unaweza kupitishwa kwa wakati.

Kwa hiyo, kwa sasa tatizo hilo limetafutiwa ufumbuzi na halina tatizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Pamoja na utekelezaji wa *REA III* unaoendelea Wilaya ya Nkasi lakini umeme unakatika kupita kawaida: Serikali ina mpango gani wa haraka wa kutatua changamoto hii ambayo wananchi wangu wanapata hasara kubwa hasa wanaosindika Samaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Nkasi wanapata umeme kutoka nje ya nchi, lakini mradi wa Gridi Imara unapeleka Gridi ya Taifa katika Mkoa wa Katavi ambao utafika pia katika Mkoa wa Rukwa na maeneo hayo. Kwa hiyo, ndani ya miezi kama 18 tatizo hili litakwisha kwa sababu tutakuwa tumefikisha umeme wa gridi kwenye maeneo hayo ambao ni umeme wa uhakika na ambao tunaweza tukau-*control* sisi wenyewe katika maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Gwajima, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini sasa mtaweza kufunga *transformer* mliyokuwa mmeahidi tangu Desemba ili kupunguza adha ya kukatikatika umeme kwenye Jimbo la Temeke? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dorothy Kilave, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *transformer* iliyotakiwa kuwekwa katika eneo la Temeke ipo katika mchakato wa manunuzi kwa sababu tayari pesa ilishatengwa na uamuzi ulishafanyika, hivyo katika miezi miwili au mitatu inayokuja tunaamini taratibu za manunuzi zitakuwa zimekamilika na *transformer* itafungwa kwa ajili ya kuongeza uwezo wa umeme katika maeneo hayo kuweza kuwahudumia wananchi wote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kavejuru, swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni lini Serikali itapeleka umeme katika vitongoji 192 katika Wilaya ya Buhigwe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kavejuru, Mbunge wa Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *REA III Round II* ambao unaendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali tuliyokuwa nayo unaendelea kupeleka umeme katika vitongoji mbalimbali ambavyo vimo ndani ya vijiji. Pia, upo mradi wetu wa *densification* (ujazilizi awamu ya pili) ambao pia unaendelea kupeleka umeme kidogo kidogo katika maeneo ya baadhi ya vitongoji. Kwa awamu hii tuna vitongoji kama 2,630.

Mheshimiwa Spika, ili kumaliza tatizo hili la umeme katika vitongoji, Serikali ipo katika taratibu za kutafuta fedha takribani shilingi 6,500,000,000,000 kuhakikisha kwamba

inapeleka umeme kwa mkupuo mmoja katika vitongoji vyote, takribani kama 36,000 tulivyokunavyo Tanzania Bara ambavyo havijafikiwa na umeme. Tunaamini mradi huu utakamilika na katika miaka mitatu au minne au mitano ijayo vitongoji vyote vitakuwa vimepata umeme.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mafinga tunaishukuru Serikali kwa kutufikishia umeme katika kila kijiji, hata hivyo vitongoji vingi havina umeme: Je, ni lini vitongoji vitaanza kupata umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge wa Mafinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika swali lililotangulia la Mheshimiwa Kavejuru, Serikali ipo katika mpango mkakati mkubwa sana wa kutafuta fedha kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote takribani 36,000 ambavyo vimebaki Tanzania Bara ambavyo havijapatiwa umeme kwa mradi utakaogharimu karibia Shilingi 6,500,000,000,000/=. Kwa hiyo, taratibu zitakapokamilika kila eneo linalohitaji umeme litafikishiwa miundombinu ya umeme katika vitongoji vyetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri matatizo ya mkandarasi wa *REA* aliyepewa *tender* ya kusambaza umeme kwenye Mkoa wa Songwe unayafahamu. Mpaka sasa hivi katika ya vijiji 127

amepeleka umeme kwenye vijiji 48 tu: Sasa hamwoni wakati umefika wa kuvunja naye mkataba kunusuru Mkoa wa Songwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Mwenisongole, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna baadhi ya maeneo ambapo Wakandarasi wetu hawajafanya vizuri. Tunachokifanya kikubwa ni kuhakikisha tunawasimamia kwa karibu kuhakikisha kwamba kazi zao zinakamilika kwa wakati. Katika eneo la Songwe, tumekuwa tukilifuatilia kwa karibu na Mheshimiwa Mwenisongole na tunamhakikishia kwamba ndani ya muda stahiki mradi huo utakamilika.

Mheshimiwa Spika, katika wale Wakandarasi ambao wako nyuma sana na hatuna namna, tutavunja mikataba yao, lakini wale ambao wanaweza kufanya kazi na kuikamilisha kwa wakati, tutasimamia vizuri ili tuweze kuikamilisha kwa wakati kwa sababu kuvunja mkataba pia siyo *option* nzuri ya kukamilisha mradi kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali ilituahidi kutuletea mkandarasi kwa ajili ya kukamilisha vitongoji 47 vilivyoko ndani ya Jimbo la Hai: Ni lini mkandarasi huyo ataanza kazi ya kukamilisha kwenye vitongoji hivi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli taratibu za kumpata mkandarasi wa kwenda kukamilisha umeme katika maeneo ya Hai na maeneo mengine ya Kilimanjaro ambayo yalikuwa yameshamaliza *level* ya vijiji yanaendelea na tunaamini katika miezi miwili ijayo Mkandarasi atakuwa amepatikana, na ataenda kuingia *site* sasa kuweza kupeleka umeme katika maeneo hayo ambayo yalikuwa hayajafikiwa na umeme.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Vijiji vingi katika Kata za Narurango, King'ori, Majengo bado havijapata Umeme wa *REA* na Mkandarasi anavyofanya kazi yake wala haeleweki, analeta nguzo, anaondoka…

**SPIKA:** Swali!

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Umeme wa *REA* utafika kwenye hizo kata ili vijiji vyote vipate umeme kulingana na ahadi ya Serikali kwamba mwisho wa mwaka huu vingepata umeme? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumetoa ahadi ya Serikali, tutahakikisha kwamba wakandarasi wote wanaotekeleza mradi wa *REA III Round II* kufikia Desemba

mwaka huu kazi hizo zitakuwa zimekamilika katika maeneo ambayo yanapelekewa umeme kwenye kata, vijiji na vitongoji ili wananchi waweze kunufaika na hiyo huduma ya umeme ambayo iko katika huo mradi mkubwa wa mwisho wa kupeleka umeme katika vitongoji na vijiji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri kuna tume mliunda ya kupitia vijiji vile vyenye sura ya miji hivi: Lini tume hii itamaliza kazi ili wananchi wajue wako wapi kwenye kuunganishiwa umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa OleleKaita, Mbunge wa Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tume iliundwa na ilipita kwenye baadhi ya maeneo kukusanya maoni na tulielekeza ihakikishe inamuona kila Mbunge. Majibu yalipokuja Wizarani tulivyojaribu ku-*crosscheck* na Waheshimiwa Wabunge tuligundua kuna Wabunge kwa bahati mbaya hawakufikiwa na hawakuonwa na timu hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeiagiza irudie upya zoezi hili kwenye yale maeneo ambayo ilikuwa haikufika na katika miezi miwili inayokuja tunaamini itakuwa imemfikia kila Mbunge na kupata maoni yake kwenye maeneo ambayo yanatakiwa kufanyiwa jitihada za kuhakikisha maeneo yenye uso wa mjini lakini ni vijijini yanapatiwa umeme kwa gharama ile nafuu. Kwa hiyo, majibu yatakapofikia mwisho tutaleta taarifa sahihi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Afya Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 72

**Hitaji la kupitia upya masharti ya fomu za Bima ya Afya**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapitia upya masharti ya fomu za bima ya afya ili kuondoa upotevu wa fedha za Vituo vya Afya kwa kushindwa kujaza fomu hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA,** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini na Balozi wa Afya ya Akili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, makato ya madai ya bima ya afya kwa watoa huduma za afya hayasababishwi na vipengele vilivyoainishwa katika fomu za bima ya afya (Fomu 2*A* na *B*). Sababu za Makato ya madai husababishwa na:-

(i) Kutozingatiwa kwa miongozo ya Tiba nchini inayotolewa na Wizara ya Afya;

(ii) Baadhi ya watoa huduma kuwasilisha madai yenye udanganyifu katika utoaji wa huduma;

(iii) Kutozingatiwa kwa bei zinazoainishwa katika Mkataba wa Huduma baina ya Mfuko na Watoa Huduma; na

(iv) Kutozingatiwa kwa taratibu za uwasilishaji wa madai ulioainishwa na Mfuko kwa mujibu wa Mkataba.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza, nashukuru kwa majibu yaliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Katika Hospitali yetu ya Mkoa wa Iringa imefungwa mashine ya *CT-scan* na inatoa huduma kwa wagonjwa wote isipokuwa wagonjwa wa bima ya afya kwa sababu *NHIF* wameshindwa kutoa kibali cha wagonjwa kupata huduma hizo. Swali langu ni kwa nini hawataki kutoa kibali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; gari ya chanjo ya Manispaa ya Iringa ni ya mwaka 1998, imekwenda zaidi ya kilometa 380,000 na zaidi na hatuna gari, gari imechakaa kabisa. Ni lini tutapata gari hiyo ili wananchi waendelee kupata huduma za chanjo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kusema kwamba Rais wetu alipopokea nchi kwenye Tanzania nzima ni hospitali mbili tu za mikoa zilikuwa na *CT-scan* na kwa sasa hospitali zote za mikoa zimepelekewa *CT-scan* na zimebaki nne za ziada maana yake Rais wetu amefanya kazi kubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tusingefurahi mtu yeyote awakoseshe Watanzania hiyo huduma ambayo Rais wao

amepeleka. Kwa hiyo, niseme tu kwa niaba ya Waziri wa Afya nimuagize *DG* wa Bima kwamba mpaka kesho saa mbili watu wa Iringa ambao wanastahili kupata huduma na waliotimiza vigezo waanze kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, swali lako la pili ni kwamba gari; tumezungumzia hapa tukasema zimenunuliwa *Ambulance* zaidi ya 727 maana yake hata Iringa itaenda kupata gari na tutaenda kuwekeza kwenye eneo hilo ambalo unasema ambalo ni muhimu sana la chanjo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, ni lini bima ya afya watasajili vituo vipya vya afya kikiwemo cha Ng'uluhe, Ruaha Mbuyuni, Ilula pamoja na Nyalungu ili waweze kuanza kupata huduma watu kupitia mfuko wa bima ya afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri inabidi uitwe kwanza ndiyo utoe majibu. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ninachoweza kukwambia ni kwamba ninakuomba tukae chini leta vituo vyako ambavyo havijasajiliwa tutizame vigezo, vikikidhi vigezo zianze kusajiliwa na huduma itolewe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 73

**Mabasi ya abiria yanayolazimishwa kulala Wilaya ya Sikonge**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuruhusu Mabasi ya Abiria yanayopita Wilayani Sikonge kuendelea na safari badala ya kuyalazimisha kulala?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Masauni, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**, alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Taska Mbogo Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mabasi ya abiria yanayokwenda Mpanda Mkoa wa Katavi ambayo yanapita Wilaya ya Sikonge zaidi ya saa nne usiku hushauriwa kulala Sikonge kwa sabubu za kiusalama. Eneo hilo lina pori la hifadhi kuanzia Sikonge hadi Inyonga lenye urefu wa kilometa 161 na halina mtandao wa mawasiliano. Hivyo si salama kupita nyakati za usiku mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuepuka adha ya kutakiwa kulala Sikonge, wamililki wa mabasi ya abiria wanashauriwa kupanga safari zao ili wapite katika maeneo hayo yenye changamoto mapema zaidi. Mabasi hayo yanaweza kuomba kuanza safari zao hasa kutoka Dar es Salaam saa tisa au saa kumi Alfajiri na Serikali itaafiki maombi yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Taska Mbogo swali la nyongeza.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa eneo la kutoka Sikonge kwenda Inyonga lenye kilometa 161 halina mawasiliano. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kunakuwepo na usalama kwenye eneo hilo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika majibu yake amesema kwamba wamiliki wa mabasi wanaweza kuomba kuondoka, kuanza safari zao pale Dar es Salaam muda wa saa tisa usiku au saa kumi. Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari kutoa tamko hapa Bungeni kwamba mabasi hayo yanaweza kuanza safari muda wa saa tisa au saa kumi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Taska Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mkakati ambao tunao katika kuhakikisha eneo hilo linakuwa salama. Kwanza nikupongeze wewe binafsi kwa kuweza kutupatia changamoto ya kufikiria kuanza usafirishaji wa mabasi ya abiria usiku.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kutekeleza maagizo Mheshimiwa Spika na maombi ya Waheshimiwa Wabunge tumeshaanza kulifanyia kazi suala hilo.

Mheshimiwa Spika, tumekaa na Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi ambao ndiyo wadau wakubwa kuangalia jinsi ya kuweza kufanya na tumeamua kulipa majukumu Baraza la Usalama Barabarani la Taifa ambalo limesheheni wajumbe ama wadau kutoka taasisi muhimu ikiwemo Jeshi la Polisi, *LATRA, TANROADS* na kadhalika ili wataalam hawa waweze

kutushauri namna bora ambayo itaweza kusaidia kuruhusu magari haya kuweza kutembea usiku ikiwemo hili eneo ambalo umeliruhusu.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mambo ambayo tunategemea kutoka kwa wataalamu hawa ni jinsi ya kuweza kudhibiti changamoto zilizopelekea maamuzi ya Serikali mwaka 1990 kuzuia ambayo ilikuwa ni mambo mawili makubwa.

Mheshimiwa Spika, moja; ilikuwa ni kutokana na changamoto ya ujambazi na utekaji kipindi hicho; pili; ilikuwa ni ajali ambazo zilikuwa zikitokea usiku na kuharibu maisha ya Watanzania wengi.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi; tunataka kuhakikisha kwamba wakati ambapo tunalitafakari jambo hili tutakaporuhusu tuweze kuhakikisha kwamba mabasi haya yanaruhusiwa kusafiri lakini wananchi wetu wanaendelea kubakia salama. Hivyo Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba jitihada hizi za kuhakikisha kwamba eneo hilo na maeneo mengine nchi nzima yanakuwa salama kuruhusu usafiri wa usiku yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusu tamko; kama ambavyo nimezungumza kwamba tunaomba nitoe tamko kwamba wale ambao wanaona kuna haja ya kuanza safari zao mapema basi walete maombi na tamko ni kwamba tutaridhia maombi hayo kwa wale ambao watakuwa na haja ya kuanza safari hizo wakati tunaendelea na jitihada hizo za kutafutia ufumbuzi wa kudumu suala hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri maombi anakuwa analeta nani, mmiliki wa chombo cha usafiri au unaleta mkoa husika au nani analeta hayo maombi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, maombi yawasilishwe na wenye vyombo vya usafiri ama wamiliki wa mabasi hayo ambayo yanahitaji kusafiri kwa nyakati hizo.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Mabasi ya abiria yanayosafiri kutoka Mkoa wa Dar es Salaam kwenda Mkoa wa Kagera na Nchi jirani ya Uganda kupita Wilaya ya Misenyi hulazimika abiria kulala katika Mji wa Kahama na wananchi kupata adha kubwa usiku kucha.

Mheshimiwa Spika, katika Pori la Biharamulo kuna vituo vya polisi vingi kila baada ya kilometa chache ambayo ni pongezi kubwa kwa Serikali.

Je, ni lini sasa mabasi yanayotoka katika Mkoa wa Dar es Salaam kwenda Mkoa wa Kagera na Nchi ya Uganda kuruhusiwa kusafiri mpaka kufika bila wananchi kulala njiani na kupata adha kubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kyombo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake linafanana na swali ambalo la msingi ambalo Mheshimiwa Taska Mbogo ameuliza. Hivyo niombe majibu ambayo nimeyajibu kwenye swali la msingi yaendelee kubakia hivyo hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi. Sheria zilizopo sasa Tanzania mabasi na malori yanatembea mchana na malori ndiyo yanayotembea usiku lakini duniani kote mabasi yanatembea muda wote, malori yanatembea mchana mwisho saa 12:00. Je, ni lini na sisi Tanzania tutakwenda na utaratibu ambao uko duniani ili twende na wenzetu katika maendeleo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahaya Massare kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo ni kuhakikisha kwamba shughuli za uchumi zinaendelea kufanyika nyakati zote. Tunaamini kabisa kwamba mabasi na malori na magari yote yakiweza kutembea masaa 24 yatachangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hivyo siyo suala la kusema yupi ni bora kuliko mwingine lakini changamoto ambayo nimeizungumza ni kwamba lazima tutakapofanya hivyo tuzingatie usalama wa wananchi wa nchi yetu na tumegundua kwamba mabasi na malori ndiyo ambayo ni visababishi vikubwa vya ajali. Nitatoa mfano wa ajali zilizotokea hivi karibuni ajali ambayo imetokea pale Tanga hivi karibuni ambayo iliua takribani Watanzania 20 ilikuwa ni kati ya lori na basi tena nyakati za usiku. Ajali iliyotokezea hapa Kongwa halikadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *concern* ya Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine kuona kwamba huduma hizi zinaweza kuimarishwa na kutoa nafasi kwa wananchi wetu kuweza kutoa mchango wao katika

uchumi wa nchi yetu kwa ufanisi zaidi tumezipokea na tutazifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza mikakati hiyo imeshaanza na tuvute subira pale ambapo wataalam wetu watatushauri utaratibu bora zaidi wa kufanya basi tuweze kuruhusu mabasi hayo yaweze kutembea muda wote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 74

**Fidia kwa wananchi wa Kata ya Moshono katika barabara ya mzunguko ya kona ya Kiseriani Arusha**

**MHE. MRISHO M. GAMBO** aliuliza:-

Je, lini Wananchi wa Kata ya Moshono katika barabara ya mzunguko ya Kona ya Kiserian watalipwa fidia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi walioathirika na kupisha ujenzi wa barabara ya mzunguko *(Arusha bypass)* kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mashaka Mrisho Gambo swali la nyongeza.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza sikubaliani na majibu ya Serikali kwenye swali langu la msingi kwa sababu ukizingatia kwamba sheria ni mwaka 2007, leo ni mwaka 2023 miaka 16 sasa bado Serikali inasema inatafuta fedha na huku wameweka vigingi kwenye maeneo ya wananchi lakini ingekuwa ni mwananchi ndiyo ameingilia kwenye hilo eneo Serikali ingeenda kumwondoa kwa nguvu. Baada ya maelezo hayo naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, ni lini sasa Serikali itawalipa fidia wananchi hawa? Swali la pili, kama Serikali haina uwezo wa kulipa fidia, kwa nini isiwaruhusu wananchi hawa wakaendeleza maendeleo hayo mpaka watakapokuwa tayari kuwalipa fidia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kulipa wale wote ambao waliathirika na ujenzi huu wa *Arusha Bypass* kwa maana hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Arusha waendelee kuwa na subira wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wananchi waruhusiwe kujenga maeneo haya. Nchi yetu inaongozwa kwa mujibu wa sheria na taratibu na sheria ya kuhifadhi barabara ambayo ilianza tangu mwaka 1932 enzi za ukoloni na

ikarudiwa mwaka 1967 na tukatunga sheria mpya mwaka 2007 ambayo inataka hifadhi ya barabara kutoka kati kati ya barabara mpaka upande wa pili iwe mita 30 na kutoka kati kati tena upande mwingine iwe mita 30 kwa maana ya kwamba jumla ni mita 60.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wote kwamba sheria hii lazima tuilinde na ikizingatiwa kwamba Arusha ni mjini tunahitaji pia kuendeleza miundombinu mizuri pale Arusha ili jiji hili la kitalii na kwa maana hiyo tuna hakika tukifanya vizuri katika suala la miundombinu hata watalii pia wataongezeka zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 75

**Kuimarisha matumizi ya kibenki kutumia bando za simu**

**MHE. JUDITH S. KAPINGA** aliuliza:-

Je, ni upi mkakati wa kurahisisha matumizi ya Kibenki kwa njia ya Simu kwa kutumia bando za simu badala ya salio la simu la kawaida?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliana na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika kurahisisha matumizi ya Kibenki kwa njia ya Simu kwa kutumia Bando za Simu badala ya salio la Simu la kawaida, utaratibu umewekwa kwamba unapokuwa na kifurushi cha *data* unaweza kutumia huduma za kibenki zinazotumia programu tumizi kama *SIM Banking App* na nyinginezo ili kuweza kupata huduma za kibenki.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo mtumiaji anatumia namba fupi fupi *(USSD)* ambazo ni huduma za ziada, mtumiaji anaweza kulipishwa ama kutolipishwa gharama za ziada; suala hili linategemea makubaliano kati ya benki na watoa huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza wigo wa matumizi ya fedha, Msimamizi wa huduma za kifedha anaweza kuwaelekeza watoa huduma za kifedha kuingia mikataba na watoa huduma za mawasiliano, badala ya kuwalipisha wanaotumia namba fupifupi kwenye huduma za kifedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga swali la nyongeza.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naipongeza Serikali kwa majibu mazuri, hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna *double standard* baadhi ya makampuni yameondoa utaratibu wa kutumia salio la kawaida unapoingia kwenye *menu* za kibenki na makampuni mengine bado yanataka utumie salio la kawaida badala ya bando ulilonalo kwenye simu. Serikali haioni umuhimu wa kuhakikisha makampuni yote yanatoa huduma hii kwa usawa kwa kuondoa utaratibu wa kutumia

salio la kawaida ili Watanzania wote waweze kunufaika na kurahisisha matumizi yao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Pamoja na Serikali kusitisha gharama ya ongezeko la bando tokea Oktoba mwaka jana, kwa sasa hivi tatizo kubwa tulilokuwa nalo ni bando za kwenye simu zetu tunazoweka kuisha kwa kasi ya haraka sana. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuhakikisha inaweka utaratibu maalum kwa ajili ya ku-*regulate* matumizi ya kasi za bando kwenye simu kama ilivyo *limit* kupanda gharama za matumizi ya bando kwenye simu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Judith Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kibiashara ni kama ambavyo nimejibu kwenye swali langu la msingi. Ni makubaliano kati ya mtoa huduma na benki na pale ambapo watoa huduma wanabadilisha wengine wanakuwa hawatozi ni masuala ya kiushindani ambapo sisi kama Serikali kazi yetu ni kuweka mazingira wezeshi ili ushindani uweze kutokea.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo unapotumia *USSD*, *USSD* maana yake si suala la kutuma meseji na kupokea, ni suala ambalo linakuwa linatoa *options* zingine ambazo mtumiaji anaweza kuona, na kuna hatua nyingi ambazo zinafanyika. Kwa hiyo, suala la kutumia bando ili uweze kukata huduma ya *USSD* inakuwa ni ngumu ni sawasawa na pale unapojiunga na bando halafu ukajaribu kupiga simu nje ya nchi. Hilo ni jambo haliwezekani, labda kama itawezekana tutakaa na watoa huduma ili tuangalie

kama kuna uwezekano wa kuwepo na bando la *USSD* ili liweze kuhudumia huduma maalum.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili suala la kasi katika matumizi ya bando, kasi ni matumizi ya mtumiaji husika. Kama ana vitu vingi vya ku-*download* na kuna vitu vingi vya ku-*upload* matokeo yake ni kwamba kasi ya bando ambalo atakuwa amejiunga litaisha mapema. Kwa hiyo, naendelea kushauri kwamba watumiaji wa bando waweze kuangalia matumizi halisi katika simu zao na pale ambapo wanakuwa hawatumii basi waweze kuzima data ili data isiweze kuisha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani Mbunge wa Singida Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 76

**Kukamilisha Miradi ya Umwagiliaji Singida Kaskazini**

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza: -

Je, lini Miradi ya Umwagiliaji katika Vijiji vya Msange na Mnghamo – Singida Kaskazini itakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa niaba ya Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Ighondo Ramadhani Mbunge wa Singida Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mwaka wa fedha 2023/2024 imetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi wa Mughamo na kuanza ujenzi wa bwawa na miundombinu mingine ya umwagiliaji katika Skimu ya Msange.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi kwanza nitoe shukrani na pongezi kwa majibu mazuri na ambayo yanaenda kutoa matumaini kwa wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini ambao wanasubiri skimu hizi kwa hamu kubwa.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; katika Skimu ya Msange wananchi wanatumia mfumo wa mafuta, yaani *diesel,* kwa ajili ya kuendesha kilimo cha umwagiliaji na tayari wananchi wameshatuma maombi kwa ajili ya kubadilishiwa mfumo kwenda…

**SPIKA:** Swali.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali iko tayari sasa kuwasaidia wananchi kubadilisha mfumo kutoka kwenye *generator* ili waepuke mafuta mengi na sasa watumie umeme?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna Bwawa la Mgori pamoja na Kisisya ambayo yamejaa tope na mifumo ya umwagiliaji imeharibika;

Je, Serikali iko tayari sasa kwenda kuyafufua mabwawa haya ili yaweze kuwasadia wananchi kuongeza kipato katika kilimo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa niaba ya Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, Mbunge wa Singida Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Kilimo itakaa pamoja na Wizara ya Nishati ili kuhakikisha wanafanikisha jambo hili kuondoa wananchi kutoka kwenye *generator* kwenda kwenye umeme. Kwa hiyo, hilo tutakaa pamoja ili kulifanikisha hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bwawa la Mgori na Kisisya ambayo yamejaa tope na yanahitaji kufufuliwa, nimhakikishie tu, kwamba nimezungumza na Waziri wa Kilimo na Wizara ya Kilimo itawatuma wataalam wake waende kufanya tathmini ili waweze kutafuta fedha kwa ajili ya kazi hiyo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere Mbunge wa Bunda sasa aulize swali lake.

Na. 77

**Kupata mkopo wa masharti nafuu**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kupata mkopo wa fedha wa muda mrefu kwa masharti nafuu ili kulipa madeni sumbufu ya awamu zote sita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Ahmad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kusimamia deni la Serikali kupitia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134 iliyobainisha vigezo vya kuzingatia wakati wa kutafuta fedha za mikopo kutoka ndani na nje ya nchi ili kugharamia shughuli za Serikali, hususan miradi ya maendeleo. Sheria hiyo pia inatumika kama nyenzo ya kudhibiti ongezeko la deni la Serikali kwa kulipa mikopo iliyoiva na kutoa kipaumbele kwa mikopo yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha awamu zote sita Serikali imeendelea kukopa na kulipa mikopo kulingana na mtiririko wa malipo kwa kila mkopo na hakuna mikopo ambayo Serikali imeshindwa kulipa. Aidha, malipo ya madeni yote ikiwemo madeni sumbufu yanaendelea kulipwa kupitia mpango na bajeti za Serikali za kila mwaka, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kama inavyoonesha, kwamba kila mwaka na kila muda tunalipa Deni la Taifa ni kwa nini sasa Deni la Taifa halioneshi dalili ya kupungua ilhali kila mwaka tunalipa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni lini sasa Serikali italeta mchanganuo wa madeni yote tunayodaiwa kama nchi ili Wabunge tupate fursa ya kushauri katika ulipaji wa madeni hayo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya kimkakati iliyo mikubwa nchini kwetu. Tunarejesha fedha lakini tuna uhitaji mkubwa tunaendelea kukopa.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, Serikali inawasilisha taarifa ya madeni yake kwenye Kamati ya Bajeti kila mwaka na kila inapohitajika. Tunaishukuru sana Kamati ya Bajeti kwa miongozo yake inayotusaidia kuendelea kufanya deni letu kuwa himilivu, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana; Mheshimiwa Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, madeni si tatizo, tatizo ni matumizi mazuri ya fedha inayopatikana kutokana na madeni.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba, kwa nini Wizara ya Fedha imeshindwa kutoa mkataba mdogo tu wa kuhamisha majengo ambayo yalikuwa yanatumiwa na

*consultant* wa *TANROADS* kuwapa Halmashauri ya Nyasa ili yatumike vizuri badala yake yanachakaa mpaka leo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Manyanya nadhani hilo upeleke kama swali la msingi kwa sababu sioni ni namna gani linahusiana na ulipaji wa madeni. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Yahaya Omar Massare Mbunge wa Manyoni Magharibi sasa aulize swali lake.

Na. 78

**Kupanda mazao yanayopendwa na wanyama hifadhini**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kupanda Hifadhini mazao yanayofuatwa na wanyama waharibifu kutoka Hifadhi za Rungwa, Muhesi na Kizigo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mary Masanja majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto ya ongezeko la matukio ya wanyamapori kuingia kwenye makazi ya watu na kusababisha madhara kwa wananchi na mali zao. Changamoto hiyo imesababishwa na uanzishwaji wa shughuli za binadamu kwenye shoroba, maeneo ya mtawanyiko wa wanyamapori na maeneo ya pembezoni

mwa hifadhi. Maeneo hayo hutumiwa na wanyamapori wanaohama kutoka katika mfumo mmoja wa ikolojia kwenda mfumo mwingine kwa ajili ya kutafuta maeneo ya malisho, maji, mazalia, ulinzi na mapumziko kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hiyo ya kiikolojia, upandaji wa mazao katika hifadhi za wanyamapori hauwezi kuzuia wanyamapori kuhama kutoka mfumo mmoja wa ikolojia kwenda mfumo mwingine.

Vilevile upandaji wa mazao hifadhini ni ukiukwaji wa sheria za uhifadhi kwa kuwa wanyamapori wanaishi katika mazingira asilia ambapo mimea mingine ambayo siyo ya asili hairuhusiwi ndani ya hifadhi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Itigi baada ya kuliwa mazao yao na hawa wanayama wanategemea kile kidogo ambacho Serikali imekiweka kwenye sheria ikiwemo kifuta machozi na kifuta jasho;

Je, ni lini sasa watamalizia kulipa wananchi ambao wameliwa mazao yao miaka miwili iliyopita?

Mheshimiwa Spika, swali la pili Serikali imegawa pori kubwa la akiba la Rungwa, Muhesi na Kizigo kuwa mapori yanayojitegemea. Rungwa peke yake, Muhesi peke yake na Kizigo peke yake. Muhesi imepakana sana karibu na vijiji vingi vya Itigi;

Je, ni lini sasa wataongeza askari wa wanyamapori ili angalau waweze kuwadhibiti hawa wanyama wanapotoka kule kuingia kwenye makazi ya watu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni mwezi wa tatu tumemaliza kulipa kifuta jasho na kifuta machozi katika Wilaya ya Manyoni hususan katika maeneo ya Vijiji vya Njiri, Rungwa, Sanjaranda na Itigi Mjini ambao walipata madhara makubwa ya wanyamapori wakali na waharibifu. Hivyo nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba kwa sasa hivi tumeshafanya tathmini kwa wale ambao wamebaki tutawalipa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la askari, tumeshaomba tayari kuongezewa tena kwa mwaka huu askari waajiriwa ambao tayari tumeshapata kibali tunaamini kwenye maeneo ambayo yana changamoto za wanyama wakali na waharibifi tutaendelea kuongeza nguvu na vituo kujengwa ili angalau tupunguze athari hii ya wanyama wakali na waharibifu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa Mbunge wa Handeni Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 79

**Ujenzi wa Bwawa la Mandela Kwenjugo na Kamkole Mabanda - Handeni**

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Bwawa la Mandela Kwenjugo na Kamkole Mabanda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji Mhandisi Maryprisca Mahundi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa Mbunge wa Handeni Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma ya maji Wilayani Handeni, Serikali ipo kwenye hatua za mwisho za usanifu wa Mabwawa ya Mandela – Kwenjugo na Kamkole – Mabanda na usanifu huo utakamilika mwezi Juni, 2023. Ujenzi utaanza katika mwaka wa fedha 2023/2024. Kukamilika kwa ujenzi wa mabwawa hayo kutanufaisha wananchi wapatao 11,004 wa mitaa ya Mabanda, Komoza, Kwenjugo, Ngugwini, Bwila, Kwedisewa na Kwedigongo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, swali la nyongeza.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; hivi sasa ipo mitambo ya Serikali kupitia *DDCA* inayochimba Bwawa la

Kwenkambala na kwa Mahizi. Kwa nini Serikali isiibakishe mitambo hii ndani ya Wilaya ya Handeni itakapokamilisha Kwenkambala na kwa Mahizi ili iendelee kuchimba mabwawa hayo mawili ambayo unayazungumzia Mheshimiwa Naibu Waziri?

Mheshimiwa Spika, swali la pili mradi wa *HTM* mkandarasi tayari amekwishapewa msamaha wa kodi na alikwishakamilisha usanifu. Ni lini mkandarasi huyu atakuwa *site* kuanza ujenzi mara moja kwa mradi huu mkubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa Mbunge wa Handeni Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mitambo kubaki Handeni hakuna tatizo tutahakikisha inabaki mpaka imalize kazi. Kuhusu mradi wa *HTM* lini utaanza tayari, mkandarasi anapaswa kuwa *site;* kwa hiyo baada ya hapa Mheshimiwa Mbunge tuonane ili tufatilie kwa pamoja kuhakikisha mkandarasi anakuwepo *site*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Ninayo matangazo hapa mbele na mambo mengine ambayo yanahitaji ufafanuzi.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tena tusikilizane na wanaotembea waketi. Jambo la kwanza, kabla sijaleta matangazo; Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akiwa anaingia Bungeni na kutoka Bungeni wako Wabunge husimama na wengine kutoka maeneo mengine husimama

pahala ili wamsalimie, jambo ambalo ni la heshima kabisa. Changamoto ni kwamba Waziri Mkuu anapokuwa anatoka muda ambao si mwisho wa Bunge maana yake kuna jambo anaenda kulifanya ili arejee. Sasa kama anakuwa amepigiwa simu na yeye hawezi kukwambia Mbunge samahani nawahi wewe umeshasimama pale unaanza kumweleza hoja zako na matatizo yako na kwa namna alivyo mstaarabu inabidi akusikilize. *(Makofi)*

Nilishalisema jambo hili huko nyuma nalirejea tena, akiwa anatoka maana yake liko jambo linalomfanya atoke muda huo. Na hapo kwenye kiti chake, ndiyo maana kuna kiti cha ziada, Mbunge yeyote mwenye hoja ambayo haina ulazima wa kukaa muda mrefu kiti kiko pale. Subiri Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa amekaa nenda kwenye kiti kamweleze hoja yako usimsimamishe njiani anapokuwa anatoka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wakati akiingia ukishatazama muda wa kuanza Bunge umefika mwache Mheshimiwa Waziri Mkuu awahi kwenye kiti chake; na ukiona tayari shughuli za Bunge zimeanza halafu Mheshimiwa Waziri Mkuu anaingia halafu unamsimamisha hiyo sasa inakuwa si heshima, kwa sababu yeye anawahi kwenye kiti chake ili shughuli za Bunge ziendelee akiwa ameketi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nia yako ni njema ya kumuheshimu Waziri Mkuu lakini sasa ukimsimamisha na yeye anashindwa kukwambia Mheshimiwa nawahi na mimi kwenye kiti. Ndiyo maana kiti kile kimeachwa pale ili Mbunge mwenye hoja anayoona ya dharura lazima amwambie Waziri Mkuu nenda kwenye kiti chake, usimsimamishe saa anayotoka, usimsimamishe saa anayoingia ikiwa Bunge limeshaanza. *(Makofi)*

Ninasisitiza, kwa sababu siku ya hoja yake wako watu mlimsimamisha huko, huku mbele akawa anakaa tu inabidi

aitwe kwa sababu ndiyo hoja yake; na mtagundua nilikaa kimya kwa muda kidogo ili kumpa nafasi akae. Maana siwezi kumwita sasa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu hebu kaa hoja yako inataka kuitwa. Sasa mmemsimamisha huko muda mrefu hoja yake inaitwa hapa inabidi ile amekiti tu hoja yake imeitwa inabidi aanze kutafuta mafaili kwenye begi. Kwa hiyo, hilo si jambo jema nadhani hilo linawezekana ndio maana mmewekewa kiti hapo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, na Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa ofisini anawaruhusu kabisa kwenda kumwona wala hana neno, kwa hiyo msimsimamishe njiani kuelezea hoja zenu. Hilo lilikuwa ni la kwanza. *(Makofi)*

Jambo la pili ni matangazo ya wageni na matangazo mengine na mambo mengine ya muhimu ambayo tutataka kuyazungumzia leo. Mheshimiwa Musukuma hapo kwenye kiti chako nisikilize kwa sababu huenda kuna hoja yako huku mbele.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika, wapo wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni viongozi wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na hawa ni Ndugu Saidi Yakubu ambaye ni Katibu Mkuu, karibu sana ambaye ameongozana na Ndugu Nicholausi Mkapa, Naibu Katibu Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Addo Komba, Kaimu Mkurugenzi wa Michezo, yupo pia Ndugu Neema Mshita ambaye ni Katibu-Baraza la Michezo la Taifa, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Wallace Karia Rais wa *TFF,* karibu sana; yupo pia Ndugu Athman Nyamrani ambaye ni Makamu wa Rais *TFF,* karibu sana; yupo Ndugu Mohamed Adem ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu Dodoma, karibu sana na yupo pia Ndugu Herman Kidifu ambaye ni Mwanasheria *TFF*, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pia wameambatana na viongozi na wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari ya *Fountain Gate* iliyopo Dodoma ambayo hivi karibuni wametwaa ubingwa wa michuano ya shule za sekondari kwa wasichana yaliyofanyika Durban, Afrika Kusini, karibuni sana, ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa vijana wetu wamefanya kazi nzuri sana, wametuheshimisha kama Taifa na kwa kweli hii inaonyesha dhahiri na hapa ni vizuri kwamba Katibu Mkuu yuko hapa, Waziri yupo na Naibu Waziri. Kwa kweli mzitazame tofauti hizi timu za wanawake katika ngazi zote kwa sababu sasa hivi sawa tunajua Simba na Yanga wanafanya vizuri kimataifa, lakini tunawatakia kila kheri kwamba na wao wamalize safari yao salama watuletee mambo kama haya. Kwa kuwa hawajaleta bado, basi timu hizi za wanawake mzitazame vizuri sana na hawa wameonyesha mfano mzuri, tunaamini huko baadaye tunaenda kuwa na kikosi kizuri sana cha timu ya wanawake, tunawatakia kila la kheri mabinti zetu na ninyi ambao mnawaongoza kutoka kwenye hii shule tunawashukuru sana kwa kazi nzuri mnayoifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wangu ambao ni wanafunzi 65 wa Umoja wa Vijana wa CCM, Tawi la *SUA* Mkoa wa Morogoro wakiongozwa na Mwenyekiti wao ndugu Laizer Sembata, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vilevile ninao wageni 76 ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya *(MUST)* wakiongozwa na Spika wao Ndugu Renatus Chitage, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge na hawa ni Wageni 50 wa Mheshimiwa Angelina Malembeka, ambao ni vijana, Viongozi wa Huduma ya Mtoto kutoka *Compassion International Tanzania*, Kata ya Misungwi, Jijini

Mwanza wakiongozwa na Ndugu Steven Lumulisha, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine 60 wa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar ambao ni akinamama wa JUWAKITA BAKWATA kutoka Jijini Dodoma, wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Fatuma Hussein, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa, Simon Songe ambaye ni mpiga kura wake kutoka Busega, Mkoa wa Simiyu Ndugu Anithia Semen, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Assa Makanika ambao ni viongozi wa CCM kutoka Kigoma Vijijini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Sylvia Sigula ambaye ni wifi yake kutoka Tabora, ndugu Janneth Byemerwa, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Jerry Silaa ambaye ni jamaa yake kutoka Jijini Dodoma Ndugu Joshua Molel. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 16 wa Mheshimiwa Muharami Mkenge ambao ni Wanafunzi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii mwaka wa tatu kutoka Kinondoni Jijini Dar es Salaam, karibuni sana sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiewa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao hapa Bungeni, ninalo Tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge. Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge, kwamba Benki ya *NMB* imeandaa *Iftar* maalum kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge. *Iftar* hii itafanyika katika Viwanja vya Bunge kesho siku ya Ijumaa 14 Aprili, 2023, kuanzia saa 12.30 jioni. Waheshimiwa

Wabunge na watumishi wote mnaalikwa katika *Iftar* hii bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, yako mambo ambayo yamejitokeza hapa Bungeni na hayo nataka niyatolee ufafanuzi sasa. Jambo mojawapo linahusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sasa kwa sababu hapa Bungeni tumekuwa na maelezo mengi wakati mwingine, mwingine anachangia, mwingine anampa taarifa, mwingine anatoa na maelezo ya ziada, lakini pia na huko nje wananchi wameipokea taarifa hii na wao wametoa mawazo mbalimbali sasa ni vizuri kuweka mwelekeo ili wote tuwe tunaelewana tunapokwenda na jambo hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba siku ya tarehe 4 Aprili, 2023, nilitoa maelezo hapa Bungeni kuhusu utaratibu wa Bunge kushughulikia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*. Aidha, mtakumbuka kwamba tarehe 6 Aprili, 2023 Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha mezani Taarifa mbalimbali za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hatua hiyo na kwa mujibu wa maelezo niliyoyatoa hiyo siku ya tarehe 4 Aprili, 2023, taarifa hizo sasa zipo mikononi mwa Bunge na pia mikononi mwa Kamati zile zinazohusu usimamizi wa fedha za umma nazo zinajipanga kuanza kushughulikia taarifa hizo kikamilifu na kupokea majibu ya Serikali kwa hoja zote, kuwaita wadau wote muhimu, kuwahoji na hatimaye kuandaa taarifa yake itakayowasilishwa Bungeni Mwezi Novemba, 2023. Pamoja na mambo mengine, umuhimu wa mchakato huu unatokana na ukweli kwamba nchi yetu inafuata misingi ya utawala wa kisheria ambapo haki ya kusikilizwa ni moja ya vipengele vyake muhimu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea Taarifa ya Kamati pamoja na maoni na mapendekezo, Bunge hili katika kutekeleza jukumu la kuisimamia Serikali litajadili kwa kina na hatimaye kutoka na maazimio ya Bunge kuhusu hoja mbalimbali zilizowasilishwa na *CAG*. Maazimio hayo yatawasilishwa Serikalini kwa utekelezaji ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua madhubuti za kisheria na kinidhamu kwa taasisi na maafisa wote watakaobainika kujihusisha na matumizi mabaya ya fedha za umma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa sheria za nchi yetu *CAG* anafanya kazi kwa niaba ya Bunge. Hivyo maoni na mapendekezo anayoyatoa na kukubaliwa na Bunge kisha kuwasilishwa Serikalini yanapaswa kutekelezwa ipasavyo. Katika kutekeleza hili, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge, kuwa Serikali imewasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge tuliyoyapitisha mwezi Novemba, 2022 kuhusiana na taarifa ya *CAG* ya mwaka wa fedha 2020/2021 ambayo taarifa hii Serikali imewasilisha kwangu nitatafuta muda nionane na Wenyeviti wa Kamati za Kisekta tuyapitie haya majibu ya Serikali halafu tuone wapi bado na wapi tayari. Kwa hiyo hii kazi inaendelea na msiwe na wasiwasi kuhusu hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matumizi mabaya ya fedha za umma yanaathiri maendeleo ya wananchi na Taifa zima kwa ujumla na Bunge ni taasisi inayokerwa na kuumizwa zaidi na jambo hilo kwa sababu tunafahamu matarajio ya wananchi kwa Serikali na tunafahamu pia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan anavyohangaika kupata pesa kwa ajili ya ustawi wa wananchi wetu. Hivyo, Bunge haliwezi kuacha kufanyia kazi kikamilifu mapendekezo yote yanayoletwa ama yanayotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hata hivyo, kwa kuwa moja ya misingi ya haki huwezi kuwa mwamuzi kwenye kesi yako mwenyewe, *CAG* amefanya kazi yake sisi ndiyo waamuzi

kuhusu taarifa hiyo na Serikali itatekeleza itakavyoagizwa na Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo niwasihi na wananchi wote tuziamini Kamati zetu zinazosimamia masuala haya ya fedha kwa maana ya *PAC* na *LAAC* kuwa zitatekeleza majukumu yao kikamilifu na wakati utakapofika Kamati hizo zitawasilisha taarifa zao Bungeni. Kwa sasa tujikite kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Hata hivyo, Mbunge hakatazwi kutumia taarifa hiyo lakini Serikali hailazimiki kujibu hoja hizo Bungeni hapa.

Waheshimiwa Wabunge, Sasa hilo tuelewane vizuri, ukiamua kuutumia muda wako wote Mheshimiwa Mbunge, kuchambua taarifa ya *CAG* ya mwaka 2021/2022 ni uchaguzi wako, lakini Serikali haitajishughulisha na hoja ulizozitoa mpaka Bunge litakapoamua kupeleka sasa Serikalini kwamba sisi kama Bunge tumemaliza kazi yetu, maazimio yetu na maamuzi yetu kuhusu taarifa ya *CAG* ni haya, hapo ndipo Serikali itachukua yale ambayo Bunge linaiagiza.

Sasa Mbunge unao uchaguzi kama utaamua kuchambua hii bajeti ya 2023/2024 na namna inavyoathiri Jimbo lako na wananchi waliokutuma hapa, unao huo uhuru, kama utaamua wewe kuchambua taarifa ambayo Bunge bado halijaifanyia kazi, lakini itakuja kufanya baadaye na Serikali hailazimiki kwa kweli kufanya kitu chochote kwenye taarifa hiyo kwa sasa kwa sababu Bunge hatujamaliza mchakato wetu, ni uamuzi wako.

Kwa hiyo nimeona nifafanue hili ili Wabunge, msilazimike kupeana taarifa. Mbunge anapoamua kutumia muda wake kuchambua taarifa ambayo Serikali haitampa majibu. Unamwacha amalize mchango wake aendelee, isipokuwa kama kuna upotoshaji, lakini kama anaitumia Taarifa ya *CAG*, mwache aitumie kwa sababu wananchi

wote wanayo na kila mtu anaisoma na wanaruhusiwa kuisoma. Pia hao wananchi wanaruhusiwa katika wale waliosoma kumwaambia Mbunge wao kwamba, Mbunge wetu kwenye hili sisi tunakutuma hivi, hiyo nafasi utapewa Mheshimiwa Mbunge mwezi Novemba. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na wananchi, msione kwamba ni muda mrefu, itakuwaje? Nimeshawaambia misingi ya haki na nchi yetu inaendeshwa kisheria kwa utawala wa kisheria lazima wale waliotuhumiwa, tuwasikilize na ziko nyakati ambazo wale waliotuhumiwa wataleta taarifa kwetu zenye vielelezo na tutasema hoja hii imekwisha na haitakuja hapa ndani, kwa maana ya mjadala, lakini tutaambiwa kwamba hoja hii imekwisha sisi tumejiridhisha *CAG* kasema hivi, lakini tumeletewa vielelezo, ufafanuzi wa Serikali tumeuelewa. Kwa hivyo wewe ukiamua kujielekeza huko ni suala lako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo, hayo yatakuwa ni maelezo binafsi uliyoamua wewe kuyatoa na wala usiwaambie Serikali, niliwahi kusema hapa Bungeni hamjalifuata jambo langu. Kwenye hoja ya *CAG* taarifa yake italetwa hapa Bungeni baada ya Kamati zetu kumaliza kazi zake na kuna watu walikuwa wanasema pengine kipindi hiki tuendelee, tuwape pengine muda kidogo Kamati hizi zifanye hiyo kazi, halafu zilete taarifa kabla hatujaanza kujadili bajeti, uhalisia ni kwamba wale Maafisa Masuuli ambao wanatakiwa kwenda mbele ya Kamati zetu hizi za Hesabu za Serikali ni wale wale ambao ndiyo wasimamizi wa bajeti kwenye hizi Wizara.

Kwa hiyo, hawawezi kufanya mambo mawili kwa wakati mmoja kwa ukamilifu. Hawezi kuwa yupo anasikiliza Wabunge wanachangia hoja ya Wizara yake wakati huo huo anaitwa na *PAC* au na *LAAC* kwenda kule kusikiliza. Kwa hiyo muda ule umepangwa vizuri kwa ajili ya kutoa fursa kwa wale Maafisa Masuuli kujiandaa na majibu wanapokwenda mbele ya Kamati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tusiwe na wasiwasi, wabadhirifu wa mali za umma watashughulikiwa ipasavyo kwa taratibu tulizojiwekea za kisheria na hakuna mtu anapaswa kuonewa. Kwa hivyo *CAG* yeye amefanya kazi yake na kama nilivyosema huwezi kuwa mwamuzi kwenye kesi yako mwenyewe. Taarifa ile ametuletea *CAG,* yeye hafanyi maamuzi juu ya ile taarifa tena na zile nyingi zinaweza kuwa na uhalisia na ndiyo ukweli, lakini nyingi zinahitaji maelezo ya ziada ndiyo maana zinakuja hapa Wabunge tushughulike nazo. Tunazojiridhisha zinaishia hapo, tusizojiridhisha tunaiagiza Serikali, huo ndiyo utaratibu. *(Makofi)*

Kwa hiyo wananchi siyo kwamba hawaruhusiwi kujadili, waendelee kujadili na sisi kama Wabunge, wao tunawasilikiliza, taarifa zao ni za muhimu, tutaendelea kutumia mawazo yao wanayo yatoa kadri muda unavyokwenda.

Waheshimiwa Wabunge, kwa ufafanuzi huo nimeletewa ujumbe hapa, kuna Mbunge ana Mwongozo tutamsikiliza halafu tutaendelea na ratiba yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu.

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuomba Mwongozo kwa Kanuni ya 76.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na mjadala mrefu sana katika Bunge letu hili kwa zaidi ya siku tatu, na Wabunge wamekuwa wakijadili sana kuhusu suala la ushoga na usagaji.

Mheshimiwa Spika, makundi mbalimbali yameweza kueleza juu ya jambo hili ikiwemo makanisa wameandamana kule Arusha, ikiwemo misikiti wameandamana kule Arusha, Mheshimiwa Rais ameshasema kuhusu jambo hili, Mheshimiwa Makamu wa Rais amesema kuhusu jambo hili, Mahakama imeshasema kuhusu jambo hili, lakini imebaki Bunge halijasema jambo lolote na ukizingatia kwamba Bunge hili limejadili kwa mapana sana kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Mwogozo wako kwa mijadala hii iliopo ndani ya Bunge hili na nje ya Bunge hili. Kwa hiyo, sasa ni wakati muafaka Bunge lako hili nalo kusema jambo kuielekeza Serikali kupitia mashirika yetu ya umma na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ikiwemo dini na mashirika yote yanayotoa elimu kuhusu ushoga Tanzania kuzuia jambo hilo, lakini pia kupitia fedha ambazo wanazipata kwa ajili ya kutoa elimu, lakini pia kuhakikisha kwamba Serikali imeleta muswada mahsusi kutokana na mapungufu ya sheria yetu ile ya kuzuia ushoga, Kanuni namba 16 ya Adhabu ili iweze kutungwa sheria ambayo ni mahsuisi kabisa kama nchi nyingine ya Uganda ili kuweza kuhakikisha kwamba jambo hili ndani ya jamii yetu linazuiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo kwa mjadala huu ulipo ndani ya Bunge hili na nje ya Bunge hili katika nchi yetu ili kunusuru Taifa letu na ushoga na usagaji ambao umekithiri kuanzia shule za msingi mpaka sekondari, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni yetu ya 76 inataka Mwongozo unaoombwa jambo liwe limetokea mapema siku hiyo hapa Bungeni, lakini hata hivyo jambo alilolizungumzia Mheshimiwa Lemburis Saputu Noah, ni jambo ambalo ni kweli limekuwa kwenye mjadala mrefu sana hapa Bungeni na imefikia pahala wako Wabunge nafikiri kwa hisia zile zikazidi sana wakawa wanatumia lugha pengine ambayo haipendezi sana kusemwa hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, kwa muktadha huo na mijadala ambayo imeendelea hapa ndani nafikiri ni kwa sababu hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya bajeti huwa inahusu mambo mengi na inahusu kimsingi mambo yote yaliyoko kwenye jamii. Lakini hata hivyo kwa namna mjadala wetu ulivyojadiliwa nafikiri sote tunakubalina kwamba jambo hili limeishasikika na limeishaeleweka, kwa maana ipi? Sote tumesikia wananchi wakilizungumzia lakini tumesikia viongozi wetu wakilizungumzia, viongozi wa dini, viongozi wa Kiserikali pia wamelizungumzia na kwa muktadha huo Serikali imeelewa kitu gani kinapaswa kufanyika kwenye jambo hili, lakini sote tunafahamu yako mambo ambayo sisi kwa ufahamu wetu tunayafahamu kwamba yanatokea sehemu nyingine, lakini hapa kwetu yapo ambayo ni mabaya sana, yanatokea huko kwingine, lakini kwetu hapa hayajafika.

Sasa nafikiri kadri tunavyozungumza na sisi tusijetukajikuta kwamba ndio tunayakaribisha hayo mambo kwa kufungua ule wigo wa kuyazungumza kwa namna pengine; moja kwa matumizi ya yale ya lugha kwa sababu chombo chetu hiki ni chombo cha wananchi, kwa hiyo wanatazama watu wazima na watoto, sasa lazima tufike mahali ambapo tunataka kufanya jambo ambalo litakuwa la faida zaidi kwa wananchi ambao tunawawakilisha kuliko kuleta uharibifu zaidi.

Kwa muktadha huo kwa kuwa nchi yetu inafuata utawala wa sheria na michango mingi imetolewa humu ndani ya mapendekezo hapa na pale, lakini iko michango mingi ambayo kimsingi ni ya malalamiko, yaani mtu analalamika kwamba jambo hili, jambo hili, jambo hili.

Sasa kwa muktadha huo sisi kama nchi kwa sababu sheria hutungwa kulingana na mazingira yetu na Sheria ya Makosa ya Kujamiiana, lakini pia Makosa ya Jinai inavyo vifungu mbalimbali vinavyohusu jambo hili. Sasa ikiwa yapo mapungufu kwenye hivyo vifungu ambavyo viko kwenye

sheria, tunayo Tume yetu ya Kurekebisha Sheria ambayo inaweza kulifanyia jambo hilo kazi. Na ili tutoke tukiwa tumeelewana vizuri na Waheshimiwa Wabunge mjue michango yenu mizito imeshachukuliwa na upande wa Serikali, mimi sasa kwa niaba yenu Waheshimiwa niiagize Serikali, Wizara ya Katiba na Sheria mkishirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini pia Wizara ya Maendeleo ya Jamii ambayo inashughulika pia na mambo haya, Mambo ya Ndani ya Nchi muone namna ya kufanya utafiti kupitia hii Tume yetu ya Kurekebisha Sheria, ufanywe utafiti ni mambo gani ambayo tunataka sasa hivi yaongezeke kwenye sheria, ili yale mapungufu yasiwepo, kwa sababu yapo mapungufu ya dhahiri ambayo yameelezwa na Waheshimiwa Wabunge hapa na ninyi mmeyasikia. *(Makofi)*

Yale mapungufu sasa ndio yazibwe mianya na ili hili jambo sasa litoke hapa Bungeni lije kwenu Serikalini mlifanyie kazi kashirikianeni na Tume hii ili wafanye utafiti kuhusu jambo hili kwa sababu sisi pia hatutataka tutunge sheria kwa mihemko, hapana. Tunataka kutunga sheria tukiwa tunaelewa tatizo ni kubwa kiasi gani kwenye jamii yetu. Maana watu hapa tu tunasema limeongezeka, kwa kiasi gani hatujui. Ni kubwa sana, je, ni kubwa sana kwa kiasi gani hatujui!

Kwa hiyo, ni muhimu Tume yetu ya Kurekebisha Sheria ifanye utafiti, ikishafanya utafiti basi upande wa Serikali huo utafiti utawapa sasa taarifa muhimu kuona namna ambavyo mabadiliko yaletwe hapa Bungeni ili Bunge lifanye kazi yake ya kurebisha sheria, yale mapungufu yaondoke na watoto wetu wakae salama, vijana wetu wakae salama na Taifa letu liwe salama. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa muktadha huo sasa kwa kuwa jambo hili limeshasikika, nadhani na leo Mheshimiwa Waziri Mkuu anahitimisha hoja yake; hoja zinazokuja tujikite

kwenye hoja za bajeti ambayo iko mbele yetu, lakini pia hoja ya utekelezaji wa bajeti ambayo inaendelea. *(Makofi)*

Kwa hiyo, jambo hili nadhani tutakuwa tumeshaelewana kwamba tumeshawakabidhi Serikali wakalifanyie kazi, Bunge kama chombo cha kutunga sheria, tutatunga sheria kulingana na taarifa hiyo ambayo wenzetu watakuwa wameipata na hivyo madhaifu yote mliyokuwa mmeyasema yatakuwa yanafanyiwa kazi na wakati huo sasa tutapata mjadala sasa hoja hii ndio itakuwa iko mezani, kwa hiyo tutaijadili tukiwa na taarifa kamili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa sasa kwa bajeti zijazo niwaombe tujielekeze kwenye hoja za kibajeti, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea, Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, ninayo majina hapa ya Wabunge walioomba kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mheshimiwa Asia Abdulkarimu Halamga, ajiandae.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii adhimu kutoa mchango wangu kuhusu bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Mwandishi mmoja Tanzania anaitwa Ndugu Godius Rweyongeza, aliandika katika Kitabu chake cha Rasilimali, tatizo si rasilimali fedha zinazopotea bali tatizo ni rasilimali watu tunazozipoteza. Maneno haya yamenifanya nitafakari sana kwa makini kuhusu ripoti za kila mwaka zinazowasilishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika ripoti hizo, mtakubaliana nami makosa yaleyale yanajirudia na pengine yanajirudia kwa sababu hakuna hatua madhubuti zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mawazo yangu kuna matatizo manne makubwa ya msingi na nitayataja ambayo Bunge lako tukufu linapaswa kuyasimamia na kuyafanyia kazi.

Kwanza, nchi yetu haina utaratibu mzuri wa kuandaa Viongozi wake. Mara nyingi watu wa kawaida tu bila ya kupewa mafunzo na maandalizi ya kutosha ya uongozi wanapewa dhamana ya uongozi, halafu matokeo yake tunalalamika Viongozi wanakosa maadili hawana uadilifu, hawana maadili ya uongozi kana kwamba maadili ya uongozi, uadilifu na uzalendo ni vitu tu ambavyo vinakuja bila maandalizi tunazaliwa navyo, hapana!*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo linalonisikitisha sana, tunapotafuta Wahasibu kwa mfano, tunatafuta watu ambao wana weledi, wana mafunzo ya kutosha, lakini watu ambao tunawapa dhamana wakisimamia Fedha za Taifa, rasilimali, mitaji, rasilimali watu hatuwapi mafunzo yanayohitajika. Kuna wakati Marehemu Baba wa Taifa alianzisha vyuo kwa ajili ya shughuli hiyo ya kuwatayarisha Viongozi wa Taifa hili. Kwa mfano, tulikuwa na Taasisi ya Uongozi ya Mzumbe, taasisi ambayo ilifanya kazi kubwa sana ya kuandaa viongozi mahiri, wenye weledi, wenye maadili, wenye uzalendo na mfano mzuri Hayati Moringe Sokoine, Mzee wetu alikuwa ni mhitimu wa Chuo hiki. Rais wetu wa sasa *Madam* Samia Suluhu Hassan, *Madam* Anna Makinda, hawa ni viongozi

wanaotokana na chuo hiki. Tunaweza kujua kwa kiasi gani Chuo hiki kilitoa mchango mkubwa sana wa uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tulikuwa na Chuo cha Kigamboni ambacho kilikuwa kimefanya kazi kubwa sana ya kuanda viongozi wa nchi hii, kwa bahati mbaya sana viongozi waliokuja baada ya Mwalimu Nyerere wamevifuta vyuo hivyo na vyuo hivyo sasa vimefanywa kuwa Vyuo Vikuu vinavyofundisha masomo ya kawaida. Ushauri wangu kwa Serikali, ninaiomba sana Serikali itafakari juu ya jambo hili la kuanzisha tena au kurudisha tena Vyuo vya Uongozi. Bila kuwatayarisha viongozi wetu hatuwezi kuwa na viongozi wenye ueledi, wenye uzalendo na wenye maadili.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nadhani linachangia katika kuwa na ripoti zisizoridhisha za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Wizara ya Elimu kila mwaka inatoa fedha kwa ajili ya kuwapatia mikopo wanafunzi wanaohitaji elimu ya Chuo Kikuu, kwa bahati mbaya sana wanafunzi hawa wanapewa elimu ambayo haiwasaidii kuwaajiri wala kuajiriwa. Unamkuta mwanafunzi ambae kwa mfano, amemaliza Shahada ya Utawala, amemaliza Shahada ya Utawala anakosa kazi, baadae badala ya kufanya shughuli ya maana utakuta sasa amejielekeza anatafuta ajira kwenye shughuli za utalii, ama anatafuta ajira kwenye shughuli za udereva. Sasa mimi nimekuwa nikijiuliza je, kama Taifa tunadhani haya ni matumizi sahihi ya rasilimali? Badala ya kufanya utafiti tukaangalia kwamba vijana wetu wanahitaji ujuzi wa aina gani tukawapa mafunzo ambayo yataweza kusaidia kujiajiri na kuajiriwa, tunawapa masomo tu ya nadharia ambayo hayawasaidii.

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu. Kwa nini Seriakli haifanyi utafiti ikabaini inahitaji watumishi wa idadi gani na ikawapa mafunzo wanafunzi ambao inaweza kuwaajili na

waliobaki ikawapeleka katika Vyuo vya *VETA* wakapatiwa mafunzo ya ufundi. Wengine tukawapeleka katika mafunzo ya utalii na ukarimu. Wengine tukawapeleka katika Vyuo vya Sanaa wakajifunza masuala ya utengenezaji filamu na muziki, mambo ambayo yanasaidia sana vijana wengi katika sehemu mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, wenzetu wa India, wenzetu wa Nigeria wenzetu wa Uingereza, wanatengeneza fedha nyingi sana kupitia vijana wao ambao wamepatiwa mafunzo ya kutosha katika sekta ya utengenezaji filamu na muziki. Kwa nini Watanzania hatufanyi jambo hilo?

Mheshimiwa Spika, nikimuangalia kijana wetu Diamond huwa ninasikitika sana, amefikia mahali amejifunza mwenyewe ujuzi wa kutengeneza muziki, sasa vijana kama Diamond hapa Tanzania wako wangapi? Diamond ana uwezo hata wa kumuajiri Daktari, ama kumuajiri Profesa! Kwa nini Serikali yetu haiviimarishi hivi vyuo ambavyo vinatengeneza filamu, vinatengeneza muziki ili tukapata Diamond kama 1,000 hivi na hao watakuwa na mchango mkubwa sana wa Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, tatu; hakuna jambo ambalo linanisikitisha sana kama kuona kwamba kazi ya kuwalea vijana wa Taifa letu siku hizi tumeikabidhi kwa dada wa kazi. Zamani tuliozaliwa zamani kidogo, tulilelewa na babu zetu, tulilelewa na bibi zetu na kwa maana hiyo tulifunzwa maadili, tulifunzwa tabia njema, tulifunzwa uzalendo, tulifunzwa heshima kwa watu. Leo tunalalamika kwamba vijana wetu wanakosa maadili lakini tunajiuliza wanalelewa na nani. Unakwenda kwenye kijiji unamchukua dada wa kazi, humjui ana maadili gani, unampa dhamana ya kukulelea watoto wako halafu tunalalamika vijana wetu hawana maadili, hawana uzalendo, hivyo Waheshimiwa Wabunge na Viongozi maadili hayo na uzalendo wao utatokea wapi?*(Makofi)*

Mehsimiwa Spika, maoni yangu nafikiri umefika wakati viongozi tujiulize, kwa nini wazazi wa zamani waliweza kuzalisha na kuwalea viongozi kama Marehemu Baba wa Taifa, Edward Moringe Sokoine, Mama Samia Suluhu Hassan na hata sisi! Lakini wengi wetu ambao tunasema tumesoma sana kinyume na wazee wetu ambao hawakusoma, hawajui hata kusoma na kuandika, lakini tunashindwa kutoa vijana ambao wana maadili mema, vijana ambao wana maandalizi ya kutosha, vijana ambao wana sifa za kuwa viongozi.

Mheshimiwa Spika, wala tusimtafute mchawi, tumelalamika hapa kuna mjadala tu toka juzi unaendelea hapa kwamba vijana maadili ya Kitanzania yanaharibika, lakini tumekaa chini tukajiuliza kwanini madili haya yanaharibika? Mimi nafikiri tusimtafute mchawi. Ni kosa letu wenyewe kama wazazi na walezi na kwa maana hiyo basi tubadilike, tubadilishe utaratibu wetu wa malezi, badala ya malezi kuwaachia Dada wa kazi imefika wakati sasa tusimamie malezi hayo sisi kama wazazi, walezi na viongozi. Tukifanya hivyo basi tutapata vijana, wenye maandalizi mema kwa ajili ya kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa niseme...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja, kengele ilishagonga Mheshimiwa.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti ya Bunge lako Tukufu, katika Kamati yetu tumebaini kwamba taasisi nyingi za Serikali zina mifumo ya kukusanya mapato iliyo dhaifu na ambayo haiwezi kuwasiliana, jambo hili limekuwa likichangia sana katika upotevu wa mapato ya Serikali. Kwa maana hiyo basi tunaishauri Serikali ifanye kila linalowezekana mifumo hii ya

kukusanya mapato iimarishwe, iunganishwe ili iweze kuwasiliana ili kudhibiti vitendo mbalimbali vya ubadhilifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nakushukuru kwa kunipa fursa hii.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nikawa najiuliza hapa Mheshimiwa Mkuchika sijui Wajukuu zake wako Dodoma humu, maana humu ndani wako vijana, wako wazee sasa sijajua itakuwaje, mambo haya ni magumu kidogo, ni magumu kidogo. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Abdulkarimu Halamga, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kipekee namshukuru Mungu kwa muda huu na afya ya kuniwezesha mimi nisimame hapa niweze kuchangia hii hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga hoja mkono na niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu wapitishe hii bajeti ya Waziri Mkuu ya shilingi 173,733,110,000 pamoja na ule Mfuko wa Bunge iliyoombwa shilingi 165,627,897,000.

Mheshimiwa Spika, nimeanzia hapo ka sababu ni dhahiri kabisa *charity starts from home,* sisi tuko hapa kwenye Fungu hili. Baada ya kuwaomba wenzangu na najua itapita bila pingamizi. Nianze sasa kuchangia hotuba ya kurasa 95 ambayo ilimsimamisha Waziri wetu Mkuu takribani masaa mawili akiisoma kwa umahiri mkubwa na baadae tukaenda Pasaka na kuweza kuizungumza huko na wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, wanawake wa Kilimanjaro wamenituma haya yafuatayo:-

Moja, kuhusu nishati safi na salama ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, wanawake wamekuwa wakipika wakilia, wakitoka machozi kwa ajili ya moshi, pamoja na hayo katika kukata miti ili ipatikane kuni au mkaa tumeendelea kuharibu mazingira, tabianchi nayo imekuwa ni tatizo. Namuomba Waziri Mkuu atueleze baada ya ule ufunguzi alioufanya Rais wetu Tarehe 01 mwezi Novemba pale katika ule Ukumbi wa Julius Nyerere ni takribani au ni *almost* miezi Sita, hatujaona jambo lolote.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kushukuru kampuni ya *Oryx* ambayo imeendelea kutoa mafunzo, tumeona wakigusa kaya mablimbali. Kilimanjaro waliweza kugusa kaya 700, huko Mwanza wakagusa kaya 700 labda na kwingineko kule ambako hatujapata taarifa. Sasa ni lini Serikali hii itatuambia hatua zinazoendelea ili sasa tuweze kuachana na shida hizi za nishati hiyo mbovu.

Mheshimiwa Spika, majirani zetu wameweza kupunguza kodi katika eneo hili ili nishati hii safi na salama iwe *affordable,* tumeona sasa hivi hakuna watu wanaokoka koka moto tena huko baadhi ya majirani zetu. Tunataka hii ifikiwe kwa sababu hata Ulaya walianza hivyo hivyo kupekicha moto wakawa wanapika kwa kuni. Sasa hivi ukienda unaoneshwa kama *museum.* Niliona kule Denmark. Sasa sisi tunataka kuachana na hiyo tunaomba sana Serikali itujibu kwa kina ni jinsi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo niende kwenye Wizara ya Mifugo, nimekuwepo hapa kwa kipindi sasa kama vipindi viwili na hiki cha tatu. Nikiomba Wizara ya Mifugo tusiende tu kuhesabu Mitamba iliyopo kwenye ranchi, sijui mbuzi waliopo kwenye ranchi na vingine, halafu iweje?

Mheshimiwa Spika, hivi ni sawa Serikali ikahesabu halafu huku kuna nguvu kazi, kuna akinamama wa Kilimanjaro ambao hawana hata ng'ombe wa kufuga, hawana kuku, hawana mbuzi, wanakaa tu, na wengine wanasubiri Serikali iwawezeshe, lakini wana migomba ya kulishia, wana majani ya kulisha na kila aina ya chakula cha mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali sasa itumie hatua ile ile aliyoitumia Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuleta mitamba bora, wakati huo nchi jirani zikiwa tatu zikiitwa *East Africa* walipokea. Kwetu baada ya zile mbegu za awali au ile mitamba ya awali kumalizika kutoka *Denmark,* maziwa yakapungua, lakini tunanunua maziwa kutoka Kenya, tunanunua maziwa kutoka Uganda, tunanunua kutoka *South Africa.* Sasa tunakwenda wapi? Iliisha ile awamu moja, hizi awamu nyingine zinaonaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona hilo niliseme. Nachukua nafasi hii kupongeza sana wale wanawake wa Uswaa, wale wanawake wa Lawati ambao ni wazalishaji maziwa. Naomba mwendelee kununua maziwa kutoka Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maziwa haya au tungepata vifaranga, ndiyo lishe bora. Juzi juzi tulikuwa na sensa ya watu na makazi, lakini taarifa zinasema kwamba bado sisi tuna udumavu, bado maeneo fulani yana viribatumbo, hiyo yote ni lishe mbovu. Endapo watu wetu wangeweza wakazalisha chakula kizuri, wakazalisha mayai, kila mtoto akala yai moja asubuhi kabla hajaenda shule, hivi vitu vinavyozungumzwa visingekuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanawake wa Kilimanjaro wamefaidika kwa ile asilimia 10 (4:4:2) na wanaomba sasa kilichowafanya wakakimbilia sana ni ile kutokuwa na asilimia ya riba. Waliokuwa wamejikusanya kwenye vikoba vyao ikiwa kama njia moja ya kujikomboa walienda wakaweza

kukopeshwa kidogo kidogo. Ni kweli kuna changamoto, lakini hapo tunapoenda kurekebisha bado wanaomba ile riba isiwepo, hilo ni ombi lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafuta ya kula yamekuwa ni tatizo katika nchi hii. Kamati ya Bajeti tuliwahi kutembelea bandarini tukaona ma-*container* kwa ma-*container* ya mafuta ya kula yakitoka nje. Siku za nyuma Manyara walikuwa wanalima alizeti, Arusha walikuwa wanalima alizeti, Kilimanjaro walikuwa wanalima alizeti, mpaka lilipotokea tatizo la ile kutu kwenye majani. Sasa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, katika mikoa ambayo itapendelewa kupelekewa kulima alizeti, hii mikoa mitatu niliyoitaja haikutajwa tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa, walioko hapa kwa ajili ya Waziri Mkuu, akiwemo huyo Katibu Mkuu na timu yake, waone kama lilitokea tatizo mahali, kule lilikotokea lirekebishwe na huko kupya pia kuendelezwe. Mafuta ya alizeti ni mafuta safi na salama na ni rahisi kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo hapo kwenye Wizara ya Kilimo wamenituma nihoji, hivi hao waliopatiwa *block farms* wamechaguliwa vipi? Mbona hawawaoni wana-Kilimanjaro waliopatiwa hizo *block farms?* Labda na mikoa mingine pia inajiuliza, watu wetu mbona hawakupatiwa? Kwa hiyo, naomba itolewe elimu ili watu wajue, hawa wanaopelekwa kwenye *block farms* wamepatikana vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale wanaokwenda jeshini tunajua, wakimaliza *form six* kuna wanaokwenda, lakini wale wengine wa darasa la saba wanapitishwa kwa Mkuu wa Mkoa, wanakwenda, Kamati zinakaa wanapatikana. Sasa swali linakuja, hawa wa *block farms* wamepatikana vipi? Tunaomba sana tujue ni jinsi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mazao yenye thamani kubwa ikiwepo kahawa. Hapa tunaambiwa *TaKRI* inatoa mbegu

kirahisi, bure *actually,* lakini mbegu hizo hatuzioni sasa zikileta *impact* kwenye kukuza mapato ya zao la kahawa. Tumeona, ukisema zao la kahawa limeongezeka Kilimanjaro ni zile *estates,* yaani yale mashamba makubwa ya wageni ambayo wamekodishiwa, lakini ukienda kwenye shamba moja moja la mkulima wa Kilimanjaro ni hoi bin taabani, hakuna kahawa. Nami hapa naomba sana Wizara ya Kilimo, pamoja na kugawa pikipiki kwa wagani na kadhalika, wapite sasa kwenye yale mashamba moja moja, sisi tunaita vihamba; waanzie huko Moshi, waende Same, waende Mwanga, waende Rombo, waende kote Kilimanjaro tuone wamesaidikaje katika kutumia vitu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawaomba hawa wa kilimo waweze kutoa elimu kwa *drip irrigation,* yaani ile ya matone, ndiyo rahisi na pia inatumia maji kidogo. Tuking'ang'ania tu *furrow irrigation,* ile ya mifereji, hatuna tena mifereji inayotiririsha maji kwa wingi. Kamati Wizara ya Kilimo itatusaidia tukawa na mahali pamoja pa chanzo cha maji, tukaweza kupata hiyo *drip irrigation* itasaidia mashamba yote.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa pia nataka kuwaomba ili waweze kutenga eneo kama pale *KIA* kwa ajili ya kongani za biashara. Watu ni wengi Kilimanjaro kutokana na sensa, lakini lile eneo pale *KIA* likitumika kwa Arusha, kwa Kilimanjaro yenyewe, wakawa na vile viwanda vidogo, vinaweza kutoa ajira kwa wengi kwa sababu wameweza sana kuwaelimisha watu. Kwa hapa naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu alivyoona *VETA* hizi zijengwe kila Wilaya na sasa zinajengwa, nami nashukuru kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme wazi, katika jambo ambalo linawafanya mabinti wapende kwenda shule, wanajua watakwenda sasa kutoka *Standard One* mpaka *Form Six.* Hili ni jambo la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wasome bure; na binti ambaye anadanganywa akaolewe kabla ya

umri asikubali. Hizo ndoa za utotoni wewe binti unaweza kusema hapana, kimbilia kwenye maeneo ambayo yanataka vijana wasome, wakomae. Usiende ukabeba ujauzito wakati ambapo viungo vyako havijawa tayari.

Mheshimiwa Spika, wamesema waliotangulia kwamba kwa sasa hivi wanapata ile hali ya kukua *(maturity)* kwenye miaka tisa. Sasa fikiria mtoto wa miaka tisa anakwenda kulea nyumba, haiwezekani. Nawaomba sana vijana mwende shule, mtulie darasani, msome kwa makini mpaka mfikie hiyo *level* ambayo Serikali yenu imejitolea na imewapa baraka mpaka *Form Six*. Ajali inaweza ikatokea njiani, lakini ajali ikitokea njiani pia wasichana wamepata tena *chance* nyingine ya kwenda kuingia shuleni kwa kufikiriwa hii ajali ilitokeaje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe sana mabinti wetu na niwaase, hakuna jambo zuri kama shule na elimu haina mwisho. Hata mkiona hapa, kama mimi mama yenu nimesimama hapa na mpaka sasa niko darasani, ukiniuliza nasoma nini? Napenda nifahamu zaidi, hakuna mwisho wa shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema hivyo na nikakumbuka, ninatumwa kila wakati salamu zako na hata leo asubuhi. Nadhani wanaonituma wamefurahi sana kwamba, umetuliza hali ya hewa. Wanasema kiambie kile kichwa kinachokalia kiti pale Bungeni, sisi tunamwelewa sana. Kijana wa boda aliyenipa usafiri leo ameniambia, amesikia kuna watu wanakuchokoza huko Mbeya, wako tayari kutoka Dodoma kwenda kunyamazisha hiyo hali ya hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingesema hili kesho akinichukua angeniambia. Mama una uhuru wa kusema, kwa nini hukututolea salamu?

Mheshimiwa Spika, pokea salamu zako, Watanzania wanakuelewa, ukizungumza wanakusikiliza. Naomba tu kwa wale wote waliopata nafasi, ambao ni jenda ya Ke, mwendelee kama hivyo. Tunawaelewa wote; Mawaziri wetu tunawaelewa, viongozi wetu ma-*RAS,* Wakurugenzi, Wakuu wa Wilaya, tunaomba sana tuendelee na mwendelee kumsaidia Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kuona kwamba, jambo hili jema linakwenda na kila kitu kinaenda kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nilikuwa naomba tu, leo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele imegonga Mheshimiwa. Sekunde 30.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nimeona ajira zilizotoka, elimu itolewe kwamba Mbunge hawezi kwenda kuomba ajira kwa maandishi. Naomba mwaelezee, ahsante.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kukumbushana. Unaponyanyuka kwenye kiti chako ukitaka kwenda kiti kingine, tazama mchangiaji yuko wapi, ili usipite katikati yake na Spika. Ni muhimu kwa sababu mchangiaji anakuwa anamtazama Spika, sasa wewe ukipita mbele yake, unapoteza hoja yake. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuzingatia hilo.

Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga, atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah ajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami kuweza kuchangia bajeti ya mwaka 2023/2024.

Kwanza nianze kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambazo anazifanya za kimaendeleo katika nchi yetu, lakini katika kuhakiisha kwamba anaendelea kupambana bila kulala, bila kuchoka, kuhakikisha anaendelea kutatua changamoto kubwa ya ajira tuliyokuwanayo vijana wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa zaidi ya Shilingi bilioni 39.8 kwenye Kiwanda cha Mkulazi, Kiwanda cha Sukari Morogoro ambacho mpaka sasa hivi kimeshaajiri takribani zaidi ya vijana 154 wa Kitanzania wako kazini. Mpaka sasa hivi zaidi ya hekta 2,900 zimeshaweza kufanyiwa kazi. Tunatarajia ndani ya mwaka mmoja zaidi ya tani 50,000 zitaweza kuzalishwa na hivyo itakuza mnyororo wa thamani ya uchumi kwa maana ya kuanzia ndani ya nchi yetu kuondoa tatizo la sukari, lakini pia baada ya kukidhi soko la ndani tunaweza kupeleka na soko la nje na hivyo kuliongezea Taifa letu mapato.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara ya Kilimo kwa ubunifu wa skimu za umwagiliaji ambao tunaamini utaenda kutatua tatizo kubwa sana; kwanza la ajira; na pili, utaenda kukuza uchumi wa nchi yetu kwa sababu ni kilimo ambacho kitakuwa ni cha muda wote na kitaendeleza mnyororo wa thamani. Naishukuru sana Wizara ya Kilimo, lakini niiombe sasa, kwa jitihada hizo ambazo imeanza kuzifanya, basi ni vyema wakashirikiana na watu wa JKT kwa maana ya kuwatumia vijana walioko makambini kwa mfano, kambi yetu ya Makutupora, kwenye kilimo cha alizeti; Kambi

ya Chita kwa maana ya kilimo cha mpunga na maeneo mengine kadha wa kadha. Kwa sababu tayari tuna nguvukazi ya Taifa hili ambayo ipo na yenye maadili makubwa na inaendelea kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaweza tukawasaidia vijana hawa kupitia JKT ili kuendelea kuhakikisha nchi yetu ya Tanzania kupitia kilimo kama ambavyo Waziri ameweza kuweka mipango thabiti ya kilimo cha umwagiliaji, basi tunaunganisha nguvu ili kuweza kukidhi soko la ndani, lakini kuendelea kufanya mazingira rafiki kwa vijana wa Kitanzania kuona tija ya kilimo na baadaye kuweza kukopesheka ili wao wenyewe wawe ni sehemu ya mitaji na sehemu ya uzalishaji kwa maana ya wao binafsi, kwa kuwa tayari Wizara imeshaonesha wapi tunaelekea? Wapi tunakwenda? Kilimo Tanzania chenye tija kinawezekana. Hongera sana Mheshimiwa Rais, hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuendelea kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha anaendelea kuwakwamua wananchi wake na hasa kupitia kilimo, na viwanda. Mheshimiwa Rais kupitia watu wa Poland waliweza kuingia makubaliano na Serikali ya Tanzania kupitia Shirika la Maendeleo la *NDC* na kuleta matrekta ndani ya nchi yetu ya Tanzania, matrekta yaliyoletwa na Kampuni ya Ursus ambayo yaliweza kukopeshwa kwa wakulima wetu hapa nchini kwa maeneo tofauti tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe masikitoko yangu kwa niaba ya wananchi, wakulima ambao waliweza kupokea matrekta hayo. Matrekta hayo yalivyoingia ndani ya nchi yetu, kwanza wakulima ambao walikuwa na sifa hizo za kupokea walitakiwa waende kuchukua matrekta hayo kwa usafiri. Maana yake wasiyatembeze mpaka maeneo wanapofika, bali watafute fedha waende wakachukue matrekta hayo.

Mheshimiwa Spika, wananchi walikopa, waliuza vitu vyao, wakasafiri wakaenda kubeba matrekta hayo na kuyapeleka *site*. Wananchi wamefika na matrekta hayo, na kwenye mkataba walikubaliana miaka miwili wataendelea kupewa huduma ya vipuri, lakini matrekta hayo yamefika kwa wakulima, na ndani ya nchi hakuna vipuri. Mkataba umekiukwa kwa sababu hawakuletewa vipuri hivyo ndani ya nchi yetu. Nini ambacho kimetokea?

Mheshimiwa Spika, kilichotokea ni umasikini mkubwa kwa wakulima wetu ambao walikopa fedha zao, badala ya kuwekeza kwenye msimu ambao siku zote wamezoea kulima kwa kawaida, walijiwekeza wakaenda kuchukua matrekta hayo. Matrekta yamefika shambani, hayana vifaa, yameharibika. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, kuna Taarifa ya kutoka kwa Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao.

**T A A R I F A**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** *Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa msemaji wa taarifa hii ya haya matrekta ya Ursus. Matrekta haya yakiingia shambani linakatika vipande viwili. Hatujui aliyekwenda kuyanunua haya matrekta. Kwa hiyo, tunaomba iundwe Tume ya Bunge kwenda kuchunguza mradi huu wa haya matrekta kutia watu umasikini. Watanzania wakulima masikini wamekwenda kufilisika. Ahsante sana. (Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**SPIKA:** Nachelea kumuuliza mchangiaji kwa sababu imetajwa hapo kampuni mahususi na tusije tukaingia kwenye mgogoro wa kibiashara hapo. Hoja ya Mheshimiwa Asia Halamga sikuiingilia kwa sababu inahusu vipuri vya hayo

matrekta ambayo yametajwa jina, lakini sasa ule udhaifu wa hayo matrekta anaouonesha Mheshimiwa Tabasam, nisingependa Bunge lijielekeze huko kwa sababu, sina taarifa. Tusije tukaingia kwenye mgogoro wa kibiashara kwamba, mtu anaharibiwa biashara yake.

Kwa muktadha huo, Mheshimiwa Tabasam, hilo eneo la kuonesha udhaifu wa hayo matrekta kwa sababu ya hoja hiyo ya kibiashara isije ikatuletea changamoto hapa, maana mimi sina hiyo taarifa, inaondolewa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Asia Halamga, malizia mchango wako.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba tu sasa kwa sababu watu hawana ufafanuzi mzuri juu ya matrekta haya, niendelee tu kuchangia kwa kusema kwamba matrekta haya wakulima wetu, kwanza wakati wanakwenda kuyachukua walitakiwa waingize fedha kwenye akaunti ya mtu binafsi ambaye alikuwa anasimamia. Wananchi wakaingiza fedha kwenye akaunti hiyo ya mtu binafsi, lakini matrekta nje ya mkataba ule ambao wamekubaliana kwamba walete vipuri na vipuri havikuja, wananchi sasa hivi wameanza kukamatwa.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi, wananchi walianza kuitwa na watu wa TAKUKURU na walikuwa wanafanya *bargaining*. Baada ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu kupitia Ripoti ya *CAG* ambapo alipoongelea masuala ya TAKUKURU kutokuingilia masuala haya ya *fine* na kadhalika, wakaweza kusimama, lakini watu hawa *NDC* wakaamua kutumia watu wa *Majembe Auction*. Watu wa *Majembe Auction* wanakwenda kuwakamata wakulima na bahati mbaya sana wakiwapigia simu wanaanza ku-*bargain* nao kwamba umelipa lini?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wakulima wamepewa akaunti nyingine ambayo wanatakiwa walipie sasa rasmi hiyo fedha, lakini fedha ya mwanzo ambayo wameitoa na kuweza kupata matrekta kipindi cha mwanzo, fedha ile haitambuliki.

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, wananchi hawa wamekosa jukwaa, kwanza la shirika lenyewe kwa sababu wametafuta nafasi mra kwa mara waweze kuongea nao kwa sababu tayari wako nje na mkataba, hawajapata nafasi ya kukaa nao. Haitoshi, wananchi hawa ambao ni wakulima wameshakuja mara kadhaa Dodoma bila mafanikio ya kukutana na viongozi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa wameandika barua hii hapa na ilikwenda kwa Wizara ya Viwanda na Biashara, wananchi hawa hawajaweza kupata majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi natokea Wilaya ya Hanang. Ukifika Wilaya ya Hanang unakutana na wamama ambao wamekimbiwa na waume zao kwa sababu wanaenda kukamatwa na *Majembe Auction* kule chini. Wamama hawa wameshindwa kuwapeleka watoto shule…

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Nani amesimama kuhusu taarifa?

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, niko huku.

**SPIKA:** Aah, Mheshimiwa Flatei.

**T A A R I F A**

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe Taarifa mzungumzaji. Pamoja na kutokuwa na vipuri

ndani ya nchi, wanaenda kuchukua vipuri hivyo nje ya nchi. Pia Jimbo la Mbulu Vijijini kuna tatizo kama hilo hilo na taarifa hii ni ya kweli.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Huyo alikuwa anachangia, lakini muda wako umekwisha Mheshimiwa Asia Halamga; nakupa dakika moja umalizie hoja yako.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, nakuomba dada yangu uniongezee muda hata wa dakika mbili niweze kumalizia.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya kumalizia na kwa sababu ya tija katika Taifa letu dhidi ya makampuni ambayo yanaweza kuleta vifaa ndani ya nchi yetu na kwenda kuwatia watu wetu umaskini na ambaye anapata doa siyo mtu wa nje, anayepata doa ni Serikali ya Tanzania wakati Mheshimiwa Rais ameamua kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu la kwanza ninaiomba Serikali kwanza ikubali kukaa na hawa wakulima ili iweze kujua changamoto zao ni zipi ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili; ninaiomba Serikali iweze kuangalia kampuni hii kama ina tija au kama haina tija kwa sababu zoezi lenyewe lina tija kwa wakulima, ninaomba iwezekane kampuni ibadiliswe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia; suala la ushoga. Niombe, wasanii wetu ndani ya Nchi yetu ya Tanzania na kupitia BASATA. BASATA wimbo ukiingia doa kidogo la kama

tusi au maadili hapohapo wanafungia wimbo, watoto wa kike wakivaa vimina hapohapo wanafungiwa wimbo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna tija gani ya watoto wetu wa kiume kuvaa mawigi, maziwa au makalio ili kuonesha sanaa? Kwani hakuna njia nyingine ya wasanii wa kiume wa Tanzania kuweza kupeleka ujumbe bila kuvaa mavazi ya kike? Wanavaa mawigi, wanapaka poda, wanapaka wanja; wanafundisha nini wakati wao ni kioo cha jamii kwa watoto ambao wanachipukia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani hilo suala nimeshalitolea maelezo kwa kirefu. Naona hapa mnapiga makofi lakini nafikiri tukiingia tu kwenye huo mjadala tutachanganyana bila kuwa na taarifa za msingi. Sanaa imekuwepo miaka yote, kama Serikali itakapoleta hiyo taarifa tutaona namna inavyofanywa sanaa inaleta changamoto, maana sasa hivi umezungumziwa upande wa watoto wa kiume, je watoto wa kike wanaovaa suruali?

Kwa hiyo, naona watu wanapiga makofi kwa bidii sana lakini mambo haya ni mambo mapana mno. Kwa hiyo, lazima tuyatazame kwa sura zote. Na ili tupate hiyo nafasi lazima hapa Bungeni wakati huo kama wenzetu watakuwa wameshamaliza utafiti tukiwa na hiyo hoja hapa ndiyo tutaweza kuijadili kwa mapana. Lakini hii ya kudokoadokoa tunaweza kutuma ujumbe ambao hauna uhalisia huko nje. *(Makofi)*

Nilitaka nikuulize swali Mheshimiwa Asia Halamga; ulikuwa unaeleza kuhusu mkataba, kwamba mkataba ulisema na vipuri viwepo, ni mkataba kati ya nani na nani? Umetumia sana neno mkataba; ni mkataba kati ya nani na nani ambao ulikuwa unataka vipuri viwepo?

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ni Serikali iliingia na hiyo kampuni, na makubaliano yalikuwa ni kuleta vipuri na kuwahudumia wakulima ndani ya miaka miwili. Na kwa sababu jambo hili lipo kiuhalisia, ukiniruhusu ninaomba nikupe taarifa mkataba huu hapa ninao, lakini pia nakala za barua ambazo wameandika wakulima kuweza kukutana na viongozi wa Serikali na *NDC*.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Halamga, nimeuliza swali dogo tu; hebu nipatie hiyo nakala hapo ya mkataba kwa sababu nataka kujua mkataba ulikuwa kati ya nani na nani, maana hili jambo leo siyo mara ya kwanza kujitokeza hapa Bungeni.

Mhudumu, vipi jamani, mbona… au umeamua kuusoma njiani huo mkataba? Ahsante sana. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nataka nielewe ili jambo hili lifike mahali ambapo hao wananchi wanaokamatwa huko, lifike sehemu nzuri. *(Makofi)*

Sawa! Sasa wakati natazama hapa naona mambo yako mengi. Wakati nikitazama nitajiridhisha kwamba mkataba uko kati ya nani na nani halafu Serikali itaambiwa nini cha kufanya.

Hapa mkataba huu Mheshimiwa, mkataba unasema umeandaliwa na *NDC* lakini ni mkataba kati ya Shirika la Taifa la Maendeleo na bwana huyu ambaye ametajwa hapa jina. Mkataba wa kukopeshwa trekta kati ya huyo mkopaji na *NDC*. Hapa ile kampuni iliyokuwa inatajwa inaingia wapi; wapi iliingia na Serikali?

Kwa hiyo kwa hoja yako ni kwamba *NDC* iliingia mkataba na ile kampuni ambayo wewe huna huo mkataba; umejuaje kwamba huo mkataba upo Mheshimiwa Halamga?

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ukinipa nafasi ninaweza kukuletea kwa sababu hata risiti za benki ambazo wananchi wameweza kulipia ninaweza kukuletea pia. Na ndiyo maana nikaiomba Serikali iweze kukutana na wakulima na iweze kupata ufafanuzi na kujua zaidi nini kilichopo ndani ya suala hili.

**SPIKA:** Sawa. Nafikiri hoja yangu hujaielewa; ili tusifike kwenye mgogoro, maana kampuni hapa imetajwa kwa jina lakini mkataba ninaouona hapa ni kati ya *NDC* na yule anayekopa. Sasa ili nisikuweke hayo mazingira ya kuniletea mkataba huo ambao upo Serikalini maana hapa ninaouona ni tofauti, na mimi nijielekeze kwenye huu ninaouona.

Haya, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naona una ufafanuzi; karibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunupa nafasi. Kampuni ya *Ursus* ni kampuni kutoka Poland, na Serikali ya Poland iliingia mkataba na Serikali ya Tanzania na *NDC* ikawa ni *implementing agency* kwenye hayo matrekta.

Mheshimiwa Spika, na nikiwa Waziri wa Viwanda na Biashara tulichambua na kuona dosari ambazo ziko katika huu mkataba. Serikali kipindi kile tukapendekeza, tu-*renegotiate* na Serikali ya Poland. Lakini moja ya changamoto ambazo tulikutana nayo ni kwamba Kampuni ya *Ursus* ni mufilisi kule Poland. Kwa hiyo, Serikali ilikuwa inaendelea na utaratibu wa kuangalia namna ya kufanya hiyo *renegotiation. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, changamoto ambayo Mheshimiwa Mbunge ameisema ninaamini Wizara ya Viwanda na Biashara wataichukua ili Serikali iendelee kulifanyia kazi. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa. Sasa naona changamoto hapo, maana yake wewe ulikuwa Waziri wa Viwanda na Biashara ukatoka, ameingia mwingine, changamoto imeendelea kuwepo. Na nafikiri labda hatujafanya kazi kwa namna inavyotakiwa kwa sababu wananchi wanaendelea kunyanyasika wakati hawana vipuri. *(Makofi)*

Sasa kama hiyo kampuni iko mufilisi kwa nini hawa wananchi wanaendelea kudaiwa, halafu vipuri watavipata wapi sasa. Na matrekta watakuwa wamepata hasara. *(Makofi)*

Maana yake kwa ununuzi wa lile trekta yeye kapata hasara, sasa kama yeye amepata hasara na sisi tunajua kwamba kapata hasara halafu tunaendelea kumdai, tunamtumia na watu wa kumkamata. *(Makofi)*

*Anyway,* sawa. Sasa kwa ufafanuzi huu uliotolewa hapa na mchango wa Mheshimiwa Asia Halamga, kwa sababu Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara haijapita bado hapa Bungeni. Kwa hiyo, nimuombe Mwenyeiti wetu wa Kamati nadhani ni Mheshimiwa Kihenzile, siyo? – Mheshimiwa Halamga, taarifa ulizonazo kuhusu jambo hili na Wabunge wa Manyara, nadhani Manyara wote mlikuwa mnasema kesi ni moja, muonane na Mwenyekiti mumueleze hoja hii, yeye ataileta kwangu nitatoa maelekezo kwa Serikali. *(Makofi)*

Kwa sababu kwa sasa hivi nashindwa kidogo nitoe maelekezo ya namna gani, lakini nikishapata hizo taarifa mahususi nitatoa maelekezo kwa Serikali ili jambo hili lifike mahali ambapo wale wananchi watakuwa hawanyanyasiki kwa kukopa matrekta ambayo wamepelekewa na Serikali. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa yangu iliyofutwa naomba iingie kwenye *Hansard* kwa kuwa tayari na wewe umeikubali taarifa hii, ahsante. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam, Waheshimiwa Wabunge, huwa napenda tuwe tunasikilizana na huwa najitahidi kweli kuzungumza taratibu ili tuwe tunaelewana.

Mheshimiwa Tabasam, hoja yako ni tofauti na ya Mheshimiwa Halamga. Mheshimiwa Halamga hajaeleza udhaifu wa matrekta, ameeleza hoja kwamba yale matrekta hayana vipuri kwa hiyo wakulima wanateseka. Wewe umeleta hoja kwamba matrekta yanakatika. Ukisema nimeikubali hoja yako ni maelezo yangu yapi yaliyokubali kwamba trekta la *Ursus* linakatika likiingia shambani.

Kwa hiyo, ndiyo maana huwa naongea taratibu na huwa inabidi ukijitahidi tu kunisikiliza lazima utanielewa. Na ninafikiri na wewe umeelewa. Kwa hiyo, maelezo yako bado yanaondoka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Kwanza siyo yanaondoka, yalishaondoka, kwa hiyo na haya uliyoyasema sasa hivi na yenyewe yanaondoka ili yaondoke yote pamoja.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo iko Mezani kwa ajili ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa taarifa aliyotusomea hapa Bungeni, taarifa ambayo imesheheni mipango mizuri ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaokuja. Ninaamini kabisa mipango hii ambayo imeelezwa hapa ikitekelezwa vizuri tutakwenda kubadilisha kabisa maisha ya Watanzania na kuweza kusogeza mbele gurudumu la maendeleo, ikiwemo utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo tuliahidi tutakwenda kuleta maendeleo kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijakwenda kuchangia hoja ambayo iko Mezani, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya kwa ajili ya Watanzania. Kazi kubwa anayoifanya katika muda wa mwaka wa fedha huu tunaomaliza sisi watu wa Singida Mashariki kwa maana ya Wilaya ya Ikungi, tumeona fedha nyingi zimeshuka katika halmashauri yetu. Na hii haijawaki kutokea, tumeweza kupata fedha nje ya bajeti iliyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tulipokea zaidi ya bilioni 12 katika muda wa mwaka huu wa fedha. Imetekeleza miradi mingi sana. Miradi ambayo hatutaisahau ni miradi ya barabara. Barabara zetu ndiyo uhai wa wananchi wetu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, barabara zaidi ya kilometa 157 ambazo zilikuwa hazipitiki kabisa zimetengenezwa na kuimarishwa ikiwemo kuwekwa madaraja. Kwetu sisi tuliona tusiposema haya tutakuwa hatumtendei haki na tutakuwa hatuitendei haki Serikali yetu. Tunashukuru sana kwa namna ambavyo Rais ametuletea fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la barabara kwa mara ya kwanza tunakwenda kupata barabara za lami katika Mji wetu wa Ikungi. Tumepata kilometa mbili ambazo

zinaendelea kujengwa na wakandarasi na kuna mpango wa kuweka taa za barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini kabisa Mji wa Ikungi sasa utakwenda kuwa na mwanga katika saa za usiku na itasaidia hata wafanyabiashara wadogowadogo kufanya shughuli zao hata kipindi cha usiku kuweza kuhudumia watu wanaopita katika eneo hili. Kwenye hili tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na tunaendelea kumuombea kila la heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kama haitoshi, kwenye eneo la elimu tumeeleza sana, lakini tumepata zaidi ya madarasa 109 ambayo yameweza kutumika, na ni zaidi ya bilioni nne na milioni 900 imetumika. Kwetu sisi ni mabadiliko makubwa sana ya kimaendeleo na tunaamini kwamba tutakwenda kuboresha elimu ya watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaeleza mengi, lakini tutaeleza upande wa *REA; REA* imeendelea kusambaza umeme katika maeneo yetu. Tarafa ya Mungaa ambayo nilikuwa nailalamikia leo kila kijiji kimepelekewa nguzo. Tunategemea ndani ya muda mfupi vijiji vyote vitakuwa vimepata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hili niendelee kuomba, kama ambavyo tumeambiwa *REA* hii Awamu ya Tatu itakwenda kupeleka kwenye vitongoji, basi kuna vitongoji ambavyo havijapata umeme. Tuweze kuangalia katika bajeti hii inayokuja. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa maeneo yote hayo, sina haja ya kurudia yote, lakini tunasema tunashukuru, na waungwana wanasema kushukuru ni kuomba tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo nianze sasa kuchangia bajeti ambayo iko mbele yetu ya Ofisi ya

Mheshimiwa Waziri Mkuu, na ameeleza zaidi katika eneo la barabara kuu ambazo zinaunganisha mikoa yetu.

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Singida bado tuna changamoto ya kuunganisha barabara katika mkoa. Tunayo changamoto ya kutoka Tanga kuja Singida, lakini bado tuna changamoto ya kutoka pale Mkiwa (Itigi) mpaka kwenda kule Mbeya. Tunayo maeneo hayo mawili bado hatujaunganishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tunayo furaha kwamba tuliwekwa kwenye bajeti inayoisha mwaka huu tuliambiwa tutajengewa kilometa 2,100. Barabara zilizotajwa ni pamoja na Mkiwa – Itigi – Makongorosi – Mbeya. Barabara hii bado hatujapata mkandarasi. Lakini bado kuna barabara ya Singida – Kwamtoro kwenda mpaka kule Kibrashi, Tanga, bado hatujaanza ujenzi wa barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara hizi zitakapokamilika zitakwenda kuongeza uchumi wa wananchi wetu, zitakwenda kuongeza thamani ya miradi ambayo tunaitengeneza. Mfano barabara hii ya Tanga kutoka Handeni kuja mpaka Singida itakwenda kuihuisha Bandari ya Tanga ambayo tumewekeza fedha nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba sana tuhakikishe kwamba barabara hii mkandarasi anaingia. Tuliambiwa tutatumia mfumo wa *EPC+F,* mpaka leo tunavyoongea wako kwenye *negotiation,* hawajamaliza hatua za manunuzi. Wamalize mchakato wananchi wanasubiri barabara hizi kwa hamu kwa sababu Serikali ilishawaahidi katika mwaka wa fedha tunaokwenda kuumaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye eneo hili la watumishi, na nieleze la watumishi kwa maana nilikuwa nalenga kwenye fedha zinazoletwa. Tunaomba sana

wananchi kwa maana ya wale waliopata nafasi ya kuwa watumishi wa Umma waitendee haki nchi. Fedha zinaletwa nyingi katika maeneo yetu; wawe wazalendo ili fedha hizi ziwe na thamani. Kwa sababu kabla hujaamua kufanya ufisadi kwenye miradi hakikisha wewe kijiji unachotoka kimemaliza matatizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tungekuwa tunaangalia umaskini uliopo kwenye vijiji vyetu tunapotoka ninaamini hakuna mtumishi wa Umma ambaye angefuja fedha za Serikali. Niwaombe sana tuwe wazalendo, tuitendee haki nchi yetu kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri katika kujenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la ajira pamoja na wastaafu; naishukuru sana Serikali, tumefanya kazi nzuri ya kuendelea kuajiri, na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Na juzi hapa tumetangaziwa tena ajira nyingine 21,000. Ni jambo zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo hili ninataka niombe; tumekuwa na wahitimu wa mwaka 2015, 2016 mpaka 2020, tumekuwa tukitangaza nafasi hawapati. Watu hawa wameshakaa mtaani vya kutosha. Zimetangazwa hizi ajira za sasa hivi, tunaomba sana wapewe kipaumbele, waweze kuajiriwa ili wasiondoke kwenye muda ule wa utumishi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wakicheleweshwa leo katika miaka mitano ijayo watakuwa hawaajiriki na itakuwa haina sababu ya kuwasomesha kwa fedha nyingi. Na wengine wamekopa kwenye mfuko wa elimu ya juu, maana yake watashindwa kulipa fedha hizi. Eneo hili tukifanya vizuri tutakuwa tumewatendea haki vijana wetu ambao wanatafuta ajira.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili la wastaafu ninataka niunganishe; tumekuwa na malalamiko ya baadhi

ya wastaafu. Wanalalamika wanapomaliza utumishi wao wamefanya kazi nzuri lakini wengine wamekuwa wakilalamika hawalipwi fedha zao kwa wakati. Hili eneo limekuwa likilalamikiwa na sisi Wabunge tumekuwa tukipata malalamiko hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mzee wangu mmoja ambaye barua yake ninayo hapa, ameniletea kama Mbunge wake. Anaitwa Simon Alberto Makia, ni mzee wangu kutoka pale Siuyu, Singida. Niombe sana nitaikabidhi hii barua yake, amekuwa akilalamika anasubiri kupewa fedha zake ambazo amestaafu.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunavyoongea amekuwa akija mpaka Bungeni hapa nje akifanya juhudi za kumuona Mheshimiwa Waziri aweze kumwambia kilio chake. Nitaomba sana kama Mbunge wake nikabidhi na ninaomba sana wa aina hii waweze kutendewa haki kwani wamefanya kazi nzuri katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimalizie kwenye eneo la utawala, lakini kabla ya eneo hilo, niishukuru sana Serikali kwa kutupatia chakula cha kupunguza makali cha bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chakula mwaka huu kimetusaidia sana watu wa Ikungi, tumeweza kupunguziwa makali ya njaa ambayo ilikuwepo. Hatukuvuna vizuri msimu uliopita lakini toka mwezi Novemba tumekuwa tukiletewa chakula cha bei nafuu. Wananchi wetu wamefarijika, wanaishukuru Serikali na wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa upendo wake na huruma yake. Ninaamini kabisa mwaka huu hali ni nzuri, tumeona mazao na huenda Mungu akajalia tukavuna vizuri. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimalizie eneo la utawala; sisi Wilaya ya Ikungi tunayo majimbo mawili ya kiutawala lakini majimbo

haya yamepewa majina ambayo ukiangalia haraka haraka ukimtajia mtu hajui kwanza jimbo liko wapi. Ninaamini kabisa sisi hatuombi eneo jipya tunachoomba ni jina tu libadilike. Tunayo Singida Mashariki na Singida Magharibi; ombi letu, na kwenye *RCC* tulishaleta, tunaomba tupate majina halisi ya maeneo husika. Kwa mfano tukipewa jina laJimbo la Ikungi angalau linaweza kuleta maana nzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiletewa Jimbo la Puma au Jimbo la Sepuka maana yake unakuwa umeshaweka *identity* ya eneo husika. Ninaamini kabisa hili jambo si kubwa, na pacha wangu ananipigia makofi maana yake anakubaliana, ili tuhakikishe kwamba tunapata *identity* halisi ya majimbo haya na wananchi wajue Wabunge wao tunapotaja Jimbo la Ikungi, Jimbo la Sepuka maana yake ni Wabunge wanaotokana na Wilaya ya Ikungi.

Mheshimiwa Spika,baada ya maneno hayo kwa heshima kabisa ninaomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini naomba tupitishe bajeti hii ili Waziri Mkuu afanye kazi nzuri anayoendelea nayo. Naunga mkono hoja, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana; Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya, Mheshimiwa Godwin Kunambi ajiandae.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote nianze kukupongeza wewe binafsi kwa busara na hekima kubwa uliyojaliwa na Mwenyezi Mungu. Nimefurahishwa sana na taarifa uliyoisoma hapa leo Bungeni asubuhi ya kutufafanulia kuhusu taarifa ya *CAG*. Naamini kabisa ni busara imekuongoza ukaona ni bora niende nikafafanue ili watu wanielewe. Tumekuelewa vizuri sana na tuko tayari kusubiri kujadili mwezi Novemba kama taratibu zetu zinavyosema.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya nchi yetu. Hakuna mtu ambaye hajui kuwa Mheshimwa Rais anafanya kazi kubwa. Mheshimiwa Rais anapambana ili kuhakikisha Watanzania wanapata maendeleo. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais na tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee na kazi ya kutupambania sisi Watanzania. Mheshimiwa Rais amefanya mambo makubwa, amefanya mambo mengi ambayo mimi binafsi siwezi kuyataja mambo yote, ni mambo mengi sana ambayo ameyafanya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye halmashauri zetu fedha zinaingia kila siku na mambo yanakwenda vizuri. Asilimia mia moja ya bajeti tangu Mheshimiwa Rais ameingia madarakani ndiyo kwanza halmashauri zimepelekewa asilimia mia moja ya bajeti. Siku zote bajeti kwenda kwenye halmashauri ilikuwa haifiki asilimia mia moja. Mheshimiwa Rais anatekeleza miradi mikubwa ya kimkakati lakini wakati huo halmashauri zinaenda fedha zote kwa ajili ya matumizi ya Watanzania. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Rais kwa kuweka ruzuku ya mafuta na mbolea. Hili jambo watu hawalioni kwa sababu limepozwa na ruzuku ya Mheshimiwa Rais. Leo Mheshimiwa Rais kwa hali ilivyokuwa kipindi kile asingeweka ruzuku ya mafuta kila kitu kingekuwa juu, na pia asingeweka ruzuku ya mbolea sijui wakulima wetu wangelimaje; nampongeza sana Mheshimiwa, Rais tunaamini anawapenda Watanzania anawafikiria na kuwahudumia.

Mheshimiwa Spika, binafsi pia nimpongeze Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya. Amekuwa akizunguka nchi nzima kutatua matatizo ya Watanzania. Nampongeza na ninamtakia afya njema aendelee kufanya kazi yake. Niwapongeze pia waheshimiwa Mawaziri kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, leo najikita tu kwenye suala la tumbaku. Mimi nimezaliwa Tabora na tumbaku ndiyo imenikuza na kunifikisha hapa. Tumbaku Tabora ilishuka kwa kiwango kikubwa. Mwaka 2010/2011 tumbaku ikakataliwa kununuliwa mpaka tukaita makinikia, tulikosa kabisa masoko. Kwa hiyo tumepambana sana akiwepo Waziri Mkuu. Kabla ya mwaka 2010/2011 tulikuwa tunauza kilo milioni 120, lakini hapo katikati tumbaku yetu ilishuka mpaka tukafikia kilo milioni 60. Lakini tangu ameingia Mheshimiwa Rais Samia Suluhu madarakani miaka miwili na kidogo, tumbaku yetu imepanda sasa hivi tuna kilo milioni 130.

Mheshimiwa Spika, nikikuambia kilo 130 ina maana naongelea dola milioni tatu, nikiongelea dola milioni tatu; ina maana Tabora tunakwenda kupokea bilioni saba. Nikiuangalia Mkoa wetu wa Tabora na zile bilioni saba naangalia kabisa jinsi biashara zitakavyozunguka, mzunguko wa fedha utakavyokuwa mkubwa na maendeleo yatakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, lakini nampongeza pia Waziri wetu wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe kwa kazi kubwa aliyoifanya kwenye Tumbaku. Baada ya kuweka wanunuzi, pia wazawa, wamesaidia sana kuhakikisha tumbaku yetu hainunuliwi. Zamani tulikuwa tunawekewa *limit* kwamba tulime kilo kadhaa tusiongeze kwa sababu hakuna wanunuzi sasa hivi ninapokwambia wanunuzi wapo wanatafuta wakulima, wako wanawa-*convince* wakulima kwa kila aina ili waweze kulima tumbaku nyingi waweze kupata na wao kununua.

Mheshimiwa Spika, Serengeti na Manyoni walikuwa wameacha kabisa kulima tumbaku kwa sababu wanunuzi walikataa kwenda kununua tumbaku kule, lakini leo hii kwa kazi nzuri inayofanya na Rais wetu wanunuzi wamerudi na wanakwenda kuanzisha Serengeti na Manyoni, kwa hiyo naamini mambo yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika,tumetoka kuuza kila dola 1.6 mpaka dola mbili sasa hivi tunauza kwa dola tatu, na kutakuwa na matabaka aina saba ya kuuza kwa dola tatu. Pia tutauza kwa dola mbili tumbaku inayofatia na kuna matabaka 17. Unaweza ukaona zao la tumbaku litaingiza fedha za dola kwenye nchi yetu kwa kiasi gani. Nizidi kuipongeza Serikali, lakini pia nizipongeze kampuni binafsi zilizojitokeza kununua, leo hii kwa kampuni hizo, hasa za wazawa, kuwa nyingi…

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Sasa hivi mnunuzi wa tumbaku akipeleka tumbaku yake sokoni analipa na elfu kumi ya kula.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Jamani taarifa mpaka had Mheshimiwa Spika aseme…

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika,taarifa

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde kuna taarifa kwa Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani.

**T A A R I F A**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji, kuwepo tu kwa Mheshimiwa Rais kama Rais wa Tanzania kampuni za tumbaku *L10F* ambayo ni daraja la kwanza ilikuwa ni dola mbili lakini leo tunavyoongea ni dola 3.56, *L1F* ambayo ilikuwa ni dola 1.04 tunavyoongea leo ni dola 2.99. Pia uzalishaji alivyosema mchangiaji sasa tumetoka kwenye kilo moja wastani wa bei kwa nchi nzima dola 1.4 sasa ni dola mbili ambazo ni fedha nyingi sana kwa Watanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah unapokea taarifa hiyo?

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa ya Mheshimiwa Cherehani na ninamshukuru sana. Niendelee kuwashukuru kampuni binafsi. Fununu zilizopo sasa hivi kampuni moja ya Mkwawa sasa hivi imenunua kilo milioni 45, lakini msimu ujao itanunua kilo milioni 80.

Mheshimiwa Spika, na kwenye ilani yetu ya uchaguzi tunatakiwa kufikia 2025 tununue tumbaku kilo milioni 200, na kwa sasaa hivi tuna kilo 130. Tunaamini ifikapo 2025 tutavuka lengo ambalo limeandikwa kwenye ilani yetu ya uchaguzi. Nawapongeza sana viongozi wetu kwa kuhakikisha zao letu linakwenda vizuri, na tuna imani kubwa sana.

Mheshimiwa Spika,kwa hiyo niombe sasa Serikali kupitia Wizara ya Kilimo; wakulima wetu wa tumbaku hawakuwahi kupata mbolea ya ruzuku, walau walinunua mbolea imeandikwa ruzuku lakini waliuziwa kwa bei bila ruzuku. Niiombe Serikali, kupitia Wizara ya Kilimo waangalie, mauzo ya mara ya pili wawarudishie fedha zao wakulima wa tumbaku ili nao waweze kunufaika na keki ya nchi hii iliyotolewa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu na waweze kufurahia jambo lao na wao waweze kuwa wamepata mbolea ya ruzuku. Hii ni kwa sababu hawakupata mbolea ya ruzuku ya tumbaku wala ya mahindi kwa sababu tu ni wakulima wa tumbaku. Naiomba sana Serikali watakapokuja ku-*wind up* watuambie kwamba wako tayari kuwarudishia wakulima pesa zao.

Mheshimiwa Spika,ombi la pili, tunaomba Serikali iwaongezee uwezo wanunuzi wa tumbaku, hasa wanunuzi wazawa, ili wakulima wetu waweze kuuza tumbaku kwa ushindani mkubwa uliopo sasa hivi na uzidi kuendelea. Nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aingile kati mchakato wa pembejeo za kilimo zifike kwa wakati.

Pembejeo za kilimo ikiwemo mbolea safari hii imechelewa kuwafikia wakulima. Naamini jambo hili la ruzuku ndiyo tumelianza kipindi hiki kwa msimu wa kwanza kwa hiyo tunaamini changamoto ndogo ndogo lazima zijitokeze. Ninaamini wamezijua na wamezielewa; na ninaamini kipindi hiki cha msimu huu watatuletea ruzuku kwa wakati na pembejeo zote kwa wakati ili wakulima wetu waendelee kulima vizuri.

Mheshimiwa Spika, fununu zilizopo ni kwamba kuna Kiwanda cha Sigara kinatakiwa kujengwa Morogoro, kitu kinauma sana Tumbaku asilimia 60 inalimwa Mkoa wa Tabora viwanda vyote vya kuchakata tumbaku viko Morogoro. Nimwombe Mheshimiwa Waziri na yeye pia ametoka Tabora asikubali kiwanda cha Sigara kijengwe Morogoro. Tunaomba kiwanda cha Sigara kijengwe Tabora ili na sisi watoto wetu wapate ajira, lile jasho la tambuku wanalotoa wazazi wao na wenyewe waweze kuajirika. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aje atupe ahadi hapa kwamba kiwanda hicho kinajengwa Tabora na si Morogoro.

Mheshimiwa Spika, inauma sana tumbaku zote tunazolima, viwanda vyote viko Morogoro, hata sitaki kusema kwa nini. Zamani walikuwa wanasema umeme sasa hivi tuna umeme wa kutosha, walikuwa wanasema maji sasa tuna maji ya kutosha, sijui Mheshimiwa Waziri atakuja atuambie kitu gani ili tuweze kumuelewa.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye miundo mbinu, tuna barabara zetu kubwa za kimkoa. Tunaiomba Serikali itufanyie barabara hizi ambazo zimeandikwa kwenye ilani zaidi ya mara tatu bila matengenezo. Tuna Barabara ya Kahama – Kaliwa – Mpanda, hii imekuwa kwenye ilani tena zaidi ya mara mbili, mara tatu haijatekelezwa. Tuna Ipole – Rungwa ambapo ikijengwa na wewe Mheshimiwa Spika utanufaika, kwa maana ya biashara za Mbeya na Tabora. Tunaomba Barabara ya Tabora – Ulyankulu, tunaomba Barabara ya

Puge – Ndaya na Ziba, tunaomba sana Serikali itakapokuja kwenye bajeti yake ituambie nini hatima ya barabara hizi ambazo mmetuahidi mara kadhaa kwenye ilani ya uchaguzi lakini bado hazijatekelezeka.

Mheshimiwa Spika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa sekunde 30 malizia hoja yako, kengele imeshagonga.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nilikuwa nataka kuongea kuhusu Kaliua, Mbunge aliongea hapa, kaka yangu Kwezi, kuhusu Kata mbili za Usinge na Kakoko. Mheshimiwa Rais alikuja kule akaahidi wananchi wale waongezewe maeneo kwenye vijiji vyao; lakini tunashangaa wananchi wale wanatakiwa wahamishwe wapelekwe sehemu nyingine ilhali kuna kaya 1,300,

Mheshimiwa Spika, unaelewa ukiambia kaya 1,300 kuna akina mama, kuna Watoto na kuna wajane wamejenga; leo unapo mhamisha unampeleka sehemu mpya ilhali Mheshimiwa Rais alisha ruhusu, na tunajua kauli ya Rais ni maelekezo, ni maagizo, haiwezi ikaanza kuchakachuliwa. Mheshimiwa Rais aliagiza waongezewe maeneo pale walipo. Niwaombe sana Serikali wafuate amri ya Mheshimiwa Rais na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hayo naomba niunge mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Prof. Shukrani Elisha Manya atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, ajiandae.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja ya hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nipende kuipongeza Serikali kwa jinsi ilivyoandaa bajeti nzuri ambayo kweli kama itakavyokwenda kutekeleza kwa jinsi ilivyoandaliwa basi inakwenda kuleta tija na maendeleo makubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea hoja tatu kama muda wangu utaniruhusu. Hoja ya kwanza ambayo napenda kuiongea katika Bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni kupongeza jitihada za Serikali katika kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili. Katika ukurasa wa 90 wa hotuba hii inasema kwamba; "Kiswahili kimetafsiriwa katika lugha rahisi katika vyombo vinavyo toa haki kwa maana ya Sheria ya nchi lakini pia Kiswahili kimeendela kufundishwa katika vyuo vikuu vya nje ya nchi."

Mheshimiwa Spika, hili si jambo jepesi; na wote tunakumbuka kwamba Kiswahili kimeendelea kuwa nembo ya umoja wetu kama Watanzania lakini pia kimekuwa ndio msingi wa ustawi wetu kwa sababu sisi ni watu ambao tumetawayika sana kwa makabila na lugha zetu, lakini Kiswahili kimeweza kutuleta pamoja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizi kubwa za Serikali mimi ninavyoangalia ni kama vile umahiri katika lugha yetu ya Kiswahili na hasa katika lugha andishi unazidi kushuka; na hii ni kwa sababu utagundua kwamba matumizi ya nahau, semi, misemo, methali katika watumiaji wa Kiswahili yanazidi kushuka.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nitoe mfano mwepesi; ukiwaita vijana wa darasa la nne ambao tunaamini kwamba ndio wameweza kujua kusoma na kuandika halafu uwaambie hivi; ninaomba muniandikie jina la Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wa Ta'ala* baadhi yao wataliandika hilo

jina kwa herufi kubwa, lakini wengine wataliandika jina hilo hilo lakini kwa herufi ndogo, na sisi wote tunajua kwamba jina ambalo ni kuu kiasi hicho linapaswa kuandikwa kwa herufi kubwa na ni makosa sana katika vitabu vya dini kulishusha hadhi ukaliandika kwa herufi ndogo.

Mheshimiwa Spika, lakini msingi wa hoja yangu ni nini? Ni kwa sababu hawakujengwa kuelewa tofauti baina ya mambo haya; na sasa sisi tunataka kukipeleka Kiswahili chetu kama bidhaa kwa watu wa nje, sasa tunapelekaje Kiswahili kama bidhaa kwa watu wa nje kama sisi msingi wetu hapa ndani si mzuri?

Mheshimiwa Spika,kule kwetu Ukerewe iwapo unachochea viazi; maana viazi ni chakula kikuu kule kwetu; ukianza na moto mdogo mdogo baadae vile viazi hata ukichochea sana havitaiva kabisa. Maana yangu ni kwamba, kama msingi wa lugha ya Kiswahili utajengwa vibaya hapa chini katika shule za awali, maana yake tusitegemee maajabu huku juu.

Mheshimiwa Spika, na Waingereza walifanikiwa sana kukifanya kingereza kikawa ndiyo lugha takriban ya ulimwengu mzima. Sisi pia tunayo nafasi sasa. Yawezekana hii ndiyo nafasi yetu kama Watanzania kuifanya lugha yetu iweze kuwa ni lugha ya bara zima lakini pia iweze kuwa ni lugha ya mataifa mengine. Sisi ndio chimbuko, sisi ndio chanzo cha lugha hii ya Kiswahili. Kwa nini wenzetu majirani wafanye jitihada hatimae watupite?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nataka kusema, kwamba tunahitaji kujenga msingi imara wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ngazi zote kuanzia zile za awali; na ikiwezekana, na ikiwezekana tutumie nguvu kubwa kuwaomba wafundishaji wa Kiswahili wapigwe msasa ili watujengee watoto ambao wanaweza wakaongea kwa umahiri na wanaweza wakaandika kwa umahiri.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu huu usichukuliwe kama mjadala wa nini lugha ya kufundisha hasa katika Vyuo Vikuu, hapana. Mimi huwa si muumini wa mjadala huu, mimi ni muumuni wa kwamba kama mazingira yanaturuhusu tuwe mahiri katika lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha yetu ya Taifa; lakini pia tuwe mahiri katika lugha ya kingereza ambayo ni lugha ya biashara.

Mheshimiwa Spika, na unapokuwa mahiri katika matumizi ya lugha unakuwa na ujasiri. Yaani huwezi kwenda mahali umeitwa ukaongee ukatoe muhadhara, ujasiri utakuja kwa sababu ya huo umahiri. Kwa hiyo hoja yangu hapa ni kwamba, tunayo nafasi kama taifa la kubidhaisha Kiswahili chetu na kwa jinsi hiyo tuichukue kwa jitihada unganishi. Kama ni vyuo, kama ni watunga Sera, kama ni wafundishaji basi tulishughulikie jambo hili ili hatimaye na sisi tuweze kupenyeza lugha yetu kuwa lugha ya kimataifa lakini iliyojengewa msingi imara.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni katika ukurasa wa 29 wa Bajeti ya Waziri Mkuu. Katika ukurasa huo tunapongeza jitihada za Serikali ambazo zimeelekezwa katika kuongeza bajeti ya kilimo, kupanua eneo la umwagiliaji na kuweka ruzuku katika mbolea na upatikanaji wa mbegu bora kama mahitaji muhimu ya kufanya kilimo chetu kiweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kuna jambo hapa ambalo huwa linasahauliwa na jambo hili ambalo linasahauliwa ni la mkulima yule mdogo mdogo. Hapa ndani ya Bunge utakuta kuna Wizara yenyewe inajinasibu na ni jambo zuri kwamba tunataka tumtue mama ndoo kichwani, jambo ambalo linapongezwa sana kwa sababu ni kweli Wizara ya Maji wamefanya jambo kubwa sana, lakini huyu mkulima mdogo nilitamani hata kama sio katika bajeti hii, tuje na *slogan,* tuje na usemi wa kwamba ni lini tutamtua mkulima mdogo wa nchi hii jembe la mkono?

Mheshimiwa Spika, lile jembe linafanya tu mikono inakuwa sugu, halina tija, yaani mtu analima hekari nyingi sana, anatumia muda mrefu sana na kula yake inakuwa ni ngumu na hawezi kupata maendeleo kupitia jembe hili la mkono. Kwa hiyo, mchango wangu ni kwamba kama haiwezekani katika bajeti hii, lakini tuje na Mkakati ambao utamtua mkulima mdogo wa nchi hii jembe la mkono. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya tatu, naamini muda wangu unaruhusu ni matumizi ya mifumo ya TEHAMA. Serikali imefanikiwa sana na hasa ilipoanzisha mfumo ule wa *GEPG* katika makusanyo ya fedha za Serikali. Pia lengo lingine la kuwa na mifumo hii pamoja na kurahisisha kutoa huduma, lilipaswa kuwa ni kupunguza ubadhirifu kupitia mifumo hii. Sasa katika Ukurasa wa 70 katika hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu wanasema kuhusu habari za rushwa, kesi za rushwa zilizoendeshwa mwaka 2022 ni 696 na 248 ziliamuliwa na 142 walikutwa na hatia".

Mheshimiwa Spika, sasa katika utendaji wa Serikali Afisa Masuuli yeye *check* yake ni yule Mkaguzi wa Ndani, lakini pia Afisa Masuuli hawezi kuamua kutoa fedha katika akaunti ya benki bila kuwa na Mhasibu. Hivi kwa nini rushwa inaendelea kutawala? Kwa nini ubadhirifu unaendelea kuwepo? Je, ni kwa sababu hatua zinazochukuliwa ni kidogo? Je, hawa watu wanatoa wapi ujasiri? Kwa nini hawana hofu? Je, hatua zinapochukuliwa zinahusisha watu watatu au idara tatu ya Afisa Masuuli mwenyewe, ya yule Mkaguzi wa Ndani na yule Mhasibu wake wote wanashirikiana katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, tungetamani kuiomba Serikali, mifumo ya TEHAMA inayoanzishwa iweze kuwa na lengo la makusudi la kuhakikisha kwamba kila mtu anapata mrejesho ili kudhibiti ubadhirifu wa mali ya umma.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwamba, wakati mwingine mifumo hii ya TEHAMA inakuwa ndio sababu ya hasara kwa wananchi. Mfano mdogo kabisa, mfumo unakuwa uko *down* pale Bandari, kwa mfano, mtu anayetoa gari, halafu siku zikipita hasara inakuja kwa mwananchi wakati mfumo ulikuwa ni hasara ya Serikali. Hebu watusaidie mifumo iweze kuwa sababu ya kurahisisha, lakini pia kutoa huduma ambayo ni njema ambayo haimpi hasara yule ambaye ni mwananchi wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hivyo, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nasikiliza kwa makini Kiswahili kilichonyooka Kiswahili fasaha na hapa nimeyasikia maneno mawili tu ya Kiingereza *slogan* na *down,* naona ni kwa ajili ya uharaka.

Waheshimiwa Wabunge tujifunze, sisi kama ndio Mama wa Kiswahili basi tuzungumze Kiswahili na kama huyu ndio Profesa maana yake na Kiingereza anakijua. Sasa mwenzangu na mimi basi, kila sentensi ushajaza maneno ya Kiingereza kama vile Kiswahili ndio hukijui vizuri. Haya sijui kama na Waingereza wakiongea cha kwao wanachanganya na Kiswahili? hapo sijajua.

Mheshimiwa Godwin Kunambi atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Maganga na Mheshimiwa Mary Masanja ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nianze kuungana na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais hasa kwa kazi kubwa anayoifanya katika kutuletea maendeleo Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mlimba tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mlimba ilikuwa haina hospitali ya wilaya lakini hadi sasa ninapozungumza hospitali ya wilaya inakamilika na tunatarajia mwezi Desemba huduma ianze kutolewa. Vile vile tunamshukuru Mheshimiwa Rais katika miradi ya maji. Tuna Miradi mikubwa ya Maji pale Mlimba Mjini inayokwenda kutoa huduma katika vijiji 11 ambapo Mradi wa Mlimba una thamani ya Shilingi Bilioni 3.7, lakini pia tuna Mradi wa Mbingu - Igima ambao thamani yake ni Shilingi Bilioni 3.6. Jambo hili jambo jema kwa wananchi wa Mlimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi, wakati naingia Bungeni hapa kwa mara ya kwanza nilieleza. Changamoto ya kwanza kwa wananchi wa Mlimba ukiwauliza ni barabara, changamoto ya pili kwa wananchi wa Mrimba ukiwauliza ni barabara na changamoto ya tatu kwa wananchi wa Mlimba ni barabara. Mheshimiwa Rais amesikia kilio cha wananchi wa Mlimba na kwa dhati kabisa namshukuru. Leo hii tunapozungumza Mheshimiwa Rais amekwishatoa kibali cha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami inayoitwa Morogoro – Njombe *Border* yenye urefu wa kilomita takribani 222. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa awamu hii ya kwanza barabara hii itaanza kujengwa kilometa 100 kwa *route* mbili, *route* ya kwanza ni kutoka Ifakara mpaka Mbingu kilometa 67.5 na *route* ya pili ni kutoka Mbingu mpaka Chita pale Kambi ya Jeshi kilometa 37.5 na hiyo itahitimisha kilometa 100.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili kwa kilomita zilizobaki, Mheshimiwa Rais amepata kupitia mahusiano aliyojenga na Taifa letu na mataifa mengine hasa na taasisi za kifedha duniani. Benki ya Maendeleo ya Afrika imeridhia kufanya usanifu wa mradi wa barabara kipande kilichobaki cha

kilomita 122 kutoka Kihansi mpaka pale Madeke, kwa maana ya upande wa Njombe. Katika hili tuna kila sababu ya kujivunia Mheshimiwa Rais na sisi Wanamlimba tunamwahidi ifikapo 2025 tutampa kura zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye eneo lingine, eneo la elimu na hasa leo hii nitazungumzia suala la elimu ya ufundi. Hapo nyuma elimu ya ufundi ilikuwa inatolea katika taasisi tatu. Taasisi ya kwanza ilikuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia, tulikuwa na Vyuo kama Dar es Salaam *Institute of Science and Technology* kwa maana ya *(DIT),* tulikuwa na taasisi pia ya Elimu ya Sayansi na Teknolojia kule Mbeya *(Mbeya Institute of Science and Technology)* na sasa hivi vyuo hivi viwili vyote vimepoteza hadhi hiyo. Leo hii ukienda Mbeya kuna Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya sio Taasisi ya Elimu ya Sayansi na Taeknolojia. Ukienda Dar esSsalaam kuna Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Dar es Salaam na sio Taasisi ya Elimu ya Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, vyuo hivi vimepoteza haiba ya kuzalisha wanafunzi ambao wanakuwa na maarifa na ujuzi na matokeo yake sasa Taifa letu tunakuwa na vyuo vikuu vingi na elimu ya chuo kikuu *basically* kwa asilimia kubwa inaandaa wanafunzi kwenda kuajiriwa. Hata hivyo, sio tu kuajiriwa inaandaa *Managers,* lakini elimu ya ufundi inaandaa watu wanaokwenda kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rai yangu, ombi langu na ushauri wangu kwa Serikali, ni muhimu sasa itazame upya suala hili na kwa sababu Taifa letu lina changamoto kubwa ya kada ya Mafundi Mchundo. Nieleze jambo hapa, katika safari yangu ya elimu nilibahatika kusoma Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi pale Kibaha, nilisoma elimu ya ufundi miaka miwili na nilisomea ufundi wa magari na mitambo.

Mheshimiwa Spika, vyuo hivi asili yake ni Sweden, Baba wa Taifa alianzisha vyuo hivi mahususi kulifanya Taifa letu liwe

na vijana wengi wenye ujuzi lakini vyuo hivi leo hii vimesahaulika kabisa na nikisema nadhani hapa Waheshimiwa Wabunge watakuwa mashahidi, baadhi nikiwambia *FDC* ni neno jipya kwao leo. Kuna Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ambavyo viko Kibaha, Ifakara pale kipo Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Ifakara. Sasa vyuo hivi ni muhimu kwa sababu vinatoa ujuzi zaidi ya *VETA*. Vijana wanasoma elimu ya ujasiriamali, vijana wanasoma elimu ya uchumi na fedha, vijana wanasoma elimu ya uhasibu. Sasa ombi langu na ushauri wangu kwa Serikali ni muhimu sasa ikatazama vyuo hivi, fedha zipelekwe.

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, eneo la tatu la ufundi ni Vyuo vya *VETA* na hii namshukuru Mheshimiwa Rais, tumepata fedha Halmashauri ya Wilaya Mlimba kwa maana ya Wilaya ya Kilombero, tumepata fedha za ujenzi wa Chuo cha *VETA* na Chuo kile kinakwenda kujengwa pale Mlimba, Kata ya Mchombe, Kijiji cha Lukolongo. Kwa hiyo, hii ni fahari kwa wananchi wa Jimbo la Mlimba hususani wa Kata ya Mchombe na Kijiji cha Lukolongo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ninapokwenda kuhitimisha hoja yangu, ni eneo la mahusiano baina ya Mamlaka za Upangaji na Wizara ya Ardhi kama Msimamizi wa Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, hapo awali kwa mujibu wa Sheria Namba 8 ya Mwaka 2007 ya Mipango Miji, mamlaka za upangaji ni halmashauri zote nchini na mpaka sasa ipo hivyo. Changamoto inayojitokeza sasa kupitia Waraka wa Utumishi wa Ardhi, Watumishi wa Ardhi walihamishwa kutoka Halmashauri kwenda Wizara ya Ardhi, sasa nini nafasi ya Mkurugenzi wa Halmashauri katika kumsimamia Afisa Ardhi ambaye yuko kwenye Halmashauri yake? Kuna ombwe hapo, ndio maana leo hii migogoro ya ardhi imekithiri nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi yeye ndio mwajiri, yeye ndiye anayepandisha madaraja ya watumishi wa kada ya ardhi. Mkurugenzi wa Halmashauri anaambiwa na niseme kwa dhati, ukiangalia Maafisa Ardhi walioko kwenye halmashauri hawatofautiani na tunaita kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kuna mtu anaitwa Mshauri wa Mgambo, yule pale amekwenda kuhifadhiwa tu na wanashauriana na Mkuu wa Wilaya ila Mkuu wa Wilaya hana Mamlaka ya kumuagiza Mshauri wa Mgambo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, leo hii nitoe mfano, Mkurugenzi wa Halmashauri amempangia kazi Afisa Ardhi, Kamishna wa Ardhi wa Mkoa naye anamwita, sasa huyu Afisa Ardhi anakwenda wapi? Anamsikiliza Mkurugenzi wa Halmashauri au anakwenda kwenye Mamlaka yake Mkoani?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA**: Mheshimiwa Kunambi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Angelina Mabula.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii. Napenda nimpe taarifa msemaji asitake kupotosha. Waraka uliohamisha Watumishi wa Ardhi kwenda Wizarani ndio ule ule uliowataja watu wa *TARURA*, ndio uliotaja watu wa maji.

Mheshimiwa Spika, la pili, kiutendaji wale watu wako *hundred percent* kwenye halmashauri kwa sababu Halmashauri ndizo Mamlaka za Upangaji. Sasa hauwezi kuwa Mamlaka ya Upangaji usiwe na sauti na yule mtu. Kwa hiyo, kama analalamikia kwamba ardhi Mkurugenzi anakosa sauti, kwa nini *TARURA* wanafanya kazi? Kwa nini Wizara ya Maji wanafanya kazi na waraka uliohamisha majukumu ulikuwa ni ule ule mmoja? Wameletwa Wizarani kwa ajili ya ajira na

nidhamu na adhabu zozote zinaanzia kwenye halmashauri husika kabla ya Katibu Mkuu kuweza kutoa. Kwa hiyo, hakuna ambacho kimeharibika katika hilo isipokuwa Wakurugenzi wanataka kukwepa majukumu yao kwa kusingizia kwamba hawa watu huwa wako Wizarani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunambi unapokea taarifa hiyo?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, namheshimu sana Mama yangu, lakini sipokei taarifa hiyo. Labda nieleze, ukizungumzia *TARURA* ni *independent,* wanajitegemea hawako kwenye Halmashauri, ndio maana wanafanya vizuri, ukizungumzia watu wa Maji *RUWASA* ni taasisi inayojitegemea, hawako kwenye Halmashauri, sasa ukitoa Mfano wa *RUWASA* na *TARURA* hapana.

**SPIKA:** Dakika moja malizia

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba nishauri, ili kuboresha ufanisi wa Sekta ya Ardhi nchini, Wizara ya Ardhi ikae na Wizara ya TAMISEMI, warejee huu waraka waone ni namna gani Mkurugenzi wa Halmashauri anakwenda kuwa na mamlaka ya kumwagiza Afisa Ardhi na watu wa mipango miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nicodemas Maganga atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Masanja na Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu ambayo ina *page 95,* imegusa maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza napenda nianze kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa mambo anayonipa ushirikiano kwenye Jimbo langu la Mbogwe na ikumbukwe tu tarehe 8 Aprili, nimefanya Mkutano pale Kata ya Ilolangulu Kijiji cha Nyashinge, nimepokea malalamiko mengi ya wananchi yanayoishutumu Serikali. Hata hivyo, nimpongeze Rais maana amekuwa ni Rais wa mfano katika Jimbo la Mbogwe. Mbogwe ilikuwa haijawahi kutengenezewa lami, lakini kwa awamu yake tumepokea lami kilomita tano. Mheshimiwa Rais ametu-*balance* hata kwenye upande wa maji japokuwa kuna maeneo mengine bado hayajaguswa, nizidi kumwombea kwa Mwenyezi Mungu Mama yangu aendelee kuwa na moyo wa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ametupatia miradi ya umeme pamoja na mambo mengi luluki. Wananchi wangu walikuwa na njaa ya kufa mtu, niishukuru Wizara ya Kilimo nilikuwa nikilia wananisaidia, Mheshimiwa Bashe Mungu amlinde sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukurani hizo, sasa uniruhusu kidogo nijaribu kuingia kwenye ilani yetu ambayo ni mkataba wetu na wananchi waliotuchagua.

Mheshimiwa Spika, neno la Mungu linasema "*watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa*". Hapo nipo kwenye maandiko kwanza bado sijaingia kwenye ilani. Ukisoma ukurasa wa 52, unaelezea bayana kwamba wananchi tuliwaahidi nini? Wizara ya Ardhi tulipanga kwamba tutatenga hekari milioni sita kwa ajili wananchi kuchungia ng'ombe pamoja na kilimo. Leo naweza nikasema kwamba haya maswali yanaulizwa sana na wananchi. Ni wapi ambapo tumetenga hasa eneo langu la Mbogwe? Kwa vile Mawaziri wapo sasa wawe makini ili waweze kunijibu huko mwishoni na uzuri Waziri wa Maliasili anakuja kuingia ajipange sasa kuja kunijibu kama anavyonifahamu kaka yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mbogwe wanapata tabu kwenye mapori. Sheria zinasema mita mia tano, ukisogea mita mia tano ng'ombe wanataifishwa, lakini hapa tuliwaahidi wananchi kwamba tutawatengenezea maeneo na wanifundishe sasa kwa vile hili suala liko kiilani halafu mpaka sasa hivi bado hawajatenga maeneo wananitakia nini mimi Mbogwe?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nigusie kidogo sheria zetu ambazo tumezipitisha hapa Bungeni, zimekuwa zikileta mkanganyiko mwingi kwa wananchi. Lazima Serikali tuishauri vizuri. Ukiangalia Sheria za Madini zinasema mtu anaweza akaomba kwenye mtandao akapatiwa leseni hata kama kuna nyumba. Suala hili kwa vile yananitokea na ninayaishi, yameleta mkanganyiko mkubwa sana kwa wananchi wa Mbogwe. Ukiangalia Kata ya Kanegele migogoro ni mingi Bukandwe pamoja na Masumbwe, wananchi wamekuwa wakilia sana. Mbaya zaidi hawa wawekezaji pale wanapozipokea hizi leseni hawasomi Sheria zinasemaje. Wanaingia na Mapolisi, wanafukuza watu, hawalipi fidia, wanajali masilahi yao, matokeo yake hii nchi inakuwa kama vile imepoteza mwelekeo.

Mheshimiwa Spika, tukikumbuka enzi za Mwalimu Nyerere aliishi vizuri na watu, aliwasikiliza wanyonge. Tunatambua sera yetu ni kukaribisha wawekezaji, lazima tufikirie hawa wawekezaji wanaoingia ni wazuri kwetu au ndio watatutoa madarakani? Tatizo hili hata Chunya, Mbeya lipo, maeneo yote yaliyozungukwa na migodi yanasumbua watu sana. Nikuombe wewe ni bosi wetu hapa Bungeni, utoe maelekezo ikiwezekana kuanzia kwenye Kamati zetu ili tuziangalie upya. Hii sheria inakinzana sana na wananchi wanyonge wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine niongezee hapohapo na Mawaziri, tuna Baraza la Mawaziri 24 lazima tuangalie vizuri, hawa Mawaziri wanamsaidia kweli Mama hawa?

Lazima tuwaangalie hawa Mawaziri 24, wanamsaidia Mama au wanaendesha V8 halafu wanakalia kusema Mama anaupiga mwingi? Wananchi wa kawaida waliumia sana juzi wakati Mama anakabidhiwa ripoti ya *CAG,* kauli aliyoitumia ni lugha ya Kiingereza, alisema *stupid! (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais ni mtu mkubwa sana kufikia kusema neno pumbavu na mtupishe wakati kuna watu wake wanaomsaidia, ina maana wao hawaoni matatizo haya, hata kama matatizo haya yanafanywa na wataalam. Kwa nini Mawaziri wasichukue hatua mapema? Mwishowe hili suala mbona linatugharimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwaombe Mawaziri, sina bifu na ninyi na wala sijaja kutafuta ugomvi hapa, hebu kila mmoja ajitathmini kwenye nafasi yake anamsaidiaje Mama hasa anapoenda Ikulu kukaa naye? Nikiangalia Wizara zipo 24 mpaka na Naibu Mawaziri hawa watu wanatumia kodi za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuingiza suala la maridhiano kwamba vyama sasa tuanze mchakamchaka sasa ndiyo tutajuana sasa mwaka 2025 ni nani Mwanamme na Mwanamke ni nani? Maandamano yameruhusiwa itafika sehemu tuchoke kuwashauri hapa Waheshimiwa Mawaziri hamchukui hatua, kitakachofuatia sisi ni kuandamana na wananchi kuja kwenye familia zenu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siwezi nikakubali kukalisha wananchi fedha zimeliwa na watu wanajulikana!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mchangiaji kwamba mwaka 2000….

**SPIKA:** Subiri kuitwa Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Nicodemas Maganga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, mpatie ili nimsikilize. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mchangiaji kwamba mwaka 2025 au 2030 tutakutana watu wenye sifa na siyo habari ya mwanamke na mwanaume, kusema kwamba nani atakuwa mwanaume na mwanamke ni kudhalilisha wanawake ambao wanafanya kazi nzuri na njema, saa nyingine kuliko hata wanaume. Haya ni masuala ya ushindani wa vigezo siyo masuala ya 'ME' na 'KE', afute hiyo aliyoisema.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa sababu umemtaka afute hiyo kauli yake. Kwanza hatupiti kwenye Kanuni ya Taarifa kama unataka mtu afute kauli. Pia mimi nilikuwa nafuatilia mchango wake anaelekea wapi kwa sababu niliyekaa hapa mbele ni mwanamke na aliyekuwa anamsifia pia ni Rais ambaye ni mwanamke. Kwa hiyo, nilikuwa naangalia hoja yake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa naisikiliza hoja yake niielewe halafu ndiyo nijue yale maneno yake yametumika isivyo ama yako sawasawa. Kwa hiyo, kwa kuwa umeomba kuhusu kufuta wacha nimruhusu aendelee na hoja yake kama kutakuwa na hiyo sababu baada ya kueleweka hoja yake, kwa sababu anaendelea kuzungumza tutajua kama anatakiwa kufuta au hapana. Endelea Mheshimiwa Maganga. *(Makofi)*

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nakushukuru kwa kunipa nafasi nilindie na muda wangu ili kusudi niweze niweze kuwasilisha mchango wangu

vizuri na sikuwa na maana mbaya kwamba nani mwanaume na mwanamke atajulikana maana yake ni nani mchapakazi ambaye anastahili kuaminiwa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tumlinde Rais wetu kwa wivu na nguvu zote, tumekuwa na Naibu Mawaziri tukiwapigia hata simu Wabunge hawapokei, tunawandikia meseji ili washughulikie matatizo ya wananchi hawatujibu. Tunatambua Wizara zipo 24 ambapo mimi Mbunge kwa nafasi yangu ni kuchukua changamoto na kuipeleka mahala husika, ndiyo maana nasema hizi Wizara ziangaliwe upya, mpaka nafika sehemu mbali sana mimi kufikiria hivi! Hivi hawa kwanza waliteuliwaje yaani mpaka nachanganyikiwa nashindwa kujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Wizara ya Afya madawa hakuna kwenye vituo vya afya, kilio kila mahala, pale Masumbwe nina kituo kikubwa sana akina Mama wengi wanahangaika. Naishukuru Serikali ilileta vifaatiba lakini mpaka leo havijaanza kufanya kazi, Mawaziri wapo hawahawa wanabadilishwa mara yupo Ustawi wa Jamii mara Maendeleo ya Jamii lakini hawafanyi kazi kiukweli, lazima tushauriane vizuri, najua ni chungu itawauma lakini ukweli lazima tuuseme. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la mikataba. Kwenye suala la mikataba najua kuna Waziri wa Mikataba hapo kuwa makini uje unijibu. Ile Halmashauri ya Mbogwe imeanza kujengwa toka mwaka 2016, Halmashauri ya Mbogwe mpaka leo ni mwaka wa Saba bado haijaisha, Mkandarasi alishakula fedha, Halmashauri tulishaazimia kwamba tupewe hata Mkandarasi mwingine, mpaka sasa hivi Milioni 700 zipo zimekaa tu kwenye *account,* mikataba haieleweki! Nakuomba utusaidie Mbogwe tuko *busy* kwanza tulishacheleweshwa zamani mno, ndiyo tumepata kafursa ka huyu Mama anatusaidia na anatusikiliza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kingine, ninyi Mawaziri ni marafiki zangu lakini inakuja suala la wananchi mimi sina urafiki. Upande wa Jeshi la Polisi Mbogwe ni Mji mkubwa Askari hawajulikani wanalala wapi? Gari la zimamoto hakuna, nyumba zimejengwa nzuri nyingine zinaungua, kila siku ninauliza maswali humu mnashughulikia mtaleta, hakuna kuona kitu kinatekelezeka. Naomba Waziri kwa vile hii hotuba ya Waziri Mkuu imegusa vitu vyote na wewe ujipange unanisaidiaje Mbogwe ili kusudi niendelee kuwa Mbunge mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla hatujaanza mikutano mwaka kesho niwaombe sana Mawaziri wengi nimewataja, kuna Waziri wa Biashara, kuna Waziri sijui wa Mifugo, kuna Waziri wa Kilimo mbolea na zenyewe ilikuwa shughuli, tulikuwa tunamaliza mikutano kisera vilevile kuna Waziri wa Habari na Mawasiliano mitandao ina-*scratch* kila wakati lakini inaonekana kwenye maeneo mengine, Waziri wa Nishati na wewe umeme unakatikakatika kila siku majibu hayaeleweki, lazima tushauriane vizuri ili kusudi hata kama tunapongezana suala liko sawasawa, tusikalie kupongezana tu lazima tusuguane ili kusudi tuendelee kushika Serikali.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kunipa muda huo nikushukuru sana na Mungu akubariki sana. Ahsante sana *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya hasa ndani ya jimbo langu la Kwela.

Mheshimiwa Spika, pili nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri unayoifanya, hasa kwa ziara yake aliyoifanya jimboni Kwela mwezi Desemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwa njia ya maandishi kwenye bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu; kwanza nianze kwa kumkumbusha Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya ahadi yake aliyoitoa siku alipofanya ziara Jimboni kwangu, juu ya ujenzi wa hospitali yenye hadhi ya wilaya katika Mji Mdogo wa Laela ambao pia ndio Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiodhihirika kwamba Hospitali ya Wilaya iliyojengwa kwenye jimbo langu ipo umbali wa zaidi ya kilometa 330 ambapo imekuwa ngumu kufikiwa na wananchi hasa waliopo Ukanda wa Ufipa ya Juu ambao ni takribani wananchi 200,000.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichangie kuhusu mgogoro wa ardhi uliopo kati ya mwekezaji wa shamba la Malonje yaani *Efatha Ministry*. Mgogoro huu umechukua muda mrefu sana. Nilisema humu Bungeni mwaka jana na Serikali ikaahidi kuchukua hatua, lakini mpaka sasa hamna hatua yoyote. Nikuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu utusaidie ili tuweze kumaliza tatizo hili lililochukua muda mrefu.

Lakini pia mgogoro wa Gereza la Mollo lililopo Wilaya ya Sumbawanga na wananchi wa Kata ya Msanda Muungano juu ya kukabidhiwa ekari 495 walizoahidiwa na Waziri wa Mambo ya Ndani alipozuru eneo hilo. Lakini ni mwaka wa tatu sasa hamna hatua yoyote iliyochukuliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya kukabidhi ardhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichagie hoja ya hotuba ya Waziri Mkuu ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2023/2024 na namshukuru Mungu kwa zawadi ya uzima na afya njema.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwaletea maendeleo Watanzania, miaka miwili ya uongozi wake tumeshuhudia ubora wa miundombinu madarasa na vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, napongeza kazi nzuri inayofanywa na Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango. Pia nampongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa umahiri wa kazi kubwa anayofanya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, mkoa wa Lindi haujaunganishwa na mkoa wa Mtwara au mkoa wowote kwa barabara kwa kiwango cha Lami. Tunaomba barabara inayotoka Masasi kupitia Nachingwea hadi Liwale ijengwe kwa kiwango cha lami mwaka huu 2023/2024, tafadhali tafadhali tumeahidiwa mara kadhaa haifanyiki.

Mheshimiwa Spika, tunaomba pia kupata maji safi na salama katika Kata za Ngunichile, Lionja, Mbondo kule Wilaya Nachingwea, hali mbaya bado akinamama wanahangaika kutafuta maji, wanakesha kutafuta maji hii ni hatari kwa usalama.

Mheshimiwa Spika, tunaomba ujenzi wa viwanja vya ndege Nachingwea na Lindi vijengwe kwa kiwango cha lami. Hii ni kwa sababu ya usalama, pia kinatumika na Mheshimiwa Waziri Mkuu anapoenda jimboni kwake Ruangwa, lakini pia kuna machimbo ya madini pale Nachingwea na Ruangwa, hii itavutia wawekezaji ndani na nje ya kupata usafiri wa uhakika, lakini pia Nachingwea kuna vikosi vya majeshi ya

Jeshi la Wananchi Tanzania pia ni kwa sababu za kiusalama na utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Lindi kuna mradi mkubwa wa *LNG* hivyo kuhitaji usafiri wa ndege kwa saa 24 na wenye kiwango cha lami kwa mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee ninaomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza miaka miwili wa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii. Na pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mawaziri, na Naibu Mawaziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka. Tathmini zinathibitisha mafanikio yao mazuri ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu. Ukuaji wa uchumi wa Tanzania kwa mwaka 2022 umepungua hadi kufikia wastani wa asilimia 4.7 kutoka ukuaji wa asilimia 4.9 mwaka 2021 na kuongezeka hadi kufikia asilimia 5.3 mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri iliojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya ushindani wa Kimataifa *(National Competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2022 mpaka Machi, 2023 Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kimkakati kwa mafanikio mkubwa sana na utekelezaji huu unaonekana mpaka kwenye ngazi ya Halmashauri zetu. Mafanikio makubwa yamejikita kwenye uboreshaji wa miundombinu ya barabara, reli, bandari, mtandao wa mawasiliano na uboreshaji wa usafiri wa anga. Naipongeza Serikali kwa hatua nzuri za utekelezaji wa mradi wa kihistoria wa ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* na ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (megawati 2,115). Miradi hii miwili ya *SGR* na umeme ni nguzo imara ya kiushindani katika uchumi wetu na nchi za Maziwa Makuu na hata za Kusini mwa Afrika na Kati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, uchumi wa dunia umekumbwa kwa kiasi kikubwa na athari za UVIKO-19 na hivi sasa kuathirika zaidi na vita ya Urusi na Ukraine. Hivi karibuni kumekuwepo na taarifa katika nchi jirani za changamoto za ukwasi, uhaba na upandaji wa bei kwenye bidhaa za petroli, ujenzi, vyakula, nishati na hata pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na athari za UVIKO-19 na vita ya Urusi na Ukraine, Serikali inatakiwa kuendelea

kuchukua hatua za kibajeti kukabiliana hasa na mfumuko wa bei na kuporomoka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani na sarafu kuu zingine. Kwa kuzingatia kuyumba kwa uchumi wa dunia, bajeti hii ijielekeze kuchukua hatua za kuchochea uzalishaji wa ndani ili kupunguza *balance of payment – BOP,* kuimarisha Pato la Taifa kupitia sekta za kilimo, madini, utalii na uchukuzi. Hatua hizi ziende sambamba na kuimarisha mazingira ya uwekezaji hasa kwenye sekta ya kilimo na madini.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali iendelee kusimamia sera ya fedha na bajeti ikiwemo kuimarisha mifumo na kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Kutokana na mfumuko wa bei kwenye bidhaa za petroli na mtikisiko wa thamani ya shilingi, kutapelekea mahitaji zaidi ya fedha za kigeni na hivyo msukumo uwepo kwenye kuongeza uzalishaji wa madini na mazao ya kilimo. Hatua hizi ni muhimu kuhakikisha utulivu wa thamani ya shilingi na pia kuimarisha uhimilivu wa deni la Taifa hasa kwenye kigezo cha ulipaji wa deni la nje kwa kulinganisha na uuzaji wa bidhaa nje (mapato ya fedha za kigeni).

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto za vita ya Urusi na Ukraine, bado kuna fursa kubwa kwa Tanzania hasa kwenye uzalishaji wa ziada wa nafaka kuziba pengo la nafaka kutoka Urusi na Ukraine kwenda nchi kadhaa za Afrika na mabara mengine. Serikali iimarishe upatikanaji wa pembejeo bora kwa bei nafuu na kuimarisha upatikanaji wa masoko ya uhakika. Kutokana na ruzuku kwenye mbolea na jitihada walizofanya Wizara ya Kilimo kuwapatia vitendea kazi Maafisa Ugani, ichochee kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo kutoka uzalishaji wa sasa wa kilo 1,000 za mahindi kwa eka mpaka kilo 4,000 kwa eka ya mahindi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na msukumo kwenye kilimo, madini na utalii, Serikali inatakiwa kuwekeza hasa kwenye miundombinu ya usafirishaji ikiwemo barabara, reli, bandari

na usafiri wa anga hasa kwa mizigo. Katika Halmashauri zetu tumekuwa tunakabiliwa na changamoto hasa kwenye miundombinu ya barabara. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, barabara zinazohudumiwa na *TARURA* kwa asilimia zaidi ya 80 zipo kwenye hali mbaya sana kwa kukosa matengenezo ya mara kwa mara. Maeneo mengi ya vijijini barabara hazipitiki kutokana na ufinyu wa bajeti ukilinganisha na mtandao wa barabara zinazohudumiwa na *TARURA*. Naomba Serikali ichukue hatua za haraka kunusuru hali hii ili wananchi waweze angalau kusafirisha mazao yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuidhisha ujenzi wa barabara ya njia nne kuanzia Nsalaga (Uyole) mpaka Uwanja wa Ndege wa Songwe. Kipande hiki cha barabara ambacho ni sehemu ya barabara kuu ya *TANZAM,* ni muhimu sana kwa kuinua uchumi wa Tanzania na hata kupunguza ajali za mara kwa mara zinazotokea katika mteremko wa Mlima Iwambi kuelekea Mji wa Mbalizi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa usafirishaji wa mazao yetu kwa soko la ndani na nje ikiwemo fursa za biashara ukanda wa *SADC* na uzalishaji mkubwa kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, napendekeza muendelezo wa uboreshaji wa barabara za *TANZAM* kipande cha Igawa - Tunduma; barabara ya *bypass* ya Uyole - Songwe; barabara ya Mbalizi – Shigamba – Isongole kutokana na uzalishaji wa mazao ya kilimo; barabara ya Mbalizi – Galula – Makongolosi kutokana na uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo na madini; na pia barabara ya Isyonje – Kikondo – Makete.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi kubwa kuhakikisha ujenzi wa *SGR* unaendelea kwa kasi ile ile na pia napongeza jitihada za kuendelea kutafuta vyanzo vya fedha vya masharti nafuu kugharamia ujenzi huo. Pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa, Serikali imefanya maboresho makubwa ya miundombinu na huduma katika bandari zetu hususan

bandari ya Dar es Salaam ili kukabiliana na ushindani mkubwa wa bandari zingine za ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika. Bandari ya Dar es Salaam inakumbana na ushindani mkubwa toka bandari za Mombasa (Kenya), Beira (Msumbiji), Nacala (Msumbiji), Durban (Afrika Kusini), Lobito (Angola) na Walvis Bay (Namibia). Maboresho ya bandari zetu iendane na kuondoa changamoto zingine ambazo zinasababisha gharama kubwa za usafirishaji kwa bandari zetu na kusababisha kupoteza biashara ya usafirishaji kwa bandari shindani. Ufanisi wa bandari unategemea pia maboresho ya barabara, reli ya kati *(TRL),* Reli ya *TAZARA,* utendaji wenye tija wa wadau wote wa bandari na hata watumishi ili kupunguza gharama za usafirishaji kwa wateja wa bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa zilizopo, karibu asilimia 72 ya mzigo wote wa nchi za nje unasafirishwa kwa kupitia *Dar es Salaam Corridor* ambapo DR Congo ni asilimia 36, Zambia asilimia 31 na Malawi asilimia tano. Pamoja na fursa za kijografia ya bandari zetu, mzigo unaopita sasa kwenye bandari ya Dar es Salaam ni asilimia 50 tu ya biashara yote ambayo kwa sasa inashikiliwa na bandari shindani. Kwa ajili ya kunusuru biashara hii inayopotea kwa bandari shindani, Serikali ichukue hatua za haraka kuboresha huduma za *TAZARA* ikiwa ni pamoja ya maboresho ya miundombinu ya reli, ununuzi wa vichwa vya reli, mabehewa na vitendea kazi vingine.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali kwa haraka ishughulikie maboresho ya mkataba wa *TAZARA* na kisha kutafuta fedha ya masharti nafuu angalau kiasi cha shilingi bilioni 300. Katika kipindi hiki cha ushindani mkubwa na hata mfumuko wa bei wa mafuta ya petroli, mbolea na bidhaa mbalimbali, usafirishaji wa reli ni mojawapo ya suluhisho kubwa kupunguzo mzigo wa bei kubwa kwa wateja wa bandari zetu na hata wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maboresha ya reli ya *TAZARA*, napendekeza kuendelea na ujenzi wa bandari kavu Mbeya ambayo ina fursa kubwa katika kipindi hiki katika kuwezesha kupunguza gharama za kusafirisha kwa wateja wa bandari na hata kupunguza bei za mafuta ya petroli, pembejeo na mazao ya kilimo. Bandari kavu ya Mbeya ni njia panda kwa wateja wa nchi za Malawi, Zambia, DRC Lubumbashi na hata kwa Zimbabwe na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, reli ya *TAZARA* ambayo ni tegemeo kusafirisha mizigo kwa mikoa ya Pwani, Morogoro, mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini na pia mizigo ya nchi za nje ikiwemo, Zambia, Malawi, na DRC Congo, miundombinu inaendelea kuchakaa kutokana na kukosa matengenezo ya mara kwa mara. Serikali ichukue hatua za haraka kuinusuru reli ya *TAZARA* hata ikibidi kurekebisha mikataba ya umiliki na uongozi ili mradi iendeshwe kwa tija. Kuna kuchukua hatua za makusudi kwa kutumia zaidi *TAZARA* kusafirisha mizigo ambayo imeelemea hata uwezo wa barabara zetu. Usafirishaji wa mizigo kwa kutumia *TAZARA* ilenge kupunguza gharama za mafuta ya petroli, pembejeo kwa wakulima na wakati huo kupunguza gharama za kusafirisha mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuboresha *TAZARA*, napendekeza kukamilisha taratibu za ujenzi wa bandari kavu ya Mbeya ambapo Mamlaka ya Bandari kwa kipindi kirefu wamewahakikishia wananchi kulipa fidia ya eneo lao wanalolichukua.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kuvutia wawekezaji na kuongeza pato la fedha za kigeni, napendekeza Serikali kuchukua hatua kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa madini ya Niobium ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kiwanda cha Ferroniobium *(FeNb)* ambacho kitakuwa cha kwanza Afrika na cha nne duniani. Kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa reli, madaraja na reli ya *SGR,* kuna mahitaji

makubwa ya vifaa vya chuma ambavyo ni imara, lakini vyepesi na vyenye ubora wa kimataifa. Kwa kutumia sheria zetu za uwekezaji, Serikali itumie fursa za kipindi hiki ili kuvutia wawekezaji kwenye madini ya viwandani ili yaongezwe thamani hapa kwetu na pia kuvutia malighafi ya madini toka nchi zingine ili yachakatwe hapo kwetu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imebahatika kuwepo kwa madini ya Niobium ambayo yanapatikana milima ya *Panda Hill*, Songwe Wilaya ya Mbeya na mahitaji ya Ferroniobium *(FeNb end product)* ni makubwa duniani na hapa kwetu pia. Kwa kutumia rasilimali zetu za madini, Serikali inaweza kutengeneza fursa nyingi na kupitia Mradi wa Niobium na Kiwanda cha Ferroniobium, ajira 2,000 zitakazozalishwa wakati wa ujenzi na pia kutakuwepo ajira za kudumu zaidi ya 600 na *indirect jobs* 7,000. Mradi utazalisha mapato kila mwaka shilingi bilioni 500 *(US$ 220 million)* ambapo mapato kwa Serikali kila mwaka shilingi bilioni 50 *(US$ 22 million),* uhai wa mgodi ni zaidi ya miaka 30. Hiki kitakuwa kiwanda cha kisasa cha kwanza Afrika *(Modern Manufacturing Plant and Smelter)*. Pamoja na kuingiza teknolojia hii adimu na ujuzi *(skills transfer)* pia itakuwa itachangia huduma za kijamii *(Corporate Social Investment in Community)* na chanzo cha fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa maandalizi ya hotuba iliyojaa ufafanuzi wa sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha yafuatayo; kwanza kazi na ajira, kupitia kilimo tunaweza kupanua wigo wa ajira, lakini pia tunaweza kujitosheleza kwa baadhi ya bidhaa ambazo kutokana na kilimo tutazizalisha na tukapunguza matumizi ya fedha za kigeni katika kuagiza bidhaa kama mafuta ya kula. Ushauri wangu wa mara zote,

kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Wizara ya Ulinzi na JKT, tuwekeni nguvu kama Taifa katika kuzalisha mbegu ambazo tutazalisha mafuta ya kula.

Mheshimiwa Spika, napongeza jitihada za Mheshimiwa Waziri Mkuu zinazoendelea kule Kigoma za kilimo cha michikichi. Ninaamini tukiwawezesha JKT tutavuka, lazima tufike wakati tuwe na uthubutu, tuwe wakweli wa nafsi, sio sawa kama Taifa kuendelea kutumia zaidi ya *USD* milioni 300 kuagiza mafuta ya kula, tuone aibu kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, hata jitihada za kupunguza *VAT* kwa waagizaji mafuta ya kula hazijawa na nafuu iliyokusudiwa, zaidi imenufaisha wafanyabiashara waagizaji wa mafuta ya kula, matokeo yake bei ya alizeti imeshuka kwa wakulima wetu na wakati huo huo bei ya mafuta ya kula haina ahueni yoyote.

Mheshimiwa Spika, tukiwekeza katika JKT sio tu kwamba tutaokoa fedha za kigeni lakini pia tutauza mafuta katika nchi jirani za DRC, Malawi, Zambia na hata Burundi na Rwanda. Nchi hizi zinategemea mafuta ya kula kutoka Malaysia, tukizalisha tunalo soko la ndani, lakini pia soko hata ndani ya *EAC* na baadhi ya nchi za *SADC*.

Kule Chita, nashauri Serikali ikajifunze kilimo cha mpunga chini ya JKT, ni aibu sisi kutoa vibali na kuagiza michele tani 90,000; haya ni mambo tunapaswa kuyakataa kwa vitendo, hizi programu za *Block Farming* zingehusisha vijana waliopata mafunzo JKT na usimamizi ungefanywa kwa ushirikiano wa ofisi hizi tatu, Kilimo, Kazi na Ajira na JKT.

Mheshimiwa Spika, pili, usalama wa mbegu na mbegu bora; pia ninashauri tuwe na mpango maalum wa kuhakikisha Taifa linajitosheleza kwa mbegu bora na salama. Mfumo uliopo kwa hakika sio salama katika suala la usalama

wa chakula na usalama wa Taifa. Nashauri pia tuhusishe vyombo vyetu hasa JKT.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kupongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwasilisha vizuri hotuba yake nzuri na utendaji wake mzuri sana, ameonesha weledi mkubwa sana katika uongozi wake. Pia nawapongeza Mawaziri wote waliopo kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa wanazozifanya kuhakikisha nchi yetu inapiga hatua kimaendeleo. Nawapongeza pia Makatibu Wakuu wote kwa utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika suala zima la ajira kwa vijana. Nchi yetu kumekuwa na tatizo kubwa la ajira kwa vijana wetu, lakini pia kuna vijana ambao wapo katika ajira zisizokidhi haja na mfano vijana wanaofanya vibarua *TPA*, wanafanya vibarua kwa miaka 10 lakini ajira zinapotokea wanaletwa wengine na wale wanaofanya kazi ya kibarua wanaendelea kuwa vibarua. Mfumo wa kutumia wakala wa vibarua kama vile SUMA JKT unadumaza maendeleo ya upatikanaji wa ajira kwa sababu wanatoa ajira za kutwa na hakuna njia nyingine.

Naiomba sana Serikali iangalie upya utaratibu wa utoaji ajira kwani kuna vijana wengi wanajitolea bure kutoa huduma kwa zaidi ya miaka mitano, lakini ajira zinapotokea hawapewi kipaumbele. Hali hiyo sio nzuri inakatisha tamaa sana kwa vijana wetu. Vijana wanaojitolea wapewe kipaumbele. Niipongeze Serikali kwa kuja na utaratibu wa *intern* kwa vijana, ni jambo jema, lakini vijana wengi wako *intern* lakini tuhakikishe kuwa hao walio *intern* wanapata ajira za kudumu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kinipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya makadirio na mapato ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Pili napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna alivyoitayarisha hotuba yake kwa ufasaha na umakini mkubwa sana na kuiwasilisha hotuba hii katika Bunge lako tukufu kwa utulivu na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza ni uvuvi; napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Mama Samia kwa namna inavyochukua jitihada kubwa za kuendeleza uvuvi nchini. Uvuvi ni sekta muhimu sana inayowaletea maendeleo wavuvi wetu. Uvuvi pia ni muhimu sana katika kuongeza ajira za wananchi wetu. Lakini pamoja na juhudi zote hizo za Serikali bado kunahitajika hatua kadhaa ili kuimarisha uvuvi nchini. Bado wavuvi wetu wanafanya kazi hii kwa mazoea. Vifaa wanavyotumia ni vilevile vya zamani, hivyo naiomba Serikali kuwapatia wavuvi vifaa vya kisasa ili kuwa na uhakika na kazi yao. Aidha Serikali yetu iwapatie elimu ya kisasa ili kuwa na ubora wa kazi yao.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu kilimo; napenda kuchukua fursa hii kwa kuipongeza Serikali yetu kwa namna inavyojitahidi kuchukua hatua za makusudi ili kuendeleza kilimo nchini. Naiomba Serikali iendelee na juhudi hizi hasa za kuendeleza kilimo nchini kwa kuendelea kuwapatia pembejeo za kilimo ili wakulima wetu wapate kulima kwa wakati na kupata mazao mengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ttau ni kuhusu Muungano wa Tanzania; napenda kumponeza sana Rais wetu, Mheshimiwa

Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyochukua juhudi za makusudi za kuimarisha Muungano wetu. Hivi sasa wananchi wa sehemu mbili za Jamhuri ya Muungano wanashirikiana katika nyanja nyingi za maendeleo. Aidha, miradi na misaada inayopatikana sasa inaenda katika sehemu zote mbili za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri Mkuu Mheshiliwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa hotuba nzuri kutoka katika ofisi yake. Pia niwapongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako pamoja na Naibu Mawaziri wao. Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wake hawa wanaupiga mwingi.

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu utajikita kwenye Kiwanda cha *Tanzania Biotech Products Limited (TBPL)* cha Kibaha mkoani Pwani kilicho chini ya Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)*. Kiwanda hiki kimeshaanza uzalishaji wa viuatilifu vya kuangamiza mbu na wadudu wa mazao na vilevile kina uwezo wa kuzalisha mbolea.

Mheshimwa Spika, bidhaa za kiwanda hiki ni za kibaiolojia. Kiwanda hiki kimejengwa kutokana na mahusiano mazuri ya kidiplomasia baina ya Tanzania na Cuba. Ni kiwanda bora na cha mfano Barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, kiwanda hiki cha viuadudu kilianza uzalishaji rasmi mwaka 2017 ambapo uwezo wa uzalishaji wa kiwanda ni lita milioni sita kwa mwaka na kinatumia malighafi inayopatikana ndani ya nchi kwa asilimia 98. Pamoja na uwezo wa kiwanda hiki, pamekuwa na changamoto kubwa ya soko la bidhaa kutoka kiwandani, hali iliyopelekea

watumishi wa kiwanda kutokulipwa stahiki zao kutokana na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, lengo la ujenzi wa kiwanda hiki lilikuwa ni kuchangia kutokomeza malaria nchini na Afrika kwa ujumla kwa kuzalisha viuatilifu visivyo vya kemikali. Lengo la pili ni kuzalisha viuatilifu na mbolea zisizo na kemikali. Mbolea hizi zitaendeleza kilimo hai ambacho kina soko kubwa duniani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwepo wa kiwanda hiki bora na cha kisasa, pamekuwepo na matumizi mabaya ya rasilimali hii kutokana na ukosefu wa soko la bidhaa zinazozalishwa. Mpango wa awali ulizitaka Halmashauri zote nchini kununua bidhaa hizo ili kuangamiza mbu waenezao malaria kwa pamoja kama nchi. Cha kusikitisha ni kwamba Halmashauri nyingi nchini hazijashiriki kununua dawa katika kiwanda hiki.

Mheshimiwa Spika, utokomezaji wa malaria hapa nchini utafanikiwa tu ikiwa nchi yetu itaanzisha programu maalum ya kununua na kutumia dawa hizi kwa wakati mmoja katika maeneo yote hapa nchini Tanzania. Huko Zanzibar matumizi sahihi ya dawa kutoka katika kiwanda hiki kumepunguza ugonjwa wa malaria kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, hapa Tanzania kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wa watu wengi kwani asilimia kubwa ya wakazi hujishughulisha na shughuli za kilimo. Lakini kilimo hukabiliwa na changamoto kubwa ya wadudu wa mazao na uchakavu wa ardhi. Pamoja na changamoto hizi, Tanzania inakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa mbolea na viuatilifu na hata zile zilizopo kutokidhi mahitaji ya soko. Uwepo wa kiwanda hiki unaweza kuwa mkombozi wa wakulima wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa kiwanda hiki, ninaishauri Serikali kufanya yafuatayo; kwanza Wizara ya Afya ihusike kikamilifu na ichukue jukumu la hukakikisha kuwa dawa kutoka kiwandani zinanunuliwa na kusambazwa nchi nzima.

Pili, ikiwezekana, Bohari ya Madawa *(MSD)* ihusishwe kununua dawa ya viuadudu vya mazalia ya mbu kutoka Kiwanda cha Biotech kilichopo Kibaha ili kuzuia malaria badala ya ilivyozoeleka kupoteza mamilioni ya fedha kununua madawa kutoka nje kwa ajili ya kutibu ugonjwa wa malaria.

Mheshimiwa Spika tatu, kwa kuwa kiwanda hiki kinamilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC),* ninashauri Serikali itenge fedha na kuwalipa wafanyakazi wanaodai stahiki zao.

Nne, Serikali ijikite kikamilifu kwenye uzalishaji wa mbolea na viuatilifu hai ili vitumike kikamilifu kwenye sekta ya kilimo kwani kuna changamoto kubwa nchini ya bidhaa hizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na uzima.

Pili, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuliongoza vizuri sana Taifa letu. Aidha, nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na wasaidizi wako wote kwa kuendesha vikao vya Bunge kwa umakini na umahiri kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa wasilisho zuri na

hotuba yenye kuleta matumaini kwa ustawi mzuri wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, naomba kuchangia sehemu mbili tu nazo ni ushirikiano kwa Taasisi za SMZ na Taasisi za SMT.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu ni kiungo muhimu sana katika kutatua changamoto mbalimbali za Tanzania Bara na Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Nazipongeza ofisi hizi kwa kazi nzuri wanazozifanya, lakini bado kuna haja kuendeleza ushirikiano kwa taasisi za zetu ambazo sio za Muungano Kikatiba. Mfano Afya, Maji, Uwekezaji, Utalii na kadhalika, kwani ushirikiano huo kasi yake ikiongezeka basi itakuwa na mafanikio kwa SMZ na SMT na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pili ni masuala ya mazima ya kupambana na masuala ya udhalilishaji na ukiukwaji wa maadili. Matendo ya kujamiiana ya jinsia moja au ndoa za jinsia moja sambamba na uharibifu wa vizazi vyetu kwa maana watoto wetu. Jambo hili ni hatarishi sana kwa ustawi mzuri wa Taifa letu. Hivyo naiomba Serikali na Watanzania kwa ujumla kukemea na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria zetu na Katiba yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia, ahsante sana.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, utangulizi; na kabla sijaanza kuchangia, niwaombe Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Spika tusikubali Bunge hili tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutumika kama sehemu ya kusafisha wahalifu na wabadhirifu wa mali za umma kwani la kuvunda halina ubani. Na hapa nichukue nafasi hii, kuzipongeza sana Mamlaka za Ukaguzi na Uchunguzi kwa kazi nzuri walizofanya katika hesabu zinazoishia mwaka

2021/2022 kwa kuibua wizi, ubadhirifu na ufisadi pamoja na matumizi mabaya ya madaraka katika taasisi mbalimbali za Serikali nchini.

Mheshimiwa Spika, hongera sana kwa CAG, CPA – Charles Kichere na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, CP – Salum Hamduni, hongereni pamoja na maafisa wote wa Ofisi zenu. Uchunguzi na ukaguzi mlioufanya ni kielelezo kikubwa cha uzalendo mlionao kwa Taifa letu, Mungu awabariki sana; na kipekee nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukataa kata kata nchi yetu kugeuzwa shamba la bibi. Na hapa naweka msisitizo Mawaziri na watendaji wote waliohusika wakamatwe na washtakiwe kwa makosa ya uhujumu uchumi.

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2023/2024, lakini pia nimesoma Mpango wa Maendeleo na ukomo wa bajeti ya mwaka 2023/2024 pamoja na taarifa ya CAG ya mwaka 2021/2022 ili kuona hatua za utekelezaji wa majukumu na changamoto za Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla. Baadhi ya masuala ya kiujumla ni kama ifuatavyo:-

(i) Bajeti ya maendeleo kushuka na kufikia 34.1% mwaka wa fedha 2023/2024 ni kinyume na Mpango wa Maendeleo III wa miaka mitano ambapo walau fedha za maendeleo zisipungue chini ya 37.1% ya bajeti nzima. Nini kimesababisha bajeti ya maendeleo kushuka?

(ii) Katiba Mpya, licha ya maelekezo ya muda mrefu ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu kuanza kwa mchakato wa marekebisho ya Katiba

na upatikanaji wa Katiba Mpya, hotuba ya Waziri Mkuu na mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2023/2024 hazijaeleza chochote kuhusu maandalizi ya suala hili muhimu. Waziri Mkuu aeleze hatua zilizofikiwa katika mchakato wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto mahsusi ya utekelezaji wa bajeti; mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2023/2024, ukurasa wa 89 kipengele cha 2:4:2 Serikali inakiri kuwepo kwa changamoto mahsusi zinazokwaza utekelezaji wa miradi nanukuu kama ifuatavyo:-

(a) Upungufu wa rasilimali watu hususan wahandisi wa kusimamia utekelezaji wa miradi pamoja na wataalamu wa uendeshaji wa mitambo na vifaa vinavyotumia teknolojia ya kisasa;

(b) Watekelezaji wa miradi kuchelewa kukamilisha taratibu za utoaji wa cheti cha msamaha wa kodi hali inayosababisha kuongezeka kwa gharama za mradi (madai ya riba) na kuchelewa kwa kutekeleza mradi;

(c) Usanifu duni wa mradi hali inayosababisha kuongezeka kwa mawanda, gharama na muda wa utekelezaji wa miradi;

(d) Usimamizi usioridhisha katika utekelezaji wa miradi kwa mujibu wa mikataba na mipango kazi kwa baadhi ya watekelezaji wa miradi;

(e) Kuchelewa kwa malipo ya makandarasi kunakosababishwa na kutowasilishwa kwa nyaraka muhimu za kuwezesha kufanyika kwa malipo kwa

wakati hali inayosababisha malimbikizo ya riba na ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi;

(f) Usimamizi na uratibu kwa baadhi ya taasisi kufanyika katika ngazi ya makao makuu bila kushirikisha wasimamizi waliopo katika eneo la mradi hali inayosababisha miradi kuchelewa, kuongeza gharama na kupunguza ufanisi katika malengo ya mradi;

(g) Ushirikishwaji mdogo wa wadau muhimu wa mradi katika kipindi cha maandalizi hali inayosababisha kubadilika kwa mawanda ya kazi wakati wa utekelezaji; na

(h) Kuchelewa kwa malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha miradi.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu wewe ndio msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali na haya yote yanatokea chini ya usimamizi wako, nini kilichoifanya Serikali ishindwe kuchukua hatua stahiki na kuondoa dosari hizo? Kama Wabunge tulitegemea Serikali ingekuwa imetatua changamoto hizo badala ya kulalamika kwa wananchi huku Taifa likiendelea kupata hasara kubwa.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa bajeti na fedha za umma; leo tunajadili hotuba ya bajeti ya mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2023/2024 kukiwa na wizi, rushwa, ubadhirifu na ufisadi wa fedha na rasilimali za umma umetamalaki kila sehemu, fedha nyingi zinazoidhinishwa na Bunge zinaishia mikononi mwa wezi wachache ndani ya Serikali kutokana na mikataba mibovu, usimamizi dhaifu wa mikataba, malipo

yasiyo na tija, matumizi na mikopo nje ya bajeti, manunuzi yasiyozingatia sheria, kuongeza bei katika hati za malipo *(over invoicing),* kutokutekeleza mipango ya manunuzi kama ilivyoidhinishwa na Bunge na kukosekana uwajibikaji Serikalini.

Mheshimiwa Spika, leo ni siku mbaya ambayo tunakwenda kuidhinisha fedha za umma zikagawanwe tena na wachache. Katika kufanya hivyo ni muhimu sana kupitia na kufanya tahmini ya kina juu ya vihatarishi vitakavyopelekea bajeti hii kutotekelezwa ipasavyo, ipo mifano michache kupitia taarifa za utekelezaji na Ripoti ya *CAG* inayoonesha kuwa kuna vihatarishi vikubwa vinavyoweza kufanya bajeti hii isitekelezeke kwa tija kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kushindwa kutekeleza mpango wa manunuzi; mapitio ya utekelezaji wa mpango wa manunuzi mwaka 2021/2022 imeonesha taasisi 22 zilishindwa kutekeleza mpango wa manunuzi wenye thamani ya kiasi cha shilingi trilioni 3.14 kati ya fedha hizo *TANROADS* ni shilingi trilioni 2.9 ambazo taasisi hiyo ilishindwa kukamilisha mchakato wa manunuzi kutokana na kuchelewa kupata kibali cha kutangaza zabuni za miradi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi *(CAG)*.

Mheshimiwa Spika, Bunge liliidhinisha fedha hizi katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya kwenda kutekeleza miradi mbalimbali kwa maslahi ya Taifa na badala yake fedha hizo hazikutumika na hazijulikani zilipo. Katika mwaka huo wa fedha mapato ya Serikali yalipatikana kwa 97.2% na mikopo ilipatikana kwa 106%; iweje zabuni zisitolewe kwa mwaka mzima, wananchi wanaendelea kuteseka kwa kukosa huduma muhimu ikiwemo barabara, Wabunge wanalia Bungeni, wengine wanapiga magoti Bungeni, wengine wanapiga sarakasi Bungeni kutokana na kukosa fedha za kugharamia miradi ya majimbo yao.

Mheshimiwa Spika, ushauri; *CAG* na TAKUKURU wafanye uchunguzi na ukaguzi maalum ili kujua sababu zilizopelekea Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, *TANROADS* na taasisi zingine kukaa na fedha mwaka mzima bila matumizi na pia kujua fedha hizo ziko wapi.

Mheshimiwa Spika, hatua kali za kiutawala na za kisheria zichukuliwe ikiwemo kushtakiwa kwa makosa ya uhujumu uchumi wa nchi kwa wote waliohusika kwa uzembe na ufisadi huu.

Mheshimiwa Spika, kutokufuata Sheria ya Manunuzi wakati wa kutoa zabuni ya Mradi wa *SGR,* kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* ya mwaka 2021/2022 inaonesha kuwa gharama ya ujenzi wa *SGR Lot. No. 3* na *Lot No. 4* ziliongezeka dola za Marekani milioni 1.3 na milioni 1.6 kwa kilometa moja ya *SGR* baada ya *TRC* kuacha njia ya ushindani na kutumia njia ya *single source* na kusababisha hasara ya jumala ya shilingi trilioni 1.7 kwa mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, *Lot No. 3* Mkataba wa *TRC* na Kampuni ya Yapi Markenz wa ujenzi wa *SGR* kipande cha Makutupora – Tabora urefu wa kilometa 368 uliosainiwa Disemba 2021 ambapo *TRC* iliacha bei ya ushindani ya kiasi cha shilingi bilioni 9 kwa kilometa ya *SGR* na kutoa zabuni kwa njia ya *single source* kwa Kampuni ya Yapi Markenz kwa shilingi bilioni 11.97 kwa kilometa ya *SGR* ambao kumeisababishia Serikali hasara ya zaidi ya shilingi trilioni 1.09.

Mheshimiwa Spika, *Lot No. 4* Mkataba wa *TRC* na Kampuni ya Yapi Markenz wa ujenzi wa *SGR* kipande cha Tabora – Isaka urefu wa kilometa 165 uliosainiwa Julai, 2022 ambapo *TRC* iliacha bei ya ushindani ya kiasi cha shilingi bilioni tisa kwa kilometa ya *SGR* na kutoa zabuni kwa njia ya *single source* kwa Kampuni ya Yapi Markenz kwa shilingi

bilioni 12.69 kwa kilometa ya *SGR* ambao kumeisababishia Serikali hasara ya zaidi ya shilingi bilioni 608.8.

Mheshimiwa Spika, licha ya *PPRA* na Bodi ya Zabuni ya *TRC* kukataa sharti la kutumia mzabuni mmoja, lakini *TRC* ilitoa zabuni hiyo kwa njia ya *single source* kwa Kampuni ya Yapi Markenz. Maamuzi haya yalitokana na maelekezo ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa barua yenye Kumb. Na. PST/GEN/2021/01/55. Ili kukidhi matakwa ya kupata mkopo kutoka Benki ya *Standard Charted* na kusababisha hasara kwa Serikali ya shilingi trilioni 1.7.

Mheshimiwa Spika, *TRC* ilimkataa mzabuni wa shilingi bilioni 616.4 na kumpa mzabuni wa shilingi trilioni 1.119 kwa ajili ya ununuzi wa vichwa vya treni vya umeme na makochi bila sababu za msingi na kuisababishia Serikali hasara ya shilingi bilioni 503 hii ni kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* ya mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, dosari alizoziona *CAG* katika *Lot No. 3* na *Lot No. 4* zipo pia katika *Lot No. 6,* Mkataba wa *TRC* na Kampuni ya *China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC)* wa ujenzi wa *SGR* kipande cha Tabora – Kigoma yenye urefu wa kilometa 506 ambapo *TRC* iliacha bei ya ushindani ya kiasi cha shilingi bilioni 9.1 kwa kilometa ya *SGR* na kutoa zabuni kwa njia ya *single source* kwa Kampuni ya *CCECC* kwa shilingi bilioni 12.5 kwa kilometa ya *SGR* hii ni zaidi ya bilioni 3.4 kwa kilometa ya *SGR* katika mkataba uliosainiwa mwaka 2022, gharama hiyo imeongezeka wakati idadi ya vifaa na ukubwa wa miundombinu umepunguzwa na kuisababishia Serikali hasara ya zaidi ya trilioni 1.7.

Mheshimiwa Spika, malipo ya ununuzi wa vichwa vya treni na makochi na ujenzi wa *SGR Lot. No. 3, Lot. No. 4* na *Lot No. 6* ambapo *TRC* iliacha bei ya ushindani na kutumia njia ya *single source* na kusababisha upotevu wa fedha kiasi cha takribani shilingi trilioni 4 huku sheria na kanuni za manunuzi ya

umma zikiwa zimevunjwa. Ufisadi huu wa fedha za umma umepata baraka zote za Waziri wa Fedha, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na *TRC* na bahati mbaya bado wako kwenye Ofisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kama Mbunge hapa Bungeni nilihoji Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi sababu za kukiuka sheria ya manunuzi na kutoa zabuni bila ushindani na kuisababishia hasara Serikali, lakini Wizara haikuweza kutoa majibu yanayojitosheleza *(Hansard* za Bunge zipo). Leo *CAG* ameweka wazi suala hili pamoja na *PPRA* na Bodi ya Zabuni ya *TRC* kutoa ushauri wa zabuni kutolewa kwa mujibu wa sheria, lakini Waziri wa Fedha na Mipango na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi waliridhia zabuni hizo kutolewa kinyume cha sheria ya manunuzi ya umma Na. 7 mwaka 2011 na marekebisho yake ya mwaka 2016 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016 kwa sababu wanazozijua wao na kuliingizia Taifa hasara ya takribani shilingi trilioni 4. Huu ni uhujumu uchumi wa nchi kwa mujibu wa Sheria ya Uhujumu Uchumi *(The Economic and Organized Crime and Control Act)*.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka pia kuwa baada ya kuchangia suala hili hapa Bungeni mara kwa mara na kukosa majibu fasaha kuhusu ukiukwaji mkubwa wa sheria, niliamua kumuandikia barua Katibu Mkuu Kiongozi yenye Kumb. Na. MB/KSS2023/21 ya tarehe 13 Machi, 2023 ambapo na wewe nilikupa nakala nikionesha ukiukwaji mkubwa wa sheria na hasara kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, hivyo badala ya kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya mradi huu hatua za haraka zifuatazo zichukuliwe:-

Mheshimiwa Spika, kwanza; hatua kali za kiutawala na kisheria zichuliwe ikiwemo kukamatwa na kufunguliwa makosa ya uhujumu uchumi wa nchi kwa Waziri wa Fedha na

Mipango, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mkurugenzi Mkuu wa *TRC* na wengine wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, pili; kuvunja mikataba au kufanya makubaliano mapya kwa mikataba ya *Lot 3, Lot 4* na *Lot 6* ili kuondoa dosari zote zinazosababisha Serikali hasara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi na mikopo nje ya bajeti; kama Mbunge nimeuliza mara kwa mara hapa Bungeni Serikali kukopa nje ya bajeti, lakini Waziri wa Fedha alishindwa kutoa majibu ya kina kueleza imekopa kiasi gani nje ya bajeti, amekopa mikopo ya ziada kwa shughuli gani na sababu za kulikwepa Bunge ni zipi *(Hansard* ya Bunge inajieleza). Leo *CAG* ameweka wazi ukweli uliokuwa unafichwa. Kama fedha hizi zilikopwa kwa nia njema na kwa maslahi ya Taifa kwa nini zipokelewe na kutumika kwa siri? Huku ni kupoka madaraka ya Bunge na kuna harufu ya ufisadi wa kutisha.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* 2021/2022 Serikali Kuu jedwali na 17 linaonesha kuwa Serikali imekopa nje ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na bila ridhaa ya Bunge kiasi cha shilingi trilioni 1.285. Waziri wa Fedha alikopa fedha hizi kwa ajili ya shughuli gani na kwa ridhaa ya nani? Fedha na kazi zilizopangwa katika bajeti 2021/2022 zilipitishwa na kuidhinishwa na Bunge tena kwa kupigiwa kura ya ndiyo, fedha za ziada alizokopa Waziri wa Fedha ni kwa ajili ya shughuli gani na kwa ridhaa ya nani?

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo *(Government Loans, Guarantees and Grants Act)* ambapo mamlaka ya kukopa mikopo amepewa Waziri wa Fedha kwa niaba ya Serikali na atafanya hivyo kwa kuzingatia ukomo uliowekwa na Bunge kupitia bajeti iliyoidhinishwa na endapo katika utekelezaji wa bajeti kutakuwa na mahitaji mapya atapata kibali cha Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 ilipotokea ongezeko la mikopo la shilingi trilioni 1.31 kutoka *IMF* kwa ajili ya kutekeleza mpango wa kukabiliana na hali ya uchumi baada ya kupungua kwa ugonjwa wa *Covid-19* bajeti ilifanyiwa marekebisho kupitia Bunge kutoka trilioni 36.68 hadi trilioni 37.99. Hapa Waziri wa Fedha alizingatia matakwa ya sheria ya mikopo inavyotaka ambapo Bunge liliridhia kwa kauli moja na hakukuwepo malalamiko.

Mheshimiwa Spika, swali kubwa wanalojiuliza Watanzania kwa nini ongezeko la mikopo ya ziada la kiasi cha shilingi trilioni 1.285 aliyokopa Waziri wa Fedha haikuwekwa wazi na hakupata ridhaa ya Bunge? Fedha hizi Bunge ni vigumu kuzisimamia kwani halijui ziko wapi na kwa matumizi gani hali inayoweza kusababisha matumizi mabaya na ufisadi. Maamuzi ya Waziri wa Fedha yamekwenda kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria ya Bajeti, Sheria ya Fedha na Sheria ya Mikopo lakini pia ni matumizi mabaya ya Ofisi kwenye Sheria ya Kanuni ya Adhabu.

Mheshimiwa Spika, ushauri; *CAG* na TAKUKURU wafanye uchunguzi na ukaguzi maalum ili kubaini sababu zilizomsukuma Waziri wa Fedha kukopa na kutumia fedha za mikopo nje ya bajeti iliyopitishwa na Bunge pamoja na uhalali wa matumizi yaliyofanywa.

Mheshimiwa Spika, hatua kali za kiutawala na kisheria zichukuliwe kwa Waziri wa Fedha na wahusika wengine wote ikiwemo kushtakiwa kwa makosa ya uhujumu uchumi wa nchi ambao umepelekea kuliingiza Taifa kwenye hasara na mzigo mkubwa wa madeni.

Mheshimiwa Spika, kushindwa kusimamia mikataba kikamilifu *(JHNPP – 2115);* kama Mbunge nilihoji mara kwa mara suala hili hapa Bungeni kuhusu Kampuni ya *Arab Contractors* kutakiwa kulipa faini ya ucheleweshaji na *CSR*

lakini Waziri wa Nishati muda wote amekuwa mtetezi wa mkandarasi *Arab Contractors* na kumkingia kifua asilipe malipo hayo halali kwa mujibu wa mkataba *(Hansard* za Bunge zipo).

Mheshimiwa Spika, *CAG* ameuweka wazi ukweli wa jambo hili kuwa *TANESCO* wameshindwa kutoza faini ya fidia ya ucheleweshaji kwa mwaka kiasi cha shilingi bilioni 327.93 sawa na kiasi cha shilingi bilioni 655.86 kwa miaka miwili. Pia wameshindwa kutoza *CSR* ya kiasi cha shilingi bilioni 270.67 kwa mujibu wa mkataba wa mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere *(JNHPP – 2115)* na kusababishia jumla ya upotevu wa fedha kiasi cha shilingi bilioni 926.53.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Waziri wa Nishati amekuwa akitumia nguvu nyingi kiasi hicho kumkwepesha mkandarasi kulipa faini iliyowekwa kwa mujibu wa mkataba? Mkataba unakaribia kufika mwisho na fedha anazodai Kampuni ya *Arab Contractors* zimepungua, je, ni wakati gani Serikali itaanza kukata madai hayo? Huu ni uhujumu uchumi lakini pia ni matumizi mabaya ya ofisi ya umma kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni ya Adhabu.

Mheshimiwa Spika, ushauri; hatua kali za kiutawala na za kisheria zichukuliwe ikiwemo kukamatwa na kushtakiwa kwa makosa ya uhujumu uchumi wa nchi kwa Waziri wa Nishati, Mkurugenzi wa *TANESCO* na wahusika wengine kwa kuisababishia Serikali hasara ya shilingi bilioni 926.53.

Mheshimiwa Spika, Serikali ianze kukata malipo ya faini ya fidia ya ucheleweshaji na mchango wa *CSR* kwa kila hati ya malipo inayowasilishwa na kulipwa na kuhakikisha kuwa fedha zote za umma zinazodaiwa zimelipwa kabla ya mkataba kumalizika.

Mheshimiwa Spika, suala la *TANESCO* kushindwa kuidai *IPTL;* kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* ya mwaka 2021/2022,

*TANESCO* kushindwa kudai malipo ya shilingi bilioni 342 kutoka Kampuni ya *IPTL* baada ya Serikali kushinda kesi Machi, 2021 fedha hizi zinatakiwa kupatikana ili kulipa deni Benki ya Standard Chartered, Hong Kong dola za Marekani milioni 148.4 pamoja na riba kama ilivyoamuriwa na Kituo cha Kimataifa cha Kutatua Migogoro ya Uwekezaji. Kitendo cha kushindwa kukusanya fedha hizi kutafanya Serikali ilipe mkopo pamoja na riba kwa Benki ya *Standard Chartered* Hong Kong. Nini kilichofanya Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha na *TANESCO* washindwe kudai *IPTL* madai hayo halali kwa amri ya Mahakama?

Mheshimiwa Spika, *CAG* hakuona hatua yoyote iliyochukuliwa na Wizara ya Nishati na *TANESCO* tangu hukumu hiyo itolewe Machi, 2021 na hivyo kuleta sintofahamu kubwa lakini ilikuwa rahisi kwa Wizara kulipa malipo ya kiasi cha shilingi bilioni 350 katika Kampuni ya *Symbion Power LCC*.

Mheshimiwa Spika, ushauri; hatua kali za kiutawala na za kisheria zichukuliwe ikiwemo kukamatwa na kushtakiwa kwa makosa ya uhujumu uchumi wa nchi kwa Waziri wa Nishati, Mkurugenzi wa *TANESCO* na wote waliohusika na kuisababishia Serikali hasara ya shilingi bilioni 342.

Mheshimiwa Spika, Serikali iitake *IPTL* kwa haraka kulipa fedha kiasi cha dola za Marekani milioni 148.4 pamoja na riba kama Mahakama ilivyoamuru.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo ya tozo za riba bila sababu za msingi; malipo ya tozo na riba kutokana na kuchelewesha malipo ya wazabuni, wakandarasi, bima na mifuko ya jamii katika Serikali Kuu, mashirika ya umma na Serikali za Mitaa na kuipelekea Serikali hasara ya kiasi cha shilingi bilioni 418.5. ucheleweshaji huu ni kinyume cha sheria na pengine unafanywa kwa maslahi binafsi na Wizara ya Fedha na taasisi zingine za Serikali. Fedha hizi zingeweza

kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo badala ya kulipa faini. Wahusika wote wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya fedha za umma nje ya bajeti; taarifa ya *CAG* 2021/2022 inaonesha kuwa matumizi ya fedha za umma nje ya bajeti iliyoidhinishwa katika maeneo mbalimbali ya Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Serikali za Mitaa ambapo kwa ukokotoaji wangu ni kiasi cha shilingi bilioni 502.87 ambapo kati ya hizo shilingi bilioni 104.21 ni za *TANESCO* hii ni kinyume na sheria ya bajeti na sheria ya manunuzi; hatua zichukuliwe kwa wahusika.

Mheshimiwa Spika, fedha kupelekwa moja kwa moja *TARURA;* taarifa ya *CAG* ya mwaka 2021/2022 inaonesha Wizara ya Fedha kupeleka moja kwa moja *TARURA* fedha za ongezeko la tozo ya mafuta kiasi cha shilingi 100 kwa lita ya dizeli na petroli badala ya kupeleka kwenye Bodi ya Mfuko wa Barabara *(RFB)* kama sheria zinavyosema kiasi cha shilingi bilioni 330.33 huu ni ukiukwaji mkubwa wa sheria ya ushuru wa barabara na mafuta Sura ya 220. Sababu za kuikwepa Bodi ya Mfuko wa Barabara *(RFB)* hazifahamiki na pengine fedha hizi zimetumika vibaya.

Mheshimiwa Spika, ushauri; TAKUKURU ifanye uchunguzi ili kubaini sababu za Wizara ya Fedha kukiuka sheria na kama fedha hizo zimefika na kutumika kihalali *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, hatua za kiutawala na kisheria zichukuliwe kwa wahusika wote.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa maamuzi katika Mahakama za Rufani za Kodi; Mahakama za Rufani za Kodi za *TRAB, TRAT* na *CAT* kuchelewa kutoa uamuzi katika mashauri ya malimbikizo ya kodi hali inayopelekea kushindwa kukusanya mapato ya Serikali katika mwaka husika na kukosesha Serikali mapato. Mara nyingi *CAG* amekuwa akijibiwa sababu za ucheleweshaji ni upungufu wa rasilimali

fedha na watu. Hizi sababu sio za msingi kwani eneo nyeti kama hili kuacha kupewa kipaumbele na kutumika kama kichaka cha kukwepa kulipa kodi. Ripoti ya *CAG* ya mwaka 2021/2022 mashauri ya malimbilikizo ya kodi yamefikia kiasi cha shilingi trilioni 4.84.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa maamuzi unaonekana kwenye malimbikizo ya kodi pekee, lakini upande wa mashauri ya kesi za manunuzi chini ya Mamlaka ya Rufani za Manunuzi ya Umma *(Public Procurement Appeals Authority – PPAA)* maamuzi yamekuwa yakifanyika kwa wakati na kusifiwa na wadau.

Mheshimiwa Spika, ushauri; Bunge liunde Kamati Teule kuchunguza chanzo cha ucheleweshaji huo na kupendekeza hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Spika, malimbikizo ya kodi yasiyo na kesi Mahakamani; taarifa ya *CAG* ya mwaka wa fedha 2020/2021 ilionesha *TRA* kushindwa kukusanya malimbikizo ya kodi yasiyo na kesi mahakamani kiasi cha shilingi trilioni 7.54 bila sababu za msingi, kitendo cha *TRA* kushindwa kukusanya kodi hizi kwa wakati kuikosesha Serikali mapato ambapo *CAG* alilalamikia kasi ndogo ya ukusanyaji wa malimbikizo hayo ambayo ilikuwa ni 10% tu. Taarifa ya *CAG* ya mwaka 2021/2022 haijatoa taarifa ya hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa malimbikizo hayo lakini pia haijaeleza malimbikizo ya kodi ya mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, eneo hili la malimbikizo ya kodi lisipotazamwa upya na kubaini sababu zinazosababisha *TRA* ishindwe kukusanya mapato ambayo imeshayafanyia *assessment* na hakuna pingamizi yoyote itapelekea taasisi hii kuendelea kupoteza uwezo wa kukusanya mapato na eneo hili kutumika kama uchochoro na kichaka cha kukwepa kodi na kuikosesha mapato Serikali.

Mheshimiwa Spika, *CAG* aweke wazi malimbikizo ya kodi yasiyo na kesi mahakamani yaliyopo kufikia mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, ushauri; Bunge liunde Kamati Teule kuchunguza chanzo cha ucheleweshaji huo na kupendekeza hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Spika, kufuta madai ya malimbikizo ya kodi; taarifa ya *CAG* ya mwaka 2020/2021 inaonesha miongoni mwa kesi za rufani zilizoisha ni kesi 45 zenye thamani ya shilingi 5,594,675,387,242.40 ambazo zipo katika mazungumzo kati ya Serikali na kampuni ya madini ambayo ni *North Mara Gold Mine, Pangea Minerals Limitied, Bulyanhulu Gold Mine* na *ABG Exploration,* kati ya jumla ya deni la shilingi trilioni 343.5. kesi hii imetolewa kutoka Mahakama za Rufani za kikodi na kurejeshwa kusikilizwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*.

Mheshimiwa Spika, kama Mbunge nimekuwa nikilihoji suala hili mara kwa mara hapa Bungeni kuitaka Serikali kueleza hatua iliyofikia ya kulipwa kiasi cha shilingi trilioni 5.595 za malimbikizo ya kodi kwa makampuni ya madini maarufu makinikia, lakini majibu ya Waziri wa Fedha yalikuwa tofauti na ripoti ya *CAG* ambapo alidai kuwa madai hayo hayapo na kwamba yalishafutwa na sherehe ya kufuta ilifanyika Ikulu. Ingawa kila nilipomuomba kutoa ushahidi kuhusu uamuzi wa kufutwa madai hayo hakufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya *CAG* ya mwaka 2021/2022 haijaonesha suala hili limehitimishwa vipi na Serikali, lakini pia malimbikizo ya kodi ya kiasi cha shilingi trilioni 5.595 ambazo zilikuwa kwenye mazungumzo na kiasi cha shilingi trilioni 343.5 ambazo zilirejeshwa *TRA* hazipo tena kwenye vitabu vya *TRA*. Nani aliyetoa maamuzi ya kufutwa madai halali ya kiasi cha shilingi trilioni 5.595 na kufutwa kwenye vitabu madai ya kiasi cha shilingi trilioni 360 bila ridhaa ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, ushauri; Bunge liunde Kamati Teule kuchunguza sababu za kufutwa madai halali ya malimbikizo ya kodi kiasi cha shilingi trilioni 5.595 na kuondolewa kwa madai ya shilingi trilioni 360 kwenye vitabu vya *TRA* na kama yamefutwa kwa mujibu wa sheria na kupendekeza hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mashirika ya Umma yaliyopata faida kupata hasara; Mashirika ya Umma 16 yamepata hasara ya shilingi bilioni 34.5 mwaka 2021/2022 wakati mashirika hayo yalipata faida ya shilingi bilioni 56.57 mwaka 2020/2021 na kupelekea jumla ya hasara shilingi bilioni 91.07 ikiwemo Kampuni ya Mawasiliano *(TTCL)* ambayo imepata hasara ya shilingi bilioni 15.56 mwaka 2021/2022 wakati mwaka 2020/2021 *TTCL* ilipata faida ya shilingi milioni 517. Hatua zichukuliwe kwa wahusika wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mashirika ya umma ambayo yameongeza hasara; mashirika na taasisi zingine za umma 45 *CAG* alipofanya ukaguzi wa utendaji wa fedha alibaini kuwa hasara katika mashirika hayo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 281.76 mwaka 2020/2021 hadi kufikia shilingi bilioni 416.37 mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 134.61 ikiwemo Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* ambao hasara yake imeongezeka kutoka shilingi bilioni 109.7 mwaka 2020/2021 hadi shilingi bilioni 204.65 mwaka 2021/2022. Hatua zichukuliwe kwa wahusika wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi yasiyostahili katika Mashirika ya Umma; *CAG* alibaini mashirika 21 ambayo yamefanya matumizi yasiyostahili ya jumla shilingi bilioni 77.75 ambayo yalitokana na malipo ya posho kwa watumishi wasiostahili, malipo yasiyokuwa na uthibitisho na vielelezo vya matumizi husika. Ikiwemo Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* ambayo ilitumia kiasi cha shilingi bilioni 65.33. Hatua kali zichukuliwe kwa wahusika.

Mheshimiwa Spika, *DPP* kushindwa kukusanya malipo ya ahadi ya washtakiwa chini ya makubaliano ya mikataba ya kukiri makosa *(plea bargain)* na hukumu za mahakama kiasi cha shilingi bilioni 179.61 bila sababu za msingi. Hatua zichukuliwe kwa wahusika na Serikali ikusanye fedha hizo haraka.

Mheshimiwa Spika, ubadhirifu wa fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; ubadhirifu na upotevu wa fedha za umma uliosababishwa ukiukwaji wa mikataba, matumizi mabaya ya fedha za umma, marejesho ya fedha ya mifuko ya kina mama, vijana na wenye ulemavu, ukiukwaji wa sheria ya manunuzi na upotevu wa mapato, katika Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa Ripoti ya *CAG* ya mwaka 2021/2022 inaonesha ukiukwaji mkubwa wa Sheria ya Fedha, Sheria ya Manunuzi na Sheria ya Bajeti ambako kumesababisha wizi, ubadhirifu, ufisadi na hasara ambapo kwa ukokotoaji wangu ni kiasi cha shilingi bilioni 637.55. Hatua zichukuliwe kwa wahusika wote.

Mheshimiwa Spika, haya yote yamefanyika Waziri Mkuu yupo, Waziri wa Fedha yupo, Mawaziri wa Wizara husika wapo, Mwanasheria Mkuu yupo, Mlipaji Mkuu wa Serikali, Makatibu Wakuu wapo, *PPRA* ipo na *PPAA* ipo hadi kufikia ubadhirifu na upotevu wa fedha za umma kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa mwezi Novemba, 2022 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitoa maazimio kuhusu taarifa ya *CAG* ya mwaka 2020/2021 kwa watu wote waliotajwa kuhusika na ubadhirifu wachukuliwe hatua, lakini hadi sasa hakuna utekelezaji uliofanyika kuarifiwa Bunge hili.

**[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**Jedwali la Ubadhirifu na Upotevu wa Fedha za Umma**

| NA. | MAELEZO | KIASI (TSH. – BILIONI) |
|---|---|---|
| 1. | Kushindwa kutekeleza Mpango wa Manunuzi katika mwaka wa fedha na fedha hizo hazijulikani zilipo | 3,140 |
| 2. | Kutokufuata sheria ya manunuzi wakati wa kutoa zabuni ya miradi ya *SGR* kwa kuacha bei ya ushindani na kutumia *single source* na kuisababishia Serikali hasara | 3,903 |
| 3. | Matumizi ya mikopo nje ya bajeti bila ridhaa ya Bunge ambapo fedha hizo hazijulikani zilipo na matumizi yake hayafahamiki | 1,285 |
| 4. | Kushindwa kusimamia mkataba kikamilifu Bwawa la Julius Nyerere *(JHNPP – 2115)* kutokana na faini ya ucheleweshaji na *CSR* na kuisababishia Serikali hasara | 926.53 |
| 5. | *TANESCO* kushindwa kuidai *IPTL* madai halali baada ya Serikali kushinda kesi mahakamani tangu Machi, 2021bila sababu za msingi | 342 |
| 6. | Malipo ya tozo za riba ya ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi, wazabuni, bima na mifuko ya hifadhi ya jamai bila sababu za msingi | 418.5 |
| 7. | Matumizi ya fedha za umma nje ya bajeti na bila ridhaa ya Bodi, Madiwani na Bunge | 502.87 |
| 8. | Fedha kupelekwa moja kwa moja *TARURA* badala ya Mfuko wa Barabara *(RFB)* kinyume cha sheria | 330.33 |

| | | |
|---|---|---|
| | na matumizi yake kutofahamika | |
| 9. | Ucheleweshaji wa maamuzi katika Mahakama za Rufani za Kodi za *TRAB, TRAT* na *CAT* na kupelekea Serikali kukosa mapato | 4,840 |
| 10. | *TRA* kushindwa kukusanya malimbikizo ya kodi yasiyo na kesi Mahakamani bila sababu za msingi | 7,540 |
| 11. | Wizara ya Fedha na *TRA* kufuta madai halali ya malimbikizo ya kodi bila sababu za msingi na bila ridhaa ya Bunge | 5,595 |
| 12. | Mashirika ya Umma 16 yaliyopata faida mwaka wa fedha 2020/2021 lakini yamepata hasara mwaka 2021/2022 na kuisababishia Serikali hasara | 91.07 |
| 13. | Mashirika ya Umma 45 ambayo yameongeza hasara mwaka 2021/2022 | 134.61 |
| 14. | Ubadhirifu wa fedha za umma katika mamlaka za Serikali za Mitaa | 637.55 |
| 15. | Matumizi mabaya ya fedha za UVIKO-19 | 212 |
| 16. | Mashirika ya Umma yenye matumizi yasiyostahili | 77.75 |
| 17. | *DPP* kushindwa kukusanya malipo ya ahadi ya washtakiwa chini ya makubaliano ya mikataba ya kukiri makosa *(plea bargain)* na hukumu za Mahakama bila sababu za msingi | 170.61 |
| | **JUMLA KUU** | **30,146.82** |

Mheshimiwa Spika, hatua za dharura na za haraka zichukuliwe ili kulinusuru Taifa kupata hasara kubwa na kudidimia kiuchumi na kushindwa kutoa huduma kwa wananchi wake kikamilifu kutokana na ufisadi unaofanywa na baadhi ya Mawaziri na watendaji wengine wa Serikali. Nikipongeze sana chama changu, Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa msimamo thabiti wa kupiga vita wizi, rushwa, ubadhirifu na ufisadi wa fedha na mali za umma.

Mheshimiwa Spika, kipekee pia nipongeze sana maamuzi ya Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi katika kikao chake cha tarehe 1 Aprili, 2023 chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuazimia na kutoa maelekezo ya kuwafuatilia watu wote wanaotumia dhamana za uongozi vibaya na kushindwa kuweka maslahi ya nchi na uzalendo mbele katika nafasi walizoaminiwa kutumikia watu, badala yake wanaweka maslahi binafsi.

Mheshimiwa Spika, aidha Kamati Kuu imeielekeza Serikali kuchukua hatua thabiti kwa wahusika waliobainika kuhusika katika ukiukaji wa sheria na kusababisha ubadhirifu wa mali na rasilimali za nchi. Agizo la Kamati Kuu litekelezwe kikamilifu.

Nawasilisha, Kazi iendelee.

**SPIKA:** Kabla hajaanza kuchangia Mheshimiwa Mary Masanja kuna tangazo hapa. Tunao wageni ambao wameingia majira haya na hawa ni wanafunzi 170 kutoka Chuo cha Uhasibu *TIA* cha Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana Bungeni *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimemuita Mheshimiwa Mary Masanja lakini sasa kwa sababu uchangiaji wa sasa naanza kwa upande wa Serikali, kwa kweli nadhani ni muhimu kutambua leo kwamba mapacha wawili chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu leo wamependeza sana hebu wasimame kidogo. Leo wamependeza sana, hongereni sana na mdogo

wao nae mnaona tai aliyopiga leo mambo mazito, tai inaendana na suti kabisa hongereni sana *(Makofi/Makofi)*

Mheshimiwa Mary Masanja atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameendelea kutupa maelekezo lakini kutekeleza shughuli mbalimbali za Serikali ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo kwa kusema ukweli tumeiona jinsi ambavyo inaenda kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuongelea suala la Maliasili Mheshimiwa Rais amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba Maliasili tunazilinda, tunazitunza pia tunaendeleza masuala mazima ya utalii. Kwenye upande wa sekta ya Maliasili na Utalii tumekuwa na changamoto nyingi sana hususani za Wanyama wakali na waharibifu na hili limeweza kujitokeza hata kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambapo tuna maeneo mengi yenye changamoto za Wanyama wakali na waharibifu pia kumekuwepo na vyakula mazao yanaliwa na wanyama wakali na kwa bahati mbaya kabisa inapelekea mpaka vifo vinatokea.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inajitahidi sana kupunguza athari hizi ikiwemo kuanzisha vituo mbalimbali vya kudhibiti wanyama wakali na waharibifu, hili tunaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu mwaka wa fedha ulioisha aliweza kutoa fedha na tumeweza kujenga

vituo takribani 16 tukavielekeza katika maeneo hususani yenye changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo mwaka huu wa fedha tunatarajia pia kujenga vituo 13 na tutaelekeza hukohuko kwenye maeneo ambayo yana changamoto hizi. Niwaombe wananchi kwamba tumeanzisha pia programu ya kufundisha vijana ambao tunawaita *VJS* walioko kwenye maeneo yetu hayahaya tunayoishi, lengo ni kuhakikisha kwamba jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi zitambue namna ya kujikinga na wanyama wakali na waharifu. Tayari tumeshaanza na kila kituo, vile vituo ambavyo tumeshavijenga tayari tumepeleka vijana wanne wanne kila kituo ambao wanatoka katika maeneo husika. Hii inasaidia kwa sababu tumeanzisha utoaji wa ajira katika maeneo hayo lengo ni kudhibiti hao wanyama wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kutoa ahadi kwa wananchi na Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali ipo na inaendelea kulifanyia kazi suala hili kwa nguvu zote na Mheshimiwa Rais analiangalia kwa ukaribu sana, hata mtakumbuka mwaka jana alifanya ziara katika Mkoa wa Simiyu, ahadi yake ilikuwa ni kuajiri askari takribani 600. Tayari tumeshaanza kupata vibali vya kuajiri.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyoongea kuna Askari 271 tayari tumeshapokea vibali vyao ambao watasambazwa katika maeneo yenye changamoto. Kwa hiyo, ninaendelea kuwatoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba changamoto hii tunaendelea kuiangalia kwa karibu sana na tunaendelea kufikisha huduma kwa wananchi ili tuweze kuokoa maisha ya Watanzania pia na mazao ambayo yameendelea kupata kadhia hii.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba ardhi haitoshi na mahitaji ya ardhi ni makubwa, kila mtu anatamani sana kuongezewa maeneo. Tutakumbuka kwamba Mheshimiwa

Rais aliruhusu kusamehe vijiji takribani 920 na baadhi ya vijiji hivyo vingi vilikuwa vimesajiliwa ndani ya hifadhi. Tunaposema tunaachia hivi vijiji kwa upande mwingine tunakaribisha changamoto ya wanyama wakali na waharibifu. Niendelee kuwaomba wananchi pale ambapo Kijiji kiliachiwa kikasajiliwa ndani ya hifadhi lakini tunakutana na changamoto hizi, basi tushirikiane pamoja kudhibiti hawa wanyama wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, kile tunachotaka sekta ya maliasili na utalii ni kuangalia maeneo mahsusi ambayo ni shoroba za wanyama wakali na waharibifu ambao wanahama kutoka eneo moja kwenda eneo jingine basi tuachie maeneo hayo ili kuruhusu mzunguko wa wanyama kiikolojia waweze ku-*move* kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde thelathini malizia mchango wako.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia na hoja iliyojitokeza katika Jimbo la Biharamulo ambalo ilielezewa na Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa. Kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwamba kumekuwepo na tuhuma ambazo zinaidhalilisha Serikali, kwamba kuna watumishi ambao wamekuwa wakipokea kiasi kidogo wanaruhusu wananchi wanaenda kulima katika maeneo ya hifadhi. Ninaahidi kwamba hili tutaenda kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, pia nataka nitoe taarifa tu kwamba tarehe 24 Oktoba, 2022 tulikamata baadhi ya wakulima ambao walikuwa wamechangishana fedha na wakataka kumrubuni Mhifadhi wa Biharamulo, taarifa hizi ziko TAKUKURU ninavyoongea na hawa watuhumiwa walifikishwa Mahakamani. Tunachoomba ni ushirikiano, anayetoa rushwa

na anayepokea wote wako matatani. Kwa hiyo, kama wananchi wanashiriki kutoa rushwa ili waende kulima kwenye maeneo yale, sheria zitachukua mkondo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kumekuwa na changamoto ya wakulima ambao wanaingia kisirisiri wanalima, tunapoenda kuyazuia yale maeneo tayari wanakuwa wamefika kwenye hatua ya kuvuna, tunaporuhusu sasa kwamba mkimaliza kuvuna sasa msiingie tena, wanaweka kwenye makoti yao mbegu tena ambayo hiyo mbegu anapovuna anapanda tena kule halafu anakuja analalamika kwamba kwa nini tumezuia haya mazao,

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu hili naomba ……

**SPIKA:** Sawa Mheshimiwa, nilishakuongeza sekunde thelathini naona umejiongeza dakika nyingi zaidi. Haya malizia sentensi yako.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, tunaomba wakulima tunapozuia basi wasiingie hifadhini kwa sababu haya maeo tunayalinda kwa maslahi ya taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima atafuatiwa na Dkt. Ndumbaro Mheshimiwa Patrobass Katambi, ajiandae.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia kwenye mjadala huu wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninawashukuru Wabunge wote ambao wamechangia katika eneo la maendeleo na ustawi wa jamii wakijielekeza kwenye hoja ya mmomonyoko wa maadili unaoathiri mila na tamaduni zetu nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kwamba mmomonyoko wa maadili ni jukumu au ni kazi ya taasisi ya familia. Taasisi ya familia ambayo ndiyo chimbuko la watoto inatakiwa kurithisha maadili mema kwa watoto wao. Hivi karibuni kama walivyosema Wabunge wengi kuna kuyumba kwa taasisi hii ya familia ambapo sasa watoto wale hakuna anaewatunza katika malezi na makuzi.

Mheshimiwa Spika, imekuwa taasisi ya familia Baba na Mama na walezi ni rahisi kulea na kutunza na kufuatilia maslahi ya gari wanaloendesha, maslahi ya nyumba waliyoijenga, mali walizonazo kama ni mashamba na vitu vingine kuliko kufuatilia malezi na makuzi ya watoto. Kinachoendelea kwenye familia kwenye suala la mmomonyoko wa maadili, linalochangia maovu mengi sana ukianza ulawiti, ubakaji, kuvuta dawa za kulevya, wizi mpaka tunapata panya *road*.

Mheshimiwa Spika, nikirudi kwenye suala la ulawiti asilimia 60 ya uovu huu unatokea majumbani. Watoto walawiti wanafundishwa na ndugu zao wa karibu halafu ndiyo wanatoka kwenda kuendeleza mtaani, hofu ya Mungu inakuwa haipo, matokeo yake kila anayekuja na mila yake anapita kokote anapandikiza kwenye kichwa cha hawa watoto lolote lile. Hivyo inabidi taasisi ya familia irudi kwenye misingi yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema Serikali inafanya nini eneo hili. Serikali imefanya mambo mengi sana na mambo haya tumekuwa tukiyatangaza na kuelimisha katika majukwaa mbalimbali na katika vyombo mbalimbali vya Habari. Kitu cha kwanza kikubwa Dkt. Samia Suluhu Hassan

alichokifanya katika kuangalia mstakabali wa hatma ya Taifa hili kwa miaka mingi ni kuiunda hii Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ili iwekeze nguvu zaidi kuhakikisha masuala ya maendeleo na ustawi wa jamii yanakaa sawa.

Mheshimiwa Spika, ninalishukuru Bunge lako Tukufu pia umeunda Kamati ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii ili kuongeza nguvu kushirikiana na Wizara hii na kutoa uongozi katika ajenda zote zilizojadiliwa humu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niseme kwamba Serikali imeendelea na mpango wake wa kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto, ulianza mwaka 2017 umeisha Juni, 2022 sasa tunakwenda kuzindua mwingine wa pili ambako ndani tumeboresha ile mikakati mpaka kwenye Halmashauri zetu kule ajenda hii tumepeleka maelekezo iwe ya kudumu kwenye vikao vyao vyote vya Kijiji, vya Mtaa, vya Kata, kwenye Halmashauri, Kamati zote za *Full Council*, na *Full Council* na tutafuatilia kuona utekelezaji wake inajadiliwa vipi.

Mheshimiwa Spika, Sheria Ndogo zitatungwa pamoja na mengine yote taarifa zitawasilishwa sambamba kama tunavyofanya kwenye lishe, tuna mikataba ya utekelezaji masuala ya lishe, hata kwenye masuala ya mmomonyoko wa maadili tutakwenda na sura hiyo ili ku-*stimulate* haya masuala yaweze kujadiliwa kwa upana wake.

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa gwajima kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

**T A A R I F A**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa mchangiaji amezungumzia akina Mama na Watoto, hivi wanaume wenyewe huwa hawapati manyanyaso maana wenyewe hajawazungumzia Mheshimiwa Waziri *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri taarifa hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Maganga unaipokea?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ninaipokea naomba kutoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, katika suala hili la ukatili wa kijinsia na kwa watoto kwenye jinsia tunamaanisha jinsia ya 'ME' na 'KE' kwa hiyo hata kwenye madawati yetu ya jinsia, kama baba amekatiliwa akiripoti pale anahudumiwa kama ambavyo mama atahudumiwa lakini wanaume wamekuwa hawaji wanaona aibu, inabidi huu utamaduni tuubadilishe, wakishaona aibu wanakaa nayo moyoni la kwanza, la pili, la tatu wanachukua kisu wanaumiza au wanaua au wanafanya chochote kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nilindie dakika zangu mbili.

**SPIKA:** Mheshimiwa ukipewa taarifa, ni sehemu ya mchango wako. Kwa hiyo, hapa hulindiwi muda wako. Siyo muda wangu unaotumika, ni wakwako. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSI, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, niendelee?

**SPIKA:** Dakika moja, malizia mchango wako.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSI, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, tuna *program* ya malezi na makuzo kama Serikali ambayo imeanza 2021 mpaka 2025. Inajielekeza kwenye malezi na makuzi ya watoto sambamba na wazazi, watapata semina jinsi ya kulea watoto wao. Tuna *program* ya kuwekeza kwenye afya na maendeleo ya vijana balehe kuanzia miaka 10 mpaka 19. Hii nayo ni mwendelezo wa Taifa kusuka mifumo ya malezi na makuzi kwa vijana wake. Pia tuna *community centered approach* ambapo kampeni za jamii zitafanyika huko huko waliko ili kuhamasisha kaya pamoja na familia ziendelee kufuatilia na kuelimika na kujua juu ya masuala haya.

Mheshimiwa Spika, tuna mambo mengi…

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa hii hoja ni ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, natarajia ulikusudia kuunga mkono hoja? Siyo!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSI, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, hakika naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, atafutiwa na Mheshimiwa Patrobass Katambi, na Mheshimiwa Profesa Ndalichako ajiandae.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia hoja iliyoko Mezani. Katika mijadala ambayo imeendelea kwa siku kadhaa humu ndani, tumekuwa tukijadili sana kuhusiana na makosa dhidi ya maadili. Michango mingi imekuwa ikionyesha kwamba kana kwamba hatuna sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kulijulisha rasmi Bunge lako Tukufu pamoja na Watanzania wote kwamba sheria hizi tunazo toka mwaka 1934. Tulizifanyia mabadiliko mwaka 1959, lakini tukafanya mabadiliko makubwa zaidi mwaka 1998 kupitia Sheria za Makosa ya Kujamiiana. Kwa hiyo, sheria hizi zipo na ni kali. Sasa changamoto imekuwa ni kwenye utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa pia kuwa tarehe 5 Aprili, 2023 Tume ya Kurekebisha Sheria kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo viongozi wa dini na wadau wengine mbalimbali ilifanya kongamano la tathmini ya utekelezaji wa sheria hizi za makosa dhidi ya maadili. Mchakato huo bado unaendelea. Sisi Serikali bado tunaendelea kupokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali kujua ni kwa nini utekelezaji wa sheria umekuwa na changamoto.

Mheshimiwa Spika, kama ulivyoelekeza leo, tutakuja na matokeo ya tathmini hiyo na ikibidi kufanya marekebisho ya sheria hiyo, tutafanya marekebisho. La msingi ni kwamba sheria zipo, hatuhitaji kutunga sheria nyingine, sana sana ikibidi tuweze kufanya marekebisho ya sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa maana ya muda, ninaomba niishie hapo, lakini muhimu zaidi naunga mkono hoja iliyowekwa Mezani na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Patrobass Katambi, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Ndalichako, na Mheshimiwa Jenista Mhagama ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii nami

niweze kuchangia katika Bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema siku hii ya leo, na pia tangu tulipoanza shughuli hizi za Bunge. Aidha, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan ambaye kwa wakati wote ameendelea kuonesha mfano tangu alipoingia katika madaraka.

Katika kipindi cha miaka miwili amefanya kazi kubwa sana ambayo Watanzania wote tunaiona na tunaishuhudia katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo miongozo yake, maelezo yake katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa kweli sisi sote ni mashuhuda kwamba Mheshimiwa Rais amedhamiria kutuletea maendeleo katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wangu Mheshimiwa Joyce Ndalichako na Mheshimiwa Mama Mhagama ambao kwa maelekezo yao wamenisaidia sana katika kutekeleza majukumu yangu pamoja na Katibu Mkuu na Watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitakushukuru wewe pamoja na Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wa Kamati za Bunge na Wabunge wote kwa kutusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, nianze kwanza kwa kusema naunga hoja mkono na vile vile kwa sababu ya muda, katika yale yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wametoa michango, maoni, mapendekezo na ushauri katika maeneo mbalimbali, niombe tu kwamba yaingie katika Kumbukumbu za Bunge *(Hansard)* katika taarifa yote ambayo nilipaswa kuiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, nitaenda kugusia machache. Mengi tunayachukuwa na tunaenda kuyafanyia kazi kadri tulivyoelekezwa na kushauriwa na Waheshimiwa Wabunge. Lipo suala la fedha za ukarabati wa Vyuo vya Watu Wenye Ulemavu na Utangamao. Ofisi ya Waziri Mkuu imefanya jukumu hilo na ilitekeleza na tumeendelea kutekeleza na mpaka sasa tunavyozungumza, kwa mafanikio makubwa Mheshimiwa Rais ametusadia kuweza kufufua vyuo zaidi ya saba ambavyo vilikuwa viko hoi, kwa zaidi ya miaka 10 vilikuwa havifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, tayari Chuo cha Masiwani Tanga kimefunguliwa, kinafanya kazi na wanafunzi ambao ni Wwatu Wenye Ulemavu tayari wameshaanza kupata mafunzo. Chuo cha Luanzari pale Tabora tayari kimeshaanza kufanya kazi, pia Chuo cha Saba Saba Singida, Mtapika Mtwara, na Chuo cha Yombo. Vyote hivi ni kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais amefanya kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, vile vile, katika maeneo hayo, pia katika hoja nyingi ambazo za Waheshimiwa Wabunge zilizoelekeza kwamba tuangalie katika kutoa unafuu kwa watu wenye ulemavu, nawashukuru sana kwa michango yao, lakini pia Mheshimiwa Rais alitoa fedha zaidi ya Shilingi milioni 60 ambazo zimeendelea kutolewa kwenye mwaka wa fedha kuwasaidia watu wenye ulemavu kupata mafuta yale maalum ya ngozi. Vile vile kana kwamba haitoshi Mheshimiwa Rais kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na kwa maagizo ya Mheshimiwa Rais na maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tayari tumeshashaandaa mwongozo maalum ambao unawataka kutoa 3% kwa watu wenye ulemavu ya ajira zote ambazo zinatangazwa. Kama mmeona Mheshimiwa Rais ameendelea kutoa ajira na watu wenye ulemavu tumeendelea kuwapa kipaumbele katika kutoa ajira kwa kufuta mwongozo huo unaotutaka katika ajira zote zinazotangazwa 3% angalau iwe ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, pia katika upande ya watu wenye ulemavu, kwenye eneo lingine, tumeweza pia kufanikiwa kupitia Mheshimiwa Rais, ameweza kuchukua Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu (SHIVIAWATA) na yeye mwenyewe aliwaalika Ikulu ya Chamwino na zaidi ya hapo akatoa ahadi ya kutoa kiwanja kwa ajili ya kujenga Makao Makuu ya Watu Wenye Ulemavu hapa Dodoma. Mheshimiwa Rais ameshaanza kutekeleza, ametoa kiwanja chenye thamani ya Shilingi milioni 37 kwa ajili wa utekelezaji wa shughuli za watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia lilikuwepo suala lingine la kuhusiana Serikali iweke mikakati ya kukusanya maduhuli kufikia lengo ambalo lilikusudiwa. Katika ukusanyaji wa maduhuli, Ofisi ya Waziri Mkuu tunaipata kupitia vibali vya kazi. Hapa tayari mpango umeshafanywa na tumeshaanza mkakati wa kuangalia namna gani tutaongeza ufanisi katika utekelezaji wa jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, tunatarajia kupata magari 17 ambayo yatafanya kazi ya kufanya ukaguzi kwenye maeneo ya kazi ili kuhakikisha kuna kazi za staha, lakini pia kuna afya na usalama mahali pa kazi na hivyo tutaweza kukusanya tozo na ushuru. Sambamba na hilo, katika sheria yetu inayoratibu ajira za wageni ambayo inataka ada zinazotolewa na watu wanaoomba ajira hawa, wamekuwa wakilipa ada na kwa sababu ya uratibu huu, na kwa sababu ya kufungua makampuni na uwekezaji mkubwa kwa Taifa letu, kumepeleka sasa kuweza kusaidia zaidi kwamba tunaweza tukafikia malengo yaliyokusudiwa kwenye kukusanya maduhuli ambayo tunayakusudia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mikakati ambayo imewekwa pia ni pamoja na kuongeza kupitia Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ni pamoja na kuongezea uwezo *OSHA* kwa maana ya kutoa ajira. Kibali cha ajira kimetoka kwa wafanyakazi zaidi ya 18 ambao tunatarajia wataajiriwa

na kuweza kuongeza fedha katika uratibu wa shughuli za OSHA katika maeneo kuhakikisha kwamba lile jukumu la Ofisi ya Waziri Mkuu la kuhakikisha kuna kazi za staha nchini linatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine kama nilivyoeleza ambazo tutazijibu tu; moja ni hii ya kwamba Serikali iongeze bajeti katika program ya kukuza ujuzi. Lengo la Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2015 kwenda 2025 tunakusudia kutoa mafunzo kwa Watanzania zaidi ya 681, na katika kufanya hivyo itakuwa ni kwa kipindi cha miaka mitano. Tayari Wizara ya Fedha imeji-*commit* kwamba tutaendelea kupata fedha kwa ajili ya kuhakikisha mafunzo haya yanafanyika. Pia kumekuwa na *program* mbalimbali za ukuzaji ujuzi ambapo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 tulipata zaidi ya Shilingi bilioni tisa ambazo zilienda kuwasaidia vijana wengi wa Kitanzania kuweza kupata mafunzo kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pia lilikuwepo suala lingine la kushirikiana na Serikali na wadau mbalimbali katika kutoa *program* hizi za mafunzo. Wapo wadau wa maendeleo ambao tunashirikiana nao; *GIZ*, *International Labour Organization* na *IOM* ili kuona kam tunaweza kushirikiana katika masuala ya kibajeti ili kuweza kuendelea kuboresha na kuhakikisha kwamba tunapata fursa, na pia kuwapa fursa Watanzania wengi katika kupata mafunzo mbalimbali yanayohusiana na kukuza ujuzi na pia kuwaandaa katika kukabiliana na soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, pia lipo suala lingine la fursa za ajira nje ya nchi. Hili tumeshaanza kulifanya. Kama tulivyoeleza pia kwenye hoja za Kamati na Waheshimiwa Wabunge kupitia Wakala wa Ajira Nchini *(TAESA)* ambapo tayari tumeshasajili na kupitia kamishna wa kazi. Tumeshasajili Wakala wa Ajira ambao wanatafuta ajira ndani na nje ya nchi na kwa kufanya hivyo, tayari tumeingia *bilateral agreement* na nchi

zaidi ya nane ambayo tunaingia nao katika majadiliano ili kuweza kuona namna gani tunaweza kupata fursa zaidi za kuwasaidia Watanzania wengi kuajiriwa nje ya nchi na kutengeneza utaratibu maalum wa kuwasajili wale walio nje ya nchi waliopata ajira ili tuweze *remittance* ambayo ni sehemu ya mapato pia katika Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia kwa kumalizia, lipo suala ambalo Waheshimiwa Wabunge walilizungumzia kuhusiana na kuweka kumbukumbu za hawa watu walioajiriwa nje ya nchi. Tayari tumeshaandaa mfumo maalum wa kieletroniki wa wao kuweza kujisajili na pia tunawasajili wale ambao wanatafutiwa na wakala mbalimbali wa ajira ili kuweza kuwa na kanzidata ambayo itatusaidia katika kuwaratibu na pia kusimamia haki zao huko wanapofanya kazi nje ya nchi. Vile vile kazi zote ambazo ni za nje ya nchi tunataka tuziratibu vizuri ili kuepusha Watanzania wengi kwenda kudhalilishwa ama kuumizwa ama kutendewa matendo yasiyofaa wakiwa nje ya nchi. Hilo ni jukumu ambalo tumeshaanza kulifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuhusiana na maendeleo ya vijana; hapa katika kuboresha kulingana na michango ya Waheshimiwa Wabunge na Kamati, tayari tumeshadilisha miongozo. Mwongozo wa utoaji wa mikopo ule wa asilimia 10 katika Halmashauri, sasa kijana mmoja anaweza kupata mkopo na ni kuanzia Shilingi milioni 10 mpaka milioni 50. Vile vile kwa watu wenye ulemavu, mikopo hii nayo pia inatolewa kwa mapato ghafi ya Halmashauri na tayari mabadiliko ambayo tumeshayafanya huko, ni kuhakikisha pia watu wenye ulemavu kulingana na changamoto zao, ilikuwa ngumu kufanya kazi wakiwa watano, lakini sasa tumefanya mabadiliko, hata mtu mmoja pia anaweza kupewa mkopo kwenye ngazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwenye eneo hilo, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana tunazidi kuuboresha sasa tuweze kuona

ni namna gani tutawafikia vijana wengi zaidi kuweza kuwasaidia: Kwanza, kuwapa mafunzo kama yale ambayo wanamaliza walio wahitimu wa vyuo vikuu, kuwatambua waliko, kutambua kada mbalimbali ambazo wamezisomea, kuwasajili *TAESA* na kuwapeleka kwa waajiri ili wakapate mafunzo ya utayari wa kufanya kazi kwa maana ya *internship.* Tayari tumeshapeleka vijana zaidi ya 6,000 kwenye maeneo mbalimbali na wanachangiwa fedha kidogo na Serikali zaidi ya Shilingi 150,000 kwa mwezi kwa ajili ya kuwaandaa.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nikimalizia kwa sababu ya muda, mambo ni mengi na kwa sababu hoja hizi tayari ziko hapa ziweze kuingia kwenye *Hansard,* Mheshimiwa Rais ameendelea kuweka mpango wa kuwaangalia vijana katika maeneo mbalimbali. Fedha za Bodi ya Mikopo, hizo nazo ni fedha ambayo ni sehemu ya kuwasaidia vijana, kuwaratibu. Zaidi ya Shilingi bilioni 570 ziliongezwa, pia fedha za Halmashauri, zote hizi zinawasaidia hao vijana ambao tumekusudia kuwasaidia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, pamoja na kupeleka mafunzo ya utaifa, uzalendo lakini pia maadili na kuweza kusaidia Taifa kuweza kuwaandaa vijana ambao ni nguvu kazi ya Taifa ya hivi sasa na hata ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, ahsante, mengine Waheshimiwa Mawaziri watanisaidia katika kuweza kuyajumuisha.

MHeshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hoja hii. Kwanza nianze kwa kusema naunga mkono hoja ambayo kwa kweli imesheheni namna ambavyo Serikali imetekeleza mipango ya maendeleo kwa ajili ya kuimarisha uchumi wetu na ustawi wa Watanzania. Pia hoja hii imeweza kuonesha Watanzania namna ambavyo Serikali imeendelea kujipanga na kuweka mipango ya mbele katika kuendelea kuimarisha uchumi na maendeleo ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii nimshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini na kunipa nafasi ya kuwa msaidizi wake katika nafasi hii ya Waziri wa Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye ulemavu. Kipekee nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ametimiza miaka miwili ya uongozi wake na ni hakika ni miaka miwili ya mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge ambao wamesimama kuchangia hapa kila mmoja ameelezea namna ambavyo katika maeneo yake katika jimbo lake ameguswa. Tanzania yote hii imeshuhudia uongozi uliotukuka wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ni kiongozi bora, kiongozi imara, kiongozi shupavu na tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema na maono zaidi ili aendelee kulitumikia Taifa letu na tuendelee kupata mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Viongozi hawa wawili pia wamekuwa wakinipa miongozo na

maelekezo ambayo yameniwezesha kutekeleza majukumu yangu. Naomba niwaahidi viongozi wangu nitaendelea kuwa mtumishi mwaminifu na nitafanya kazi zangu kwa weledi kwa maslahi mapana ya Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nikupongeze wewe, Spika wetu mahiri, Spika wa viwango kwa hakika unatuheshimisha sana Wabunge. Nakupongeza wewe pamoja na Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wetu wa Bunge kwa kazi nzuri wanazofanya na Wenyeviti wote wa Kamati kwa kweli pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote ambao kwa hakika mnatupa ushauri na maoni na mapendekezo yenu yameendelea kuwa chachu ya sisi kujituma zaidi kwa sababu mnawakilisha wananchi. kwa hiyo, lazima tuwasikilize, lazima tufanyie kazi mapendekezo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nishukuru kipekee Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii chini ya uongozi wa Mwenyekiti, Dada yangu Mheshimiwa Fatma Toufiq kwa namna ambavyo wanatupa ushirikiano, ushauri na maelekezo. Wakati wa kuchambua bajeti hii kuna mambo mengi walitushauri na tuliyazingatia wakati tunaandaa bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze dada yangu, pacha wangu Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama kwa kuteuliwa kuwa Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu na nimwahidi kwamba tutafanya kazi kama ilivyo kawaida yetu, kwa weledi wa hali ya juu. Namshukuru kaka yangu Mheshimiwa Boniface Simbachawene ambaye tumefanya naye kazi vizuri mpaka hapo Mheshimiwa Rais alipomteua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee namshukuru Naibu Waziri wangu, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa, bila kuwaacha wadau

wangu wa utatu; Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania pamoja na Chama cha Waajiri Tanzania kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa, pamoja na washirika wa maendeleo; *ILO, UNICEF, UNDFPA* pamoja *GIZ*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee niwashukuru pia wapiga kura wangu Jimbo la Kasulu Mjini ambao ndio wamenipa heshima ya kuwa katika Bunge hili, na niwaahidi kwamba nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, naomba sasa nijibu baadhi ya hoja za Wabunge. Naomba nianze na suala ambalo Waheshimiwa Wabunge wamechangia kuhusu maslahi ya wafanyakazi na hususan wakazungumzia maslahi ya wafanyakazi katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, niwaambie katika pongezi ambazo nimempa Mheshimiwa Rais katika miaka miwili ya uongozi, kama kuna eneo ambalo Mheshimiwa Rais ameligusa na ameweka alama ni kwenye suala la watumishi wa umma na kwenye sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inawathamini wafanyakazi na mchango wao na kupitia Bodi ya Kima cha Chini cha Mishahara tumeweza kutoa amri kupitia Gazeti la Serikali Na. 687 ambalo lilichapishwa tarehe 25 mwezi wa 11 ambapo kima cha chini cha mishahara kwenye sekta binafsi kimeongezwa na utekelezaji umeanza tarehe 1 Januari, 2023.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuendelea kusisitiza waajiri ambao bado wana uzito wa kutekeleza amri hii ni kuwaambia kwamba ni haki ya wafanyakazi kupata mshahara kama ambavyo imeainishwa katika amri ya kima cha chini cha mishahara. Kwa hiyo, katika kaguzi zetu tutaendelea kufuatilia ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanalipwa kama ambavyo Bodi ya Kima cha Chini cha Mishahara imependekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo limezungumziwa ni masuala ya malipo ya mafao ya wastaafu na hata mchangiaji ambaye amezungumza asubuhi hii ya leo amezungumza pia kwamba kuna wastaafu ambao hawalipwi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba ulipaji wa mafao kwa wastaafu umeimarishwa kwa kiwango kikubwa na changamoto zilizokuwepo ambazo zilikuwa zinasababisha wastaafu wasilipwe kwa wakati, Serikali hii ya Awamu ya Sita tayari imezifanyia kazi na changamoto kubwa iliyokuwepo ilikuwa ni ukwasi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na deni la wafanyakazi waliorithiwa kutoka kwenye mfuko uliokuwa *PSPF* ambao wafanyakazi kabla ya mwaka 1999 walikuwa hawachangii. Kwa hiyo, Serikali ilivyowaingiza kwenye mfuko ikawa imeahidi kwamba itawalipia michango kiasi cha shilingi trilioni 4.6 na ninaomba niliambie Bunge lako tukufu. Serikali ya Awamu ya Sita tayari ukiangalia katika Hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 67 aya ya 124; Serikali imeeleza kwamba tayari kiasi cha shilingi trilioni 2.17 kimelipwa. (Makofi)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hoja ni ya Waziri Mkuu kwa hiyo Mawaziri chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu wanajikuta na wao wako katika mazingira ya kuchangia lakini hoja inapokuwa inahitimishwa na Waziri kikanuni haiwezi kupewa taarifa. Kwa hiyo, tuwe tumeelewana vizuri. Mheshimiwa Ndalichako kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya.

**T A A R I F A**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Ndalichako kwamba suala la

ukwasi kwenye *PSSF* bado lipo na kama anasema limeisha niko tayari ku-*resign* Ubunge na mpaka sasa hivi kwa mujibu wa sheria ukwasi inatakiwa iwe 40%. Mpaka sasa hivi kwa taarifa *latest* bado 22% na suala la fedha ambazo unasema zimelipwa, ile ni hatifungani na bado mifuko iko kwenye hali mbaya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, ukwasi huo wa kiasi ulichotaja wewe mwenyewe kabla sijarudi kwa unayempa taarifa unatosheleza kulipa watu mafao ama hautoshelezi, ukwasi huo huo wa asilimia ishirini na ulizozisema wewe.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ukwasi huo kwenye hii mifuko hautoshelezi na ndiyo maana mifuko inaenda kuchukua mpaka kwenye fedha za michango. Mpaka fedha za michango unakwenda kukopa kwenye maeneo mengine. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndalichako unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, siipokei taarifa yake kwa sababu kwanza kazi ya michango ndiyo pamoja na kulipa mafao. Wanakusanya ili pia waweze kulipa mafao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimeeleza deni ambalo Serikali imelipa kupitia hatifungani shilingi trilioni 2.16. Taarifa ya ukwasi anayoizungumzia Mheshimiwa Ester Bulaya ilifanyika mwaka 2020. Leo hii tuko mwaka 2023, kabla ya hapo deni lilikuwa halijalipwa na pamoja na hizi fedha hatifungani ya shilingi trilioni 2.17 lakini pia kulikuwa na madeni mengine ambayo yanatokana na uwekezaji Serikali imelipa shilingi bilioni 500 katika mifuko ya hifadhi ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niendelee.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la ucheleweshwaji wa malipo kwa wastaafu, naomba nilihakikishie Bunge lako kwamba mifuko ya hifadhi ya jamii imeimarisha mifumo yake ya ulipaji wa mafao kwa wastaafu na inalipwa kwa wakati. Kama kuna ucheleweshwaji wowote, basi naomba tupate taarifa lakini niwahakikishie Bunge kwamba sasa hivi Mfuko wa *NSSF,* Mfuko wa *PSSF* unalipa mafao ya wastaafu ndani ya muda ambao umewekwa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana ikatokea kuna tatizo la michango ya mtumishi ambaye anastaafu, hiyo itakuwa ni *case* tofauti. Nazungumzia mtu ambaye amestaafu, michango yake iliwasilishwa na taarifa zake zimekuja kwenye mfuko analipwa mafao yake ndani ya muda ambao umewekwa kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue nafasi hii kutoa wito kama kuna mtu yeyote ana changamoto zozote za kulipwa kwa wakati atoe taarifa ili tuweze kuifanyia kazi lakini kwa maana ya mifuko, mifumo iko imara na wastaafu wanalipwa mafao yao ndani ya muda ambao umewekwa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo lilizungumziwa la kuimarisha mahusiano kazini na kuhakikisha kwamba mabaraza ya wafanyakazi yana fanya kazi vizuri. Kwanza niliambie Bunge lako tukufu sasa hivi tumeimarisha usimamizi kuhakikisha kwamba mabaraza ya wafanyakazi yanaundwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nitoe wito kwa waajiri kuhakikisha kwamba mabaraza haya ya wafanyakazi ambayo yameundwa yanafanya kazi kwa mujibu wa sheria. Watoe nafasi kwa wafanyakazi kufanya vikao kama ambavyo inatakiwa kwa mujibu wa sheria na ofisi yangu

kupitia kwa Kamishna wa Kazi tutaendelea kufuatilia ili kuhakikisha kwamba wanafanya kazi kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, pia umetolewa ushauri kwamba tuendelee kuimarisha Baraza letu la Ushauri na Masuala ya Kazi, Uchumi na Kijamii *LESCO* ili liweze kufanya majukumu yake ipasavyo. Nikuhakikishie kwamba Serikali imejikita katika kuhakikisha kwamba inashughulikia masuala ya wafanyakazi kwenye Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mambo ambayo yamefanyika kupitia *LESCO* katika kipindi cha mwaka wa fedha huu ambao tunauzungumzia. Kwanza ni kutoa ushauri kuhusiana na kima cha chini cha mishahara ambacho kimeshatangazwa kwenye Gazeti la Serikali cha mwezi Novemba na kimeanza kutekelezwa mwezi Januari.

Mheshimiwa Spika, pia *LESCO* imetoa ushauri katika kanuni za sheria ya usalama na afya mahali pa kazi ambazo nazo zinaanza kutumika. *LESCO* imetoa ushauri kuhusu viwango vya posho kwa madereva ambao wanasafirisha shehena za mizigo kwenda nje ya nchi. Waheshimiwa Wabunge mnafahamu kwamba kuna kipindi hali ya upande wa usafirishaji ilikuwa inakuwa tete kutokana na changamoto za madereva kutopata maslahi yao vizuri lakini kupitia *LESCO* tumeweza kufikia mahali ambapo kumekuwa na viwango ambavyo vimependekezwa na tayari vinatumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie jambo jingine kuhusiana na kanuni ya mafao kwa watumishi wa umma almaarufu kama kikotoo. Kumekuwa na upotoshaji mkubwa kuhusiana na hii kanuni ya mafao kwa watumishi na labda hapa nitatumia muda kidogo ili tuweze kwenda vizuri na nitumie fursa hii pia kutoa elimu hata kwa wafanyakazi ambao watakuwa wanatufuatilia kwenye Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kanuni hii ya kukokotoa mafao kwa watumishi wa umma ambayo imeanza kutumika tarehe 1 Julai, 2022 imetokana na sheria Na. 2 ya mwaka 2018 ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambayo ndiyo ilianzisha Mfuko wa Watumishi wa Umma *PSSSF* na iliunganisha mifuko minne; Mfuko wa *GEPF, LAPF, PPF* na *PSPF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuunganisha mifuko hii, mifuko hii ilikuwa na kanuni tofauti za ulipaji wa mafao. Mfuko wa *GEPF* na *PPF* ulikuwa unalipa mafao ya mkupuo ya 25% na mfuko wa *LAPF* pamoja na Mfuko wa *PSPF* ulikuwa unalipa mafao ya mkupuo ya 50%.

Mheshimiwa Spika, vile vile tulikuwa na mfuko kwa ajili ya watumishi kwenye sekta binafsi, *NSSF* ambao ulikuwa unatoa mafao ya mkupuo ya 25%. Baada ya kuunganisha mifuko kulikuwa na ulazima wa kuiainisha kanuni. Huwezi ukawa na mfuko mmoja ambao unalipa wanachama wake kwa kutumia kanuni tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mwaka 2018 ziliundwa kanuni kwa ajili ya kutekeleza sheria hii ambazo ziliweka watumishi wote walipwe mafao ya mkupuo ya 25%. Sasa baada ya kutunga kanuni hizo waliokuwa wanapata mafao ya 50%.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndalichako kuna taarifa. Waheshimiwa Wabunge, kwa kutazama muda wetu taarifa hiyo itakuwa ya mwisho.

**T A A R I F A**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa Waziri kwanza anatakiwa akiri hapa, mifuko iliunganishwa kwa sababu Mfuko Mkubwa wa *PSSF* ulikuwa

kwenye hali mbaya na ulikuwa unakufa. Huo ndiyo ukweli wa kwanza ambao aukiri kwa sababu anafahamu kabla mifuko haijaunganishwa, deni la *PSSF* kwa Serikali ya *pre 1999 and past 1999* ilikuwa zaidi ya shilingi trilioni saba. Kwa hiyo, wakaenda kufanya uhakiki wakaja na shilingi trilioni 4.5 waliokuwa wanataka kuisema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo la kwanza lakini la pili.

**SPIKA:** Haya ahsante sasa taarifa ni moja Mheshimiwa. Mheshimiwa

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo akiri siyo anaongea vitu ambavyo havipo.

**SPIKA:** Mheshimiwa sasa wewe unampa taarifa au unamuuliza swali?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nampa taarifa na ushauri.

**SPIKA:** Wewe umempa taarifa kwa hiyo ana uamuzi wa kupokea taarifa yako au hapana. Sasa ukimwambia akiri maana yake umemuuliza swali. Mheshimiwa Prof. Ndalichako unipokea taarifa hiyo au hapana?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, siwezi kuipokea taarifa kwa sababu hata yeye mwenyewe mtoa taarifa naona hata haelewi anazungumza anataka sijui. Kwa hiyo, siipokei taarifa yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kwa sababu nilikuwa naeleza na Waheshimiwa Wabunge naomba tuwe na utulivu tusikilize kwa sababu nilichokuwa naeleza na yeye anachoingilia sasa ilikuwa ni kitu tofauti. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mifuko hiyo baada ya kuunganishwa na kanuni zikatengenezwa zilikuwa zinalipa watumishi wote mkupuo wa 25%. Sasa baada ya kanuni hii kuanza kutumika ni dhahiri kwamba wale waliokuwa wanalipwa 50% kutoka 50% mpaka 25% walikuwa wanaona wameshushwa mahali pakubwa. Kwa hiyo, kukawa na malalamiko na Serikali hii ni Sikivu, Serikali ikasema kwamba isitishe kuendelea kutumia na hizo kanuni tukae chini tukutane na wafanyakazi na wadau wanaohusika tuje na kanuni ambayo…

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, kuna taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** …itawakutanisha watumishi katikati. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano na kushirikishana, taasisi ambazo zinahusika na wafanyakazi ndiyo tumekuja na kanuni ya 33%. Kwa hiyo, kanuni hii lengo lake ilikuwa inataka kuwakutanisha katikati waliokuwa wanapata 50% na waliokuwa wanapata 25%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niliambie Bunge lako tukufu, kanuni hii ambayo ya 33% imeongeza mafao ya mkupuo kwa wanachama 1,364,050 sawa na 81% ya wanachama wote, waliokuwa wanapata 25%. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watumishi kwenye taasisi zote za umma mafao yenu yameongezeka kutoka 25% mpaka 33%. Watumishi kwenye sekta binafsi kupitia kanuni hii, mafao yenu ya mkupuo yameongezeka.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kanuni hii kuna wafanyakazi 326,137 sawa na 19% ndiyo hao ambao walikuwa wana 50% wamekuja kwenye 33% lakini mafao yao ya pensheni kwa mwezi yameongezeka. Walikuwa wanlipwa 50% sasa wanalipwa 67%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimeona nitoe ufafanuzi huo kwa sababu jambo hili linakuwa linaongelewa kana kwamba yaani wafanyakazi wote wameshushiwa. Wafanyakazi 81% mafao yao ya mkupuo yameongezeka. Wote waliokuwa wanachama wa *PPF* waliokuwa wanachama wa *GEPF, NSSF* mafao yao yameongezeka kutoka mkupuo wa 25% kwenda kwenye mkupuo wa 33%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimalizie kwa kushukuru tena kwa nafasi hii ambayo nimeipata ya kuchangia na naomba niseme naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi huo. Jambo moja tu ambalo inabidi upande wa Serikali muendelee kulifanyia kazi nilishawahi kulizungumza hapa. Wakati wa kutoa ufafanuzi umeeleza kwamba wale ambao wanakuwa wamestaafu wanapewa mafao yao kwa wakati ambao umewekwa kisheria na kikanuni.

Sasa umeeleza kwamba pengine kwa wale ambao wana changamoto kwa michango yao. Hapa pana shida kwa sababu mfanyakazi michango kufika au kutokufika kwenye ule mfuko siyo kazi yake. Yeye anakatwa fedha na mwajiri kwa hiyo, ni kazi ya mwajiri kupeleka na ni kazi ya mfuko kumfuatilia mwajiri ambaye hapeleki hiyo michango. *(Makofi)*

Sasa ile changamoto ile ndiyo inabidi Serikali muendelee kuifanyia kazi. Mtu anapostaafu mpeni mafao yao kwa sababu sheria imeweka utaratibu. Mwajiri ambaye halipi kuna riba ya kulipa na imewekwa ile riba ili apeleke na mtu wa kumdai siyo mwajiriwa. Mwajiriwa hawezi kumwambia mwajiri peleka, nimeambiwa upeleke atafukuzwa hata hiyo kazi. Kwa hiyo, kwenye hilo kidogo nadhani mlifanyie kazi ili mwajiriwa yeye alipwe mafao yake hao wanaodaiana waendelee kudaiana kwa sababu siyo kazi yake kwa kweli kufanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilishamtaja Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu sasa ni nafasi yake ya kuchangia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kabla sijaendelea ninaomba niunge mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao wameunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nianze bila kujisahau kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya ndani ya Taifa letu na kwa kweli naungana na Waheshimiwa Wabunge ambao wanatoa wito kwa Watanzania wote kuendelea kumuunga mkono Rais wetu na kuendelea kumtia moyo, kumwombea na kwa kweli kuhakikisha kwamba anatekeleza majukumu yake sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi, kama mwanamke na ninaamini wanawake wote wa Tanzania baada ya miaka 60 ya uhuru tumeweka historia ya kuwa na Rais wa kwanza mwanamke. Hatusemi ni Rais wa kwanza mwanamke tu lakini tunasema ni

Rais ambaye ana maono makubwa kwa Taifa hili la Tanzania. Kwa hiyo, kwa kweli tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Rais wetu. Tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kazi za Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ninaongea hapa kwa kuchangia hoja muhimu ya Bajeti na ni Bajeti yangu ya kwanza toka Mheshimiwa Rais amefanya mabadiliko ya Baraza la Mawaziri nami naomba nimshukuru sana kwa unyenyekevu mkubwa kwa kuendelea kuniamini na kunipa jukumu la kuja kuwa Waziri wa Nchi ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu lakini ninayehudumu katika eneo la Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la Bunge ni eneo ambalo kwa kweli ninajisikia kwamba ninakuja kuwa mtumishi wenu Waheshimiwa Wabunge wenzangu na ninasema mtumishi wenu kwa maana ipi? Kazi yangu nyingine kubwa ni ya uratibu na hapa leo baadhi ya Wabunge wanasema Mheshimiwa Rais alikuja huku, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja huku, hiki hakijaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizo ni kazi zangu naomba mnitume na nitakuwa mnyamwezi wenu ili ndani ya Serikali tuweze kuongea vizuri pamoja na tunachotaka kwa kweli Waheshimiwa Wabunge mnawawakilisha wananchi. Kwa hiyo, yale ambayo viongozi wetu wakuu wamekuwa wakiyaahidi huko ni wajibu wetu kama Serikali kuyatekeleza na kuhakikisha yanafanyiwa kazi ili ustawi wa wananchi wa Tanzania na Taifa zima viweze kuendelea kwa mbele. Kwa hiyo, ni mtumishi wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana Makamu wa Rais Daktari Mpango kwa kazi kubwa ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. Vilevile nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kazi kubwa anayoifanya. Binafsi nina historia ya kufanya kazi pamoja naye, nimefanya kazi na Waziri Mkuu

kwa miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano; na sasa ninakwenda kwa mwaka mwingine mwaka mmoja Serikali ya Awamu ya Sita na Mheshimiwa Rais amenirudisha tena hapa. Kwa hiyo ninaomba niwahahakikishie yale mnayoyasema wenzangu kuhusu Mheshimiwa Waziri Mkuu ni sahihi, kwa hiyo na yeye tuendelee kumpa nguvu aendelee kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe, jembe letu Dkt. Tulia Ackson na ninaomba kubwa ili tujenge utaratibu tu ndani ya Taifa hili. Mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni.

Mheshimiwa Spika, umeendelea kuliendesha Bunge hili kwa viwango vya kimataifa, umeendelea kuliheshimisha Taifa letu, umeendelea kuwaheshimisha wanawake wa Tanzania, wanaweza. Pia umeendelea kuwaheshimisha wanaume wa Tanzania kwa kukuunga mkono kwa kazi nzuri unazozifanya. Kwa hiyo kwa kweli tunakushukuru sana, tunaona jinsi unavyotekeleza majukumu yako bila upendeleo lakini ukizingatia taratibu, sheria na kanuni zilizowekwa ndani ya Bunge letu. Kwa hiyo nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Naibu Spika, tunawapongeza Wenyeviti wetu wa Bunge. Tumeshuhudia hapa Wenyeviti wetu wa Bunge wakiwa wazoevu kweli kweli na wao wakifuata nyayo zako; tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ninaomba binafsi niwapongeze Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge kule ambako Wizara yangu imewajibika kwao. Tunaye Mheshimiwa Joseph Mhagama, Makamu wake na Wajumbe wa Kamati yake ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Nyongo, Makamu Mwenyekiti, na Wajumbe wote wa Kamati ya Afya na UKIMWI. Mheshimiwa Fatma Toufiq, Makamu Mwenyekiti wake na Wajumbe wote wa Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Mwisho na si kwa umuhimu Mheshimiwa kaka yangu

Sillo Mwenyekiti wa Bajeti, Makamu wake na Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, na huko kwenye Kamati ya Bajeti, Ofisi ya Waziri Mkuu imepitisha Bajeti ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na hapa kabla sijasahau ninaomba nimshukuru sana Daktari Samia Suluhu Hassan kwa kutoa kipaumbele na kutizama mahitaji ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili liweze kufanya kazi zake vizuri katika kuisimamia Serikali yetu. Kwa hiyo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na tunaishukuru sana Kamati ya Bajeti kuendelea kuishauri Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa pacha wangu hapa amenipongeza, na mimi naomba nimpongeze na nimshukuru sana. Ninaomba kumuahidi ushirikiano wa kutosha yeye na Naibu Waziri lakini na timu nzima ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa upande wake. Kwa namna ya pekee nikushukuru sana kaka yangu George Simbachawene, naamini kabisa yale ambayo nimeyakuta umeanza kuyatekeleza kwenye ofisi hii na mimi nitaendelea kuyasimamia na kazi iende mbele na iendelee. Pia nimpongeze Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Ummy ambaye kwa kweli tunajivunia, sasa yuko *maternity leave* kuonyesha akina mama wana uwezo wa kufanya kazi hizo zote, kwa hiyo nampongeza sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Katibu wa Bunge, vilevile Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu na watumishi wote na wakuu wa taasisi zote ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. Kwa namna ya pekee niwashukuru sana wadau wakubwa wa Ofisi yetu, vyama vya siasa nchini, ninawashukuru sana kwa kazi nzuri, ushirikiano, na kila siku wameendelea kutushauri.

Mheshimiwa Spika, hoja zilizoletwa ni nyingi lakini tutazijibu zile ambazo tunaweza kuzijibu hapa, hoja nyingine

zitajibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenye hoja na hoja zingine tutaziwasilisha kwako kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, nimesema hapa ninampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini ninaomba niyaseme kwa ufupi yote ambayo nafikiri ni ya muhimu na baadaye nitaanza kuyachambua moja baada ya nyingine kama muda utaniruhusu.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ninaomba Wabunge wote tuinuke na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna yoyote tunayoweza kwa maamuzi na maono yake ya falsafa yake ya *4R* ambayo ameanza nayo ndani ya nchi hii. Tumeshuhudia kwa kutumia falsafa hiyo Taifa letu limeingia kwenye maridhiano na kutafuta suluhu katika kila jambo, tunampongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kutumia falsafa hiyo tumeweza kujenga Taifa hili likiwa na ustahimilivu; na kila mmoja amekuwa ni mstahimilivu kwa mwenzake, kuanzia vyama vya siasa lakini hata Watanzania kwa namna moja ama nyingine, Mheshimiwa Dkt. Samia tunakupongeza sana kwa falsafa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia Mheshimiwa Rais wetu amekuja pia na falsafa ya *reform,* kuleta mabadiliko. Katika falsafa hii tumeshuhudia mabadiliko makubwa ya kiuongozi, kidemokrasia na ya kiuchumi ndani ya Taifa letu na mahusiano ya kimataifa, hongera sana Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tumeona falsafa hii inataka kutujenga upya; kwa hiyo kila Mtanzania aonje kwamba ni muumini wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa Watanzania wote, tuunge mkono falsafa ya Dkt. Samia ya *4R* katika kuhakikisha Taifa letu linasonga mbele na hasa wale wote ambao ni wadau wakubwa wa demokrasia na siasa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikuhakikishie kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, katika kipindi hiki kifupi tulipata maoni ya kutosha sana kutoka Waheshimiwa Wabunge kuona ni namna gani pamoja na jukumu la kimuundo la Ofisi ya Waziri Mkuu kufanya kazi ya kuratibu shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini kulikuwa na jambo hapo katikati ambalo lilikuwa halijakaa sawa, nalo ni jambo la ufanyaji wa tathmini na ufatiliaji wa shughuli za Serikali kila siku hapa nchini. Ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kupitia bajeti yetu ya mwaka huu maamuzi ya Serikali, kwa maono ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari sasa imeanzishwa idara maalum chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu itashughulika na suala zima na tathmini na ufatiliaji wa masuala na sekta zote ndani ya Serikali katika utendaji kazi wa kila siku. Kwa hiyo naomba tumpongeze sana Mheshimiwa Rais, na pia tumpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kipindi hiki nasema ni kwa nini tunaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Wabunge wamechangia hapa ndani, ilikuwa ni namna gani tunajipanga kukabiliana na maafa kwa namna moja au nyingine, ikiwemo magonjwa haya ya mlipuko ambayo yamekuwa yakijitokeza. Naomba niwahakikishie kwenye bajeti ya mwaka huu ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu tumeanzisha kitengo maalum cha dawati moja la afya katika kushughulikia uratibu wa sekta zote pale yanapotokea magonjwa ya mlipuko ili tuweze kukabiliana nayo na kuangalia usalama wa wananchi wa Tanzania. Kwa hiyo jambo hili pia limefanyiwa kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, tumefanya kazi nzuri pia na Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwenye eneo zima la lishe, tumeshaanza kujitengenezea uratibu na kujiratibu ndani ya Serikali hasa katika kuitizama Sera ya Lishe. Nilimsikia hapa mdogo wangu Neema amezungumza sana jambo hili ni

jambo la mtambuka, na naomba nimwakikishie mdogo wangu Mheshimiwa Mbunge Neema, Wizara ya Afya pamoja na Ofisi ya Waziri Wakuu sasa tunaanza mkakati rasmi wa kuhakikisha Sera hiyo ya Lishe inafanyiwa kazi na tunakuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, vilevile sio Sera ya Lishe tuna sera nyingine muhimu ambazo tuliagizwa, kwa mfano Sera ya UKIMWI na Sera ya Dawa za Kulevya; hayo yote tumeyapa kipaumbele kama Wabunge walivyotushauri kwenye bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo lingine ambalo tumefanya kazi nzuri ni mapambano dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya nchini. Sasa hivi tumeanza kuona kwamba changamoto za kimaadili zinachukua taswira na sura tofauti. Ningeomba tu nitoe wito kwa wananchi wa Tanzania na Waheshimiwa Wabunge, tunaposhughulika na changamoto za kimaadili hizo nyingine tusisahau bado tuna tatizo la UKIMWI na pia tuna tatizo la matumizi ya dawa za kulevya ambazo pia zinaletea uvunjivu mkubwa wa maadili.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya pekee niwapongeze sana mamlaka iliyopewa dhamana ya kupambana na dawa za kulevya hapa nchini. Na kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema na Kamati ilivyotushauri kwa sababu wameendelea kufanya kazi ya kutosha kwenye maeneo yote manne ya kimkakati katika kupambana na matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni eneo la *supply reduction,* kwa maana nyingine kupunguza uingizaji wa dawa za kulevya. Hapo wamefanikiwa kufanya *operation* mbalimbali za kukamata hao ambao wanatuingizia dawa hapa nchini. Tayari watuhumiwa 7,113 tumewakamata; ni kazi nzuri iliyofanywa na mamlaka yetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile wameweza kufanya kaguzi 149 katika maeneo mbalimbali yanayofanya biashara ya kemikali bashirifu. Tumegundua sasa hivi kadiri tunavyoendelea kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya hawa wafanyaji biashara wa dawa za kulevya wanatafuta aina za dawa mbadala na kuendelea kuangamiza kizazi cha Taifa letu. Kwa hiyo tumeendelea kufanya ukaguzi kuhakikisha hata kemikali bashirifu haziwezi kutumika kuwa ni *alternative* ya matumizi ya dawa za kulevya nchini.

Mheshimiwa Spika, tumefanya maboresho ya sheria, na hapa ninaomba niinue sauti yangu kuishukuru sana Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika eneo ambalo limesaidia kupunguza madhara makubwa ya vijana wetu kwenye matumizi ya dawa za kulevya ni utungwaji wa sheria kali, sheria ngumu, ambayo kwa kweli imesaidia sana kupunguza madhara haya. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge, tukiona sheria hii tuliyoiboresha bado haikidhi vigezo vya kupambana na matumizi ya dawa za kulevya mtukubalie tulete tena humu ndani ya Bunge tuendelee kuibadilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki kifupi tumeweza pia kuteketeza mashamba ya bangi ekari 1,133, ili kuhakikisha kwamba tunakuwa salama. Tumefanya kazi nzuri kwenye *demand reduction,* uelewa na utoaji wa elimu kuhusu matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumefanya kazi nzuri kwenye masuala ya *harm reduction,* yaani kupunguza madhara na eneo hili tumeendelea na tiba ya *methodin,* na pia tumeendelea na huduma za *Multiclinics* na bajeti hii tutaongeza ujenzi wa *multi-clinics* nyingine tatu.

Mheshimiwa Spika, tumefikiri sasa tuanze kuwa na *rehabilitation center* ambazo zinamwondoa mtu kwenye

matumizi ya dawa zinamwingiza katika kujifunza ujuzi ili akitoka pale akajiajiri na akafanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru sana Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi wameweza kuchukua vijana 245 kwenye *program* ya kukuza ujuzi, hawa ambao wamekuwa wakitumia dawa za kulevya na wameacha matumizi na wamefundishwa ujuzi.

Mheshimiwa Spika, lakini tunaendelea kufanya ushirikiano wa kinchi, kikanda na kimataifa ili kuhakikisha jambo hili mtambuka tunalifanyia kazi. Tumefanya kazi nzuri kwenye Tume ya Kudhibiti UKIMWI tumeshafanya mapitio na tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Nne wa Kudhibiti UKIMWI, na tayari tumeshaanda mkakati wa tano wa kudhibiti UKIMWI. Na hapa naomba tukumbushane; mnakumbuka mkakati uliopita ulibainisha kwamba changamoto kubwa ilikuwa ni wanaume hawataki UKIMWI na kutumia dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI. Kwa hiyo tunataka kuona utafiti utakaofanyika na ambao umeendelea kufanyika safari hii utatusaidiaje kupambanua changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ilikuwa ni maambukizi makubwa kwa vijana. Kwa hiyo katika mkakati wa tano tutaongeza nguvu zaidi kuhakikisha vijana na nguvu kazi ya Taifa iweze kuwa salama.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ambayo tuliambiwa na Waheshimiwa Wabunge na hasa Kamati kwa mfano ni matumizi ya Ofisi ya Msajili wa Vyama tunayoijenga. Ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa ofisi hiyo itakuwa na tija. Hapo ndipo tutakuwa ni kitovu kikubwa cha mahusiano na ushirikiano wa Baraza la Vyama vya Siasa Nchini kushauriana na kujenga muafaka katika kuendesha siasa kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ofisi hiyo pia ina uwezo wa kutumika kama ni kituo cha kutoa elimu vilevile hata kuwa kitega uchumi kuongeza mapato kwa ajili ya Baraza la Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, pia tumeombwa tuhakikishe tunajenga Kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, tunaishukuru Serikali imetoa fedha bajeti iliyopita na bajeti hii tumepata fedha. Hapa ninaomba kutoa wito kwa taasisi zote za Serikali kutofanya machapisho ya *document* zozote za Serikali nje, na badala yake sasa zipelekwe kwenye kiwanda chetu cha Serikali cha Mpiga Chapa. Hilo ni jambo muhimu na ninaamini ni lazima tulisimamie sana.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, wametushauri Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali sasa awe Wakala; ninaomba kuwadhibitishia mchakato umeanza na ndani ya mwaka wa fedha wa 2023/2024 tutakamilisha na tunamfanya huyu atakuwa ni wakala ili aweze kushindana kwenye soko la ushindani kama wengine wanavyofanya ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ilikuwa ni kuhakikisha tunakuwa na miradi ya maendeleo na hasa kwenye mamlaka ya kudhibiti dawa za kulevya nchini. Kama nilivyosema mwanzo, mwaka huu tumepata fedha ya maendeleo, tuna bilioni sita fedha za nje na biliioni mbili fedha za ndani. Nimesema hapo mwanzo kwamba kazi yetu ni kujenga *Multiclinics* vilevile tutajenga *rehabilitation center* hapa Dodoma ya mfano, ambayo itawaondoa waraibu kwenye kutumia dawa, inawapeleka katika kujifunza ujuzi waweze kujiajiri na kuacha tabia hizo za matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, *ATF* tuliulizwa hapa mfuko wa UKIMWI, kwamba Serikali imejipangaje; tumefanya kazi nzuri Serikali imeweza kutoa fedha ya ziada kabisa tumepata

bilioni moja milioni mia nane themanini. Pia Serikali itaendelea kutenga fedha. Tulichokifanya ni kuwaambia *TACAIDS* kupitia sheria lakini kupitia mameneja ambaye ameajiriwa kuongeza mapato ya mfuko atengeneze mpango mkakati wa kuhakikisha mfuko unatuna na pia tunajenga uwezo wa ndani wa kupambana na UKIMWI badala ya kuendelea kuwa tegemezi. Kwa hiyo jambo hilo pia tumelifanyia kazi ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana ndani ya Serikali wale wasichana ambao wamekuwa wakifanya kazi ambazo si za staha tutashughulika nao pia kuona ni namna gani tunawaondoa huko na tunawafundisha ujuzi ili waweze kujiajiri na kuweza kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, la mwisho labda na si kwa umuhimu, nimepokea maombi ya Mheshimiwa Miraji Mtaturu, ameomba hapa kuangalia majina ya majimbo katika eneo analotoka. Ibara ya 74(6)(c) na Ibara ya 75 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, imeipa jukumu Tume ya Uchaguzi kuratibu, kutathmini na kujenga mipaka ya majimbo nchini. Kwa hiyo tulikuwa tunaomba tu itakapofika muda Mheshimiwa Kingu na Mheshimiwa Mtaturu basi mtuletee mapendekezo ya majina ya hayo majimbo, na hasa kama hayatakuwa na gharama ya kuyagawa na kuyapanga upya basi tunaweza kuangalia tu jina liweze kulingana na sifa na stahiki ya matakwa ya wananchi. Kwa hiyo tutapokea na tutakapopokea basi tutaweza kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda ninaomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu na ninaomba niwaahidi kwa niaba ya watumishi wote kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu tutaendelea kufanya kazi pamoja na nyie, tutaendelea kuratibu shughuli za Serikali, tutaendelea kusikiliza kero za wananchi na kuzifanyia kazi na tutaendelea

kufatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, nakushuru sana, narudia tena kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha kwanza kwa siku ya leo, kwa hivyo tutarejea tena baadaye; lakini kabla sijasitisha shughuli za Bunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo nilikuwa nimesema akutane na Wabunge wa kutoka Manyara kwa ajili ya kujadili changamoto hii ya matrekta haya ya *URSUS* na changamoto wanazozipitia wakulima wa maeneo hayo; lakini nimepata taarifa wako wakulima wa maeneo mengine ambao pia walikopeshwa matrekta hayo.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wote mnaotoka maeneo hayo mkabidhini Mwenyekiti changamoto hizi. Zoezi hilo lifanyike kati ya leo na kesho, kesho mchana Mwenyekiti aniletee hizo changamoto halafu tutatoa maagizo kwa Serikali kuhusu jambo hilo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi kamili alasiri leo.

*(Saa 7:40 Mchana Bunge Lilisitishwa Hadi Saa 10:00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

**13 APRILI, 2023**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Tunaendelea na majadiliano sasa nimwite Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, ili aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa fadhila zake ambazo zimetuwezesha kukutana kwenye Kikao hiki cha Sita cha Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Kumi na Mbili kwa ajili ya kuhitimisha mjadala kuhusu Hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, mbili, kipekee nakushukuru sana wewe binafsi, pia Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza kwa umahiri Bunge lako Tukufu wakati wa mjadala kuhusu Hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa mwaka 2023/2024 tangu nilipowasilisha hoja hii.

Mheshimiwa Spika, tatu, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati za Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba. Pia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini pia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki na Kamati ya Kudumu ya Bunge, Ustawi na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa

Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum kwa kazi kubwa waliyoifanya ikiwemo kutoa michango yenye tija kwenye hoja ya Waziri Mkuu, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne nitumie fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mawaziri wa Sekta na Naibu Waziri waliochangia hoja ya Bajeti ya Waziri Mkuu, kadhalika nawashukuru Makatibu Wakuu na Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara, Mashirika, Wakala na Taasisi zote za Serikali kwa ushirikiano wao mkubwa wa kujitoa kwao katika kufanikisha Hoja ya Bajeti ya Waziri Mkuu, Taasisi zake pamoja na Mfuko wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, tano, vile vile niwashukuru kwa dhati watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri waliyoifanya na ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kipindi cha maandalizi hadi tunapoelekea kuhitimisha mjadala wa Hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sita, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, wenzangu wote kwa hoja na michango yenu muhimu yenye nia ya kuimarisha utendaji wa Serikali. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kuwa michango yenu itakuwa chachu katika kutekeleza kikamilifu wajibu wetu wa Kikatiba na vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wote kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge 101 wamechangia Hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu wakati wa mjadala huu kati yao Waheshimiwa Wabunge 10 walichangia kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja ya Waziri Mkuu. Aidha, kutokana na ufinyu wa muda naomba uridhie nisiwataje mmoja mmoja kwa majina na badala yake majina yao yaingizwe moja kwa moja kwenye *Hansard*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nikiendelea na mjadala wa Hoja ya Waziri Mkuu. Serikali imetoa majibu ya hoja nyingi zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge, kupitia Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, hata hivyo kutokana na ufinyu wa muda Serikali itatoa majibu yenye ufafanuzi zaidi kuhusu hoja zilizosalia kwa maandishi, lakini vile vile Waheshimiwa Mawaziri, wataendelea kutoa ufafanuzi wa kutosha wa baadhi ya hoja zilizoibuliwa kwenye mjadala huu wakati wakiwasilisha hoja ya bajeti za sekta zao.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tarehe 4 Aprili, 2023 katika Mkutano wake wa Kumi na Moja, Kikao cha Kwanza, Bunge lako Tukufu liliazimia kwa pamoja kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuimarisha demokrasia na kukuza diplomasia ya uchumi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nami nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitaungana na Waheshimiwa Wabunge, wenzangu kumshukuru kwa mara nyingine tena Mheshimiwa Rais, kwa juhudi zake katika kuhakikisha kuwa ustawi wa demokrasia nchini sambamba na kuhimarisha miundombinu ya kiuchumi na kijamii ili kuwaletea maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia falsafa yake ya maridhiano, ustamilivu, mageuzi na mabadiliko ameonyesha wazi na tena kwa vitendo nia yake ya kuifanya Tanzania kuwa moja, salama na bila kundi lolote kuwa nyuma katika kufurahia

demokrasia ya kweli hapa nchini. Kwa lugha nyingine amefanikiwa kuendeleza misingi aliyoipokea kutoka kwa watangulizi wake na Waasisi wa Taifa hili ya kukaa pamoja na kushirikiana katika kutafakari, kujadili na kutafuta suluhu ya mambo yanayotuhusu na hivyo kuimarisha umoja na mshikamano wa kitaifa.

Mheshimiwa Spika, nasi tukiwa wawakilishi wa wananchi tumefanya jambo la msingi kutumia jukwaa hili adhimu kabisa katika kumuunga mkono Mheshimiwa Rais, katika kuimarisha demokrasia nchini. Niendelee kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuendelee kuenzi mfumo wa kujadiliana, kukosoana na kutumia Bunge hili Tukufu kuibua mijadala kitaifa pamoja na kuikosoa na kuirekebisha Serikali pale inapobidi.

Mheshimiwa Spika, vile vile nikishukuru Kituo cha Demokrasia Nchini *(TCD)* kwa kuendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Rais, katika kuimarisha demokrasia pamoja na kutatua changamoto za maendeleo ya demokrasia hapa nchini. Sambamba na *(TCD)* inalishukuru sana pia Baraza la Vyama vya Siasa Nchini kwa kuendelea kuhimiza siasa za kistaarabu zinazozingatia sheria na maslahi ya nchi kwa ujumla na kuimarisha uhusiano mzuri baina ya Vyama vya Siasa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tangu kuundwa kwake mwaka 2009, Baraza la Vyama vya Siasa limefanya mambo mengi katika kuhakikisha kunakuwa na siasa za kistarabu zinazozingatia sheria na maslahi ya nchi kwa ujumla na kuimarisha uhusiano mzuri baina ya Vyama vya Siasa. Aidha, Baraza limekuwa kiungo muhimu katika kufanikisha kuundwa kwa kikosi kazi cha Mheshimiwa Rais, ili kushauri masuala mbalimbali ya kuboresha demokrasia ya vyama vingi hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kutoa rai kwa Baraza la Vyama vya Siasa, kuendelea kufanya kazi kwa karibu na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Serikali Kuu na wadau wengine wa Demokrasia ya Vyama vingi ikiwemo Taasisi zisizokuwa za Serikali na zile za Serikali kama Jeshi la Polisi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na Bunge. Serikali kwa upande wake itaendelea kushirikiana na Baraza la Vyama vya Siasa na wadau wote muhimu katika kujenga mustakabali mwema wa demokrasia yetu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nianze kuzungumzia huduma za elimu. Nyote mtakubaliana nami kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kufanya marekebisho ya mazingira kujifunzia na kufundishia kuanzia elimu ya msingi hadi elimu ya juu. Sote tumeshuhudia maboresho makubwa yaliyofanywa katika shule zetu za sekondari, vyuo vya kati na vile vya elimu ya juu hususani katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu na upanuzi wa taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwa upande wa sekondari kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imefanikiwa kujenga vyumba vya madarasa elfu ishirini na kuwezesha wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa mkupuo mmoja kwenda shule. Licha ya mafanikio hayo kwa upande wa elimu ya sekondari katika kipindi cha hivi karibuni tumekuwa tukishuhudia uwepo wa changamoto za msongomano wa wanafunzi wa shule za msingi kwa baadhi ya maeneo, mathalani kati ya shule za msingi 17,000,182 zilizosajiliwa shule 10,000,804 sawa na asilimia 62.87 zina msongamano mkubwa wa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie mpango wa Serikali kuboresha elimu kwenye shule za msingi. Kufuatia hali hiyo Serikali imeanza kutekeleza mpango wa maboresho makubwa ya elimu msingi. Pamoja na mambo mengine mpango huo unalenga kuondoa changamoto ya

msongamano wa wanafunzi kwenye shule za msingi na kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Hadi kufikia Machi, 2023, Serikali imetoa shilingi bilioni 230 kwa halmashauri zote nchini kwa ujenzi wa shule mpya za msingi 302, ujenzi wa vyumba vipya vya madarasa 3,338 kwenye shule za msingi zenye msongamano mkubwa wa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine maboresho haya yameenda sambamba na ukarabati wa shule nane za msingi na ujenzi wa nyumba 41 za Walimu. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa watoto wetu wanapata mazingira rafiki ya kujifunzia ili waweze kutimiza zao na falsafa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine Serikali imetenga shilingi bilioni saba kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vilivyoboreshwa vya mafunzo ya elimu ya awali na mafunzo ya kuwajengea uwezo Walimu wa madarasa ya awali. Kupitia mpango huu madarasa 7,000 ya elimu ya awali yatashehenezwa na vifaa mbalimbali na Walimu zaidi ya 34,000 wa elimu ya awali watajengewa uwezo kuhusu matumizi ya vifaa hivyo pamoja na mbinu bora za ufundishaji.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo zinatekelezwa sanjari na mpango wa miaka mitano ya mafunzo endelevu ya Walimu kazini (MEMKWA). Lengo ni kuboresha utendaji wa Walimu darasani na ujifunzaji wa wanafunzi ambapo Walimu wote wa shule za msingi watanufaika na mpango huo.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kutoa majibu ya hoja mbalimbali. Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 kipengele cha 13 cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba nitumie nafasi hii kujibu na kufafanua baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge zilizoibuliwa wakati mjadala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilikuwa ni Wakurugenzi wa Halmashauri wanazitumia fedha za Mfuko

wa Jimbo kinyume cha sheria. Fedha hizi hazitumiki kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopitishwa na Kamati ya Mfuko wa Jimbo hasa Maafisa Manunuzi kuzuia ununuzi wa vifaa vilivyopendekezwa na Mheshimiwa Mbunge kununuliwa. Je, Mfuko wa Jimbo ni wa Mbunge au ni wa Mkurugenzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jibu hapa ni kwamba, moja ya hoja iliyoibuka wakati wa kuchangia Bajeti ya Waziri Mkuu ni kuhusu fedha hizi kutokutumika kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopitishwa na Kamati ya Mfuko wa Jimbo hasa kutokana na Maafisa Manunuzi kuzuia ununuzi wa vifaa vilivyopendekezwa kununuliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba, Fedha za Mfuko wa Jimbo zinasimamiwa na Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Sura Na.99 na imeeleza kinagaubaga kuwa usimamizi wa fedha za Mbunge wa Jimbo utafanyika kupitia Kamati ya Mfuko wa Jimbo hilo ambayo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hilo na Katibu wake ni Afisa Mipango wa Halmashauri husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa lugha nyingine Mheshimiwa Mbunge, ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko wa Jimbo inayoratibu miradi na shughuli zitakazoelekezwa kupitia Mfuko huo na pia ndiye mwenye mamlaka ya kuitisha vikao vya Kamati hiyo. Kwa upande wake Kamati inalo jukumu la kupokea, kujadili na kupitisha vipaumbele vya matumizi ya fedha za Mfuko huo wa Jimbo kama ilivyokubaliwa na hakuna kikao ambacho kitakaliwa nje ya Mwenyekiti ambaye ni Mbunge wa Jimbo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ni Afisa Masuuli na anao wajibu wa kusimamia na kuhakikisha kwamba fedha za Mfuko za Jimbo

zinaelekezwa kwenye vipaumbele vilivyopitishwa na Kamati ya Mfuko wa Jimbo ambayo Mwenyekiti ni Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika sheria inataka ununuzi wa bidhaa, kazi na huduma kwa kutumia fedha za mfuko ufanyike kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi, Sura Na.410 na kwa msingi huo nitumie nafasi hii kuwaelekeza Wakurugenzi wote wa Halmashauri kuheshimu na kuzingatia vipaumbele vinavyopitishwa na Kamati ya Mfuko wa Jimbo pamoja na kuhakikisha matumizi ya fedha hizo yanazingatia Sheria ya Mfuko wa Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pia ipo Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348 na Sheria ya Manunuzi, Sura 410. Aidha, nimemwelekeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa Maafisa Manunuzi kwenye Halmashauri hawawi vikwazo katika kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vya matumizi ya Fedha za Mfuko wa Jimbo hususani upatikanaji wa vifaa kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma. Pia halmashauri isifanye maamuzi yake nje ya Uenyekiti wa Mbunge ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ni Mikopo kwa Makundi Maalum. Kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu kiasi kidogo cha fedha za mikopo kinachotolewa kwa Makundi Maalum ya Vijana, Wanawake na Wenye Ulemavu kutokidhi matakwa ya kuyainua makundi hayo kwa kufanya shughuli za uzalishaji au biashara. Aidha, kumekuwa na changamoto kwenye baadhi ya halmashauri kutoa fedha hizo kwa Watumishi wa Halmashauri au wakati mwingine vikundi hewa badala ya walengwa na kusababisha fedha za mikopo hiyo kutorejeshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia malalamiko hayo na maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa

Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu matumizi mabaya ya fedha hizo, nazielekeza sasa halmashauri kote nchini kusitisha utoaji wa fedha za mikopo hiyo zitakazotokana na makusanyo ya kuanzia mwezi Aprili hadi Juni mwaka 2023, wakati Serikali inajipanga kwa mfumo mpya wa utoaji wa mikopo hiyo utakaoelekezwa kabla ya mwezi Juni mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni Serikali kuwa tayari kuchukua hatua pale majanga yanapotokea kama ilivyoainishwa kwenye sheria kuendana na uhalisia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa Mpango wa Taifa wa Kujiandaa Kukabiliana na Maafa kwa mwaka 2022 ambao umezingatia viashiria vya maafa nchini, mifumo ya kitaasisi, mahitaji na maendeleo katika shughuli za kujiandaa na kukabiliana na majanga kitaifa. Mpango huu umewezesha utekelezaji wa shughuli za kujiandaa na kukabiliana na maafa kwa kuzingatia taasisi yenye jukumu la msingi na ushirikiano wa sekta na taasisi zisizokuwa za kiserikali kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 6 ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Tawala za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinahimizwa kushughulikia maafa katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kujumuisha katika Mipango ya Bajeti zao hatua za kuzuia na kupunguza madhara ya majanga na kujiandaa kukabiliana na maafa kwa mujibu wa sheria husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni Serikali iweke mkakati maalumu wa kujumuisha watu wenye ulemavu kwenye program ya Taifa ya Kukuza Ujuzi chini ya program nyingine ili kuhakikisha kuwa fursa kwa wenye ulemavu zinaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, jibu hapa ni kwamba Serikali imeandaa mwongozo wa utekelezaji, ujumuishwaji na uimarishwaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu wa mwaka 2022 kwa lengo la kuhakikisha ujumuishwaji wa masuala ya watu wenye ulemavu kwenye programu, miradi na mipango mbali mbali ya maendeleo katika sekta zote za uchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa programu ya Taifa ya kukuza ujuzi, watu wenye ulemavu wamekuwa wakijumuishwa kwa kuhakikisha kuwa matangazo yote ya fursa za mafunzo yanatafsiriwa kwa lugha rafiki na kupelekwa kwenye vyama vya Watu Wenye Ulemavu na kwa Maafisa wa Ustawi wa Jamii na Maafisa wa Maendeleo ya Jamii waliopo katika Halmashauri na Vyombo vya Habari. Mathalani katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya vijana walemavu 1,171 wamenufaika na programu za kukuza ujuzi zinazoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na masuala ya ujuzi, Serikali inahakikisha watu wenye ulemavu wanapewa upendeleo maalum katika masuala ya ajira pamoja na kuimarisha miundombinu mbalimbali na kuifanya kuwa rafiki kwa mahitaji yao. Kwa mfano, katika kutekeleza mpango wa maboresho ya elimu ya msingi kwa mwaka 2022/2023 Serikali inajenga vyumba vya madarasa 41 kwa watu wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, vilevile chini ya Mpango wa Maendeleo ya Ustawi wa Taifa wa Mapambano dhidi ya UVIKO-19 Serikali yetu imetumia Shilingi Bilioni 3.46 kwa ajili ya ukarabati wa Vyuo Vinne vya Ufundi Stadi na marekebisho ya Rwanzari kule Mkoani Tabora, Sabasaba Mkoani Singida, Mtapika Mkoani Mtwara na Yombo Mkoani Dar es Salaam. Ukarabati huo umewezesha vyuo hivyo kuongeza uwezo wa udahili wanafunzi wenye mahitaji maalum kutoka 407 kabla

ya ukarabati na kufikia 800. Aidha fani zilizokuwa zinatolewa awali zimeongezeka kutoka Tatu hadi 10.

Mheshimiwa Spika kama utakavyoona Serikali imeendela kutoa fursa za upendeleo maalum kwa watu wenye mahitaji maalum, katika kuingia kwenye programu ya Taifa ya kukuza ujuzi, chini ya programu nyingine ili kuwawezesha kujikwamua kiuchumi na kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni juu ya hoja kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG),* itakumbukwa kuwa Tarehe 29 Machi, 2023 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* aliwasilisha kwa Mheshimiwa Rais, Taarifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2022. Uwasilishwaji huo ni takwa la Kikatiba kwa mujibu wa Ibara ya 143 kipendele cha (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura Na. 418.

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliainisha baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa na viashiria vya usimamizi usioridhisha wa mali na fedha za umma. Maeneo hayo ni pamoja na matumizi mabaya ya mikopo ya Halmashauri, kasoro za utekelezaji wa miradi na baadhi ya mifumo kutosomana.

Mheshimiwa Spika, wakati wa mjadala wa hoja ya Waziri Mkuu ya mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali ya mwaka 2022/2023 na mwelekeo wa kazi zake kwa mwaka 2023/2024. Waheshimiwa Wabunge wenzangu sambamba na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya hawakuweza kuficha hisia zao kuhusu mwenendo usioridhisha wa uwajibikaji kwa baadhi ya Viongozi na Watendaji ndani ya Serikali, kama ilivyoonesha katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 06 Aprili 2023, taarifa hiyo ya Mdhibiti na Mkaguzi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliwasilishwa hapa Bugeni ikiwa ni utekelezaji wa takwa la Kikatiba linaloielekeza Serikali kuwasilisha Bungeni taarifa hiyo ndani ya siku Saba za kazi kuanzia siku ya Kikao cha Kwanza cha Bunge tangu kuwasilishwa kwake kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, binafsi ninatambua hisia za Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi kwa ujumla, kuhusu ubadhilifu wa mali na fedha za umma uliobainishwa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, sote tulishuhudia hisia na namna Mheshimiwa Rais alivyoonesha kutoridhishwa na ubadhilifu uliobainishwa katika taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hali hiyo na wakati huu ambapo Bunge lako tukufu linaendelea na taratibu zake za kufanyia kazi hoja zilizowasilishwa katika taarifa hiyo, nitumie fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba baada ya ripoti hiyo kuwasilishwa Bungeni, tayari Serikali kwa upande wake imeanza kuifanyia kazi mara moja.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ni kuhakikisha kuwa Maafisa Masuuli wote wanaandaa majibu ya hoja kama inavyoelekezwa katika Sheria na Kanuni za Ukaguzi wa Umma na kusisitizwa na Mheshimiwa Rais. Aidha, nitumie fursa hii kuiwakumbusha Maafisa Masuuli wote kuzingatia maelekezo ya Mhehsimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba wanapitia kwa kina taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kujibu na kuchukua hatua za haraka juu ya hoja zote zilizoibuliwa kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, vilevile naahidi kuwa pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali, taarifa ya kina katika maeneo yaliyobainishwa kuwa na hoja katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali itawasilishwa

katika Bunge lako tukufu kwa kuzingatia Kanuni husika. Aidha, nilihakikishie Bunge na wananchi kuwa Serikali ya Awamu ya Sita haitamfumbia macho yeyote atakaebainika katika ripoti hiyo kuwa amehusika katika matumizi mabaya ya fedha na mali za umma na kuwa hatua kali zitaendelea kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyojadiliwa mbele yetu ni changamoto ya mmomonyoko wa maadili na vitendo vinavyokwenda kinyume ya mila, desturi na tamaduni za Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaendelea na mjadala wa hoja hii ya bajeti ya ofisi ya Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wengi walionesha kukerwa na uwepo wa matukio mbalimbali yanayokinzana na tamaduni, mila na desturi zetu. Matukio na matendo haya yamekuwa yakihatarisha uimara wa ustawi wa familia zetu na msatakabali wa Taifa kwa ujumla. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa nchi yetu inazo sheria kali tu na sheria zetu zote zinasimamia kila eneo, pia zinakataza bayana vitendo hivyo na zimeweka adhabu mbalimbali kwa makosa ya namna hiyo na yale ya udhalilishaji kwa watoto ikiwemo ulawiti. Pia sheria zinazokataza kuweka kwenye mtandao maudhui yanayochochea mahusiano ya jinsi hiyo au maonesho ya sanaa yanayochochea vitendo vinavyoashiria mmomonyoko wa maadili yetu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura Namba 16 ya Sheria ya Tanzania, ambayo inatamka bayana kwamba vitendo vya mapenzi ya jinsia moja au kinyume na maumbile iwe kwa faragha au kwa makubaliano ni kosa la jinai. Sheria hiyo pia inakataza udhalilishaji wa watoto kwenye matendo yanayofanana na hayo, pamoja na kuweka adhabu kwa kosa la kujaribu kufanya vitendo vilivyokatazwa chini ya sheria husika.

Mheshimiwa Spika, Mbili; Kanuni za Maudhui ya Mtandaoni chini ya Tangazo la Serikali Na. 538 la mwaka 2020, linakataza kuweka mtandaoni maudhui yenye kuonesha mahusiano ya jinsia moja sambamba na adhabu zake. Tatu; ipo Sheria ya Makosa ya Kimtandao Sura Namba 22, inazuia kutangaza au kusababisha machapisho ya ngono au matusi kupitia mfumo wa kompyuta au mfumo mwingine wowote wa kiteknolojia na Kanuni nyingnine ni Kanuni ya Baraza la Sanaa la Taifa za mwaka 2018 zinaweka masharti kwamba hakuna kazi ya sanaa itakayopelekwa sokoni kwa walaji kabla ya kupewa kibali cha kuthibitisha kuwa maudhui yamezingatia maadili.

Mheshimiwa Spika, aidha Baraza katika kuhakiki maadili na maudhui linajiridhisha kuwa kazi ya sanaa haishawishi wala kuhamasiha vitendo vya ngono, ushoga, usagaji au matumizi ya dawa za kulevya wakati wote sanaa hiyo inapowasilishwa kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imepokea hoja na michango mbalimbali iliyowasilishwa na itaielekeza Tume ya Marekebisho ya Sheria kuzipitia sheria hizo, kuzifanyia utafiti wa kina na utafiti wa kitaalam ili kubaini mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji na kufanya maboresho yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha nitoe wito kwa Taasisi zote zilizo na wajibu wa kusimamia Sheria, Kanuni na Taratibu tulizojiwekea kama vile Jeshi la Polisi, BASATA, *TCRA,* kutosita kuchukua hatua kali kwa yeyote atakaebainika anavunja sheria hii inayogusa maeneo haya ya kukiuka mila, desturi na utamaduni wetu na kukiuka misingi ya taratibu zetu tulizojiwekea.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hoja na hisia za Wabunge kuhusu matendo haya, watoto wetu pia

wamekuwa ni miongoni mwa wahanga wakuu, kutokana na hali hiyo Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa watoto wanalindwa dhidi ya vitendo vya ukatili.

Mheshimiwa Spika, mathalani, kutokana na matukio ya unyanyasaji wa watoto yaliyoripotiwa hivi karibuni Serikali imechukua hatua Madhubuti, zikiwemio kutoa waraka kwa wamiliki wote wa shule nchini unaoelekeza kuwa kuanzia tarehe 1 Machi, 2023, kuanza utaratibu wa uwepo wa wahudumu wa jinsia ya kike na wa jinsia ya kiume kwenye magari yanayobeba wanafunzi kuelekea na kutoka majumbani mwao.

Mheshimiwa Spika, Mbili; kusimamia ukaguzi wa mara kwa mara kwenye mabasi ya shule ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wa agizo hilo na uwepo wa wahudumu wa jinsia ya kike na kiume kwenye magari hayo unazingatiwa. Tatu; kuthibiti nyimbo na video zisizo na maadali kuchezwa au kuoneshwa kwenye magari ya wanafunzi yanapofanya safari zake. *(Makofi)*

Mhehsimiwa Spika, pamoja na hatua hizo tumeendelea kuimarisha mifumo ya ushirikishwaji jamii ili kurahisishwa upatikanaji wa taarifa pindi jamii inapobaini uwepo wa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na ukiukwaji wa mila, desturi na tamaduni zetu na kuchukua hatua mbalimbali za kisheria kwa wale wanaobainika kuvunja sheria hizo za nchi.

Mheshimiwa Spika, mtakubaliana nami kuwa suala la malezi ya watoto na utunzaji wa mila, desturi na tamaduni zetu ni jukumu la kila mmoja hivyo sote tunao wajibu wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na kizazi salama chenye kuzingatia sheria, mila, desturi na tamaduni. Tamaduni hizi ni zile ambazo tunaziheshimu ambazo pia zinaleta utu na kuimarisha mshikamano wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, nami nitumie fursa hii kuwaasa Watanzania wenzangu kuendelea kuienzi misingi yetu ya mila, tamaduni na desturi zetu nzuri na kuendelea kuzingatia sheria za nchi. Aidha, nitumie Bunge lako tukufu kuwasihi wafuatao:-

Wazazi na walezi; imarisheni uhusiano na urafiki wa watoto wetu ili kupata taarifa za viashiria wa uwepo wa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Jengeni utamaduni wa kutenga muda wa kuwasilikiza watoto ili kujua kinachoendelea katika maisha yao ya nyumbani, mtaani na shuleni vilevile na kuchukua hatua stahiki ikiwemo za kisheria pale inapotokea kuna ukiukwaji wa misingi yetu ya maadili ya malezi ya watoto wetu.

Viongozi wa dini; endeleeni kuwakumbusha waumuni wetu kuzingatia maadili na kushiriki kikamilifu katika kuwalea watoto wetu kiroho, kuwahimiza kuwa waadilifu na kuepuka vitendo visivyokubalika katika jamii. Tumeshuhudia karipio lenu kupitia mikutano yenu, endeleeni kukaripia jamii yetu ili kila mmoja azingatie maadili yetu ya Kitaifa.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wenzangu; endeleeni kuiunga mkono Serikali katika suala la ulinzi wa mtoto wa Kitanzania na usimamizi wa maadili yetu, sote kwa nafasi zetu tuendelee kuhimiza jamii na kuwa mfano katika kutekeleza sheria tulizozitunga wenyewe, kutunza mila, desturi na tamaduni zetu.

Wito kwa Wizara za kisekta; kusimamia kikamilifu sheria tuliojiwekea Kanuni tulizoziweka na miongozo tulionayo pamoja na kuchukua hatua kali za kisheria kwa wale watakaobainika kufanya vitendo kinyume cha sheria na maadili ya Taifa letu.

Asasi za Kiraia; kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa vibali vyao vya usajili kwa Taasisi zitakazobainika kwenda

kinyume na malengo ya usajili ikiwemo kuhamasisha mmomonyoko wa maadili na vitendo vinavyokinzana na mila za nchi hii, utamaduni wa nchi hii na desturi zetu tutachukua hatua kali za kisheria dhidi ya Taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiwa naelekea kuhitimisha hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu, naomba uniruhusu nitumie jukwaa hili kuzungumzia kwa uchache kabisa kuhusu masuala mawili kama ifuatavyo:-

Suala la kwanza ni pongezi kwa timu yetu ya mpira wa miguu ya *Fountain Gate* kwa kutwaa Ubingwa Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Wanawake wa Shule za Sekondari Barani Afrika. Nikiwa mdau wa michezo nanyi mkiwa wadau wa michezo mmefurahi leo kwamba asubuhi tuliwapokea hapa Bungeni mabingwa wa soka la wanawake wa Shule za Sekondari Barani Afrika kwa mwaka 2023. Shule ya Sekondari ya *Fountain Gate* iliyoko Jijini Dodoma, ambao wameambatana na wanafunzi wenzao. Mafanikio yao yanaifanya *Fountain Gate* kuwa mfano wa kuigwa wa shule na vituo mbalimbali katika kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo kwa watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii hatuwezi kuzungumzia mafanikio ya soka la wanawake nchini bila kuitaja *Fountain Gate*. Kwa mfano, katika kikosi cha Timu cha Wanawake wa *Serengeti Girls* kilichoshiriki katika fainali za Kombe la Dunia za Soka la Wanawake nchini India mwaka 2022 na kuingia hatua ya robo fainali, Timu ya *Fountain Gate* ilikuwa na wachezaji Saba katika kikosi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tumekuwa nao hapa Bungeni, mashujaa wetu, mabinti zetu wa *Fountain Gate*, baada ya kupata mafanikio makubwa na kutwaa ubingwa wa michuano ya *CAF* kwa shule za Sekondari Barani Afrika na kuwa timu ya kwanza kutoka Tanzania kutwaa kombe

lililoandaliwa na *CAF*. Hongereni sana *Fountain Gate*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuipongeza Wizara ya Utamaduni na Michezo kwa kusimamia vema utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995, ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kutengeneza mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuwekeza katika michezo kwa maslahi ya Taifa. Pia napenda kuipongeza Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa kusimamia kikamilifu uendeshaji wa shughuli za michezo shuleni, kutoka shule za msingi na mashindano ya UMITASHUMTA na shule za sekondari kwa mashindano ya UMISETA. Vilevile napongeza Baraza la Michezo Tanzania kwa utendaji mahiri ambao umekuwa chachu ya mafanikio kwenye tasnia ya michezo ikiwemo mpira wa miguu wa wanawake.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji uliofanywa na mmiliki wa *Fountain Gate* wa Jijini Dodoma ni miongoni mwa vielelezo vya mafanikio katika utekelezaji wa sera ya maendeleo ya michezo nchini. Hivyo basi, nitoe wito kwa wadau wa michezo kuiunga mkono Serikali katika kuimarisha miundombinu ya michezo, kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo mbalimbali. Aidha, niwapongeze tena mabinti zetu wachezaji mahiri, mashujaa wanafunzi wa *Fountain Gate* kwa historia waliyoiweka katika soka la Afrika na kulitangaza Taifa letu duniani. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukio la pili ni baadhi ya kumbukizi muhimu katika kipindi cha Aprili kwa Taifa letu. Itakumbukwa kuwa tarehe 7 Aprili mwaka huu, tuliadhimisha kumbukumbu ya miaka 51 tangu kitokee kifo cha Muasisi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mzee wetu Hayati Sheikh Abeid Aman Karume. Aidha leo tunaadhimisha mwaka wa 110 tangu kuzaliwa kwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, jana tarehe 12 Aprili mwaka huu wa 2023 kumeadhimishwa kumbukizi ya miaka 39 tangu kitokee

kifo cha Hayati Edward Moringe Sokoine, Waziri Mkuu wa Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nyote mtakubaliana na mimi kwamba kumbukizi za viongozi hao ni urithi muhimu kwa Taifa kutokana na uzalendo, uwajibikaji na utumishi wao uliotukuka katika Taifa hili, kwa mantiki hiyo, tukiwa Taifa linalothamini na kuenzi utendaji wa Viongozi wetu tunao wajibu siyo tu kuwakumbuka lakini pia kurithisha urithi huo kwa vijana wetu wa sasa na vizazi vijavyo. Kwa kufanya hivyo, tutasaidia vijana wetu na vizazi vijavyo kuyaiga, kuyaenzi na kuyaishi matendo bora yenye tija waliotuachia viongozi hawa na hivyo kuimarisha umoja na mshikamano wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napoelekea kuhitimisha hoja yangu, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuendelea kuiunga mkono Serikali yetu kupitia Bunge hili Tukufu ikiwa ni pamoja na kutoa mapendekezo ya kujenga umoja, kuimarisha mshikamano wa Kitaifa kusaidia Serikali kuwahudumia ipasavyo wananchi wake na kuikosoa pale inapobidi. Aidha, katika maeneo yetu ya uwakilishi tuimarishe ushirikiano na wananchi katika kuhakikisha kwamba miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwenye maeneo yetu inaleta tija iliyokusudiwa na kuhakikisha thamani ya fedha ya umma ambayo imetumika kwenye miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Watanzania wenzangu niwaombe kuendelea kumuunga mkono Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikiwa ni pamoja na kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumjaalia afya njema, maono, hekima na busara katika kuliongoza Taifa hili na kufanikisha azma yake ya kuliletea maenedeleo.

Mheshimiwa Spika, kadhalika niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba Serikali kwa

upande wetu itaendelea kutoa ushirikiano stahiki kwa wananchi na wadau wote muhimu, katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake kwa kuzingatia mustakabali na maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATBU WA BUNGE:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kamati yako sasa ijielekeze kwenye Kitabu cha Pili, Matumizi ya Kawaida. Fungu 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu, ambayo iko ukurasa wa 122.

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 25 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*...........................Sh. 17,440,724,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kifungu hiki kina mshahara wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kuna Wabunge hapa wanataka ufafanuzi wa mambo ya kisera.

Tutaanza na Mheshimiwa Joseph Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa miaka zaidi ya minne Bunge limekuwa likiitaka Serikali kuboresha kazi za ufuatiliaji na tathmini, hasa kwa kuja na Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini na Sheria yake. Imekuwa kila wakifanya *attempt* wanakuwa na migongano kati ya Ofisi ya Rais, Utumishi; Wizara ya Fedha; na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Rais aliagiza tangu mwaka jana 2022 kwamba, sasa masuala ya *M and E* yaboreshwe Serikalini, naomba ufafanuzi kwenye suala hili. Kwa kweli, kama sitaridhika, itabidi nishike Shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, yamekuwa ni maelekezo ya Serikali, maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba tunatakiwa ku-*streamline* masuala ya *Monitoring and Evaluation* katika Serikali. Ni kweli, historia ya masuala haya ya *Monitoring and Evaluation* yalianza toka mwaka 2008 wakati Serikali ikifanya maboresho kwenye sekta ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008 wakati wa maboresho, kulikuwa na *components* nane. Kati ya *component* hizo nane, kubwa ambazo naweza nikazikumbuka kwa sasa ilikuwa ni kuhakikisha kwamba kila

Wizara inakuwa na *section* ya *Monitoring and Evaluation*. Pia tunashughulikia masuala ya *OPRAS,* na pia ilikuwa ni lazima tuhakikishe kwamba tunafuatilia zile *clients service charter.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021, Wizara ya Fedha yenyewe ilianzisha *Department* ndani ya Wizara ambayo ilikuwa inasimamia ufuatiliaji kwenye miradi mikubwa ya kitaifa na ndani yake ikawekwa *unit* ndogo ya *Monitoring and Evaluation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 52 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inampa Mheshimiwa Waziri Mkuu majukumu ya udhibiti kwenye shughuli zote za Serikali, majukumu ya usimamizi wa kazi zote za Serikali na ufuatiliaji. Kwa hiyo, Serikali imefanya maamuzi sasa rasmi kwamba, shughuli zote za *Monitoring and Evaluation* zisimamiwe sasa na Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuzisimamia sekta zote na kusimamia utendaji wa Serikali kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea jukumu hilo, sasa kwenye bajeti ya mwaka huu, tayari Serikali imetenga fedha ya kuanzisha Idara ya *Monitoring and Evaluation* ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Idara hiyo imeshaanza kazi. Kazi kubwa inayofanywa sasa hivi, ingawa suala la sera lilikuwa linafanywa na Wizara ya Fedha, kwa hiyo, sasa tumeanza kukubaliana kwamba ni lazima Ofisi ya Waziri Mkuu iwe Mratibu Mkuu, tupate hiyo sera. Baada ya kupata hiyo sera, sasa tuwe na hiyo sheria kadiri tutakavyokuwa tunakwenda huko mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeamua sasa zile *sections* ambazo zilikuwa katika Wizara zote zibadilishwe na kuwa *units* na zianze ku-*report* moja kwa moja kwa *Accounting Officers.* Mwaka huu wa fedha maelekezo ya Serikali ni bajeti zote na taasisi zote za umma na Serikali kwa ujumla waanzishe kuwa na hizo *units* ambazo zitakuwa

zinashughulikia masuala ya *Monitoring and Evaluation* na yapangiwe bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nilihakikishie Bunge lako kwamba maelekezo ya Mheshimiwa Rais, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, tumeyatekeleza, na tunatekeleza hiyo Ibara ya 52 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hati Idhini ya Mheshimiwa Rais ya kazi za Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa tunalifanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa maelezo hayo, tuchukue muda kama Bunge, kuwaombea wenzetu Serikali kwamba hiyo dira ambayo ameisema Mheshimiwa Waziri iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kuwaombea! Ama sijasikia vizuri! Kuwaombea kwa maana ya kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu, ama!

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani kuwaombea wawe na nguvu ya kuweza kutekeleza haya ambayo wamesema.

**MWENYEKITI:** Aah, kuwaombea, *okay,* sawa. Basi mwenye hoja ameshaelewa, lakini hapa nina jina lingine la Mheshimiwa Mbunge anayetaka ufafanuzi wa jambo la jumla la kisera. Mheshimiwa Ali Hassan King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nataka ufafanuzi juu ya hoja ya *program*

ya Taifa ya kukuza ujuzi nchini, ambapo makubaliano yaliyokuwepo ni kwamba, program hii itapatiwa fedha kupitia *Skills Development Levy* ambayo ni *1/3* ya kila mwaka inayokusanywa na Serikali. Kwa bahati mbaya, kwa sasa haipelekewi fedha hizo. Kwa mwaka huu ilikuwa inakwenda fedha ambayo *program* haitoshelezi kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naiomba Serikali, kwa kuwa hoja hii iko katika malengo ya kitaifa na *program* za kitaifa, kwamba kwa nini Serikali haifanyi yale makubaliano yake ya kutumia ule mfuko kwa ajili ya kui-*fund* hii *program* ambayo ni ya kukuza ujuzi ambayo tunatarajia kuongeza ajira kwa vijana ambapo ajira nyingi sana zinakosekana kutokana na vijana kukosa ujuzi:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba nipate ufafanuzi wa Serikali. Kama ufafanuzi hautakuwa mzuri, nitaendelea kuikamata shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ali King, hiyo 1/3 ni ya makusanyo gani?

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni 1/3 ya makusanyo ya *Skills Development Levy (SDL)*.

**MWENYEKITI:** Hiyo nimeelewa. Ukishasema 1/3 ya makusanyo, nataka nijue makusanyo ya nini? Maana isije kuwa ni makusanyo ya kodi.

Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi. Mheshimiwa Ndalichako.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Ali King pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamekuwa mstari wa

mbele kuhakikisha kwamba wanatetea maslahi ya vijana ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na *program* zinazowajengea ujuzi vijana ili wapate ujuzi unaohitajika katika soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya program hii ya kukuza ujuzi ya kitaifa ni kuwawezesha vijana kupata mafunzo kupitia uwanagenzi, kuwawezesha kupata fursa ya kupata uzoefu, yaani mafunzo kwa vitendo kazini. Hii asilimia anayoisema, yaani mgawanyo wa 1/3 ya fedha za *Skills Development;* fedha hizo zunagawanywa kwa kuzingatia mfumo ambao umewekwa kisheria. Hii 1/3 ni kwa ajili ya ujuzi ambao kati ya fedha hizo nyingine zinakwenda *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kimsingi Serikali inatoa kwa kufuata ule mgawanyo, isipokuwa wanaotoa ujuzi ni zaidi ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, tutakachokifanya, ndani ya Serikali tunaendelea na majadiliano ili *program* hii iweze pia kuendelea kuongezewa fedha kwa ajili ya utekelezaji wake, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ali King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameelezea ule ukweli mpaka, kwenye hii *program*. Ndani ya program hii na makubaliano yake, *VETA* haimo. Ni kwamba, hii programu ina vitu vinne, katika hivyo vitu vyake vinne kama alivyosema, ni mafunzo ya wanagenzi, kuna masuala ya *internship* kwa wanaomaliza vyuo, na pia kuna masuala ya pia kurasimisha ujuzi kwa watu ambao labda pengine wana ujuzi, lakini hawana vyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fedha hizi katika Ofisi hii ya Waziri Mkuu na hasa hii programu, jambo la *VETA* humu halimo. Sasa mimi nilikuwa naulizia mahususi kwamba, kwenye hii programu kwa nini tusitumie na makubaliano hayo yapo? Programu hii ina malengo, ambayo ni kufikia vijana

681,000. Tulipoanza tulikuwa na vijana 42,000, sasa hivi tumeshashuka tuko 12,000 na fedha zile…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ali King, ukisema *VETA* haipo, unamaanisha Waziri alichosema, hayuko sawasawa au unamaanisha katika ule mgawanyo *VETA* haitakiwi kuhesabiwa?

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu ndani ya *program* hii, *VETA* haimo.

**MWENYEKITI:** Yaani haimo kwamba, haitakiwi kuwemo. Yaani *VETA* ihesabiwe kwingine!

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ina *funds* zake nyingine. Sasa…

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa kwa sababu, hii ni mara yako ya pili kuzungumza, tunafahamu kanuni zetu. Ukishakuwa hukubaliani na Waziri, unasema unachotaka kusema.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

**MWENYEKITI:** Kama unataka kuendelea ili tutoe sasa fursa.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyeti wa suala la vijana, tunavyowaona na kila mtu ana jimbo hapa, tunajua vijana; nilikuwa naomba nitoe hoja ili tujadili na Wabunge, ili Serikali iweze kutoa fedha hizi kama ilivyopangwa katika makubaliano haya. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Haya, hoja haijaungwa mkono. Kwa hiyo, tunaendelea. Jina la tatu hapa, Mheshimiwa Neema Mwandabila.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Naona Wabunge mnaguna. Nafikiri hoja yake haijaungwa mkono kwa sababu watu hawajaelewa watachangia kitu gani. Kama hawajaelewa, ndiYo mazingira hayo. Ndiyo kanuni zetu zinataka hivyo, haijaungwa mkono, haijaungwa mkono.

Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nina hoja yangu katika suala la Sera ya Lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishaeleza awali kwamba suala la lishe ni ajenda ya kitaifa na ni ajenda ya kimataifa. Mheshimiwa Rais mwenyewe amekuwa *champion* namba moja, na hata mwaka 2022 tarehe 30 Septemba, walipokuwa wanafanya mapitio ya utekelezaji wa mikataba ya lishe aliagiza kwamba Sera ya Lishe iweze kuhuishwa. Mpaka sasa sera inayotumika ni ya mwaka 1992.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitamani kupata kauli ya Serikali, ni lini sera hii itakuwa tayari? La sivyo, niseme ukweli leo nitashika shilingi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya, naona Mheshimiwa Waziri wa Afya anataka kutoa ufafanuzi.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, nimshukuru sana Mheshimiwa Neema Mwandabila kwa swali lake zuri, na kwa hoja yake. Suala la lishe ni suala la kimkakati ndani ya Serikali na tayari mchakato wa kutunga sera mpya ya lishe tumeshaanza chini ya uratibu wa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mitazamo miwili. Kwa sababu, sera iliyokuwepo, kama alivyosema Mheshimiwa, ni ya *1992,* kwa hiyo, kuna baadhi ya mambo kwa mfano *food fortification* hayapo. Kwa hiyo, tuna mitazamo miwili ndani ya Serikali; tutunge sera moja chini ya Waziri Mkuu halafu sekta ziwe na utekelezaji wa matamko ya kisera au tutunge sera chini ya Wizara ya Afya, lakini iwe chini ya uangalizi wa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo jambo kidogo ndiyo tumepata wataalam. Kama alivyosema, Mheshimiwa Rais ni Mjumbe wa *Presidential Group on Nutrition,* Marais kama watano, sita. Kwa hiyo, ameshaelekeza, tunafanya *review* ili tuje na sera ambayo itakuwa pia imechukua *into consideration* maelekezo au maoni ya kamati hii ambayo imeundwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tumwahidi Mheshimiwa Mbunge, ndani ya miezi sita tutakuwa angalau tuna Rasimu ya Sera ya Taifa ya Lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja pia imetoka, isiwe tu ni Sera ya Lishe, tuseme Sera ya Taifa ya Lishe na Usalama wa Chakula. Kwa hiyo, ni jambo ambalo tunahitaji kufanya mashauriano makubwa ndani ya Serikali na nje ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema. Aah, humu ndani mko Neema wawili. Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naongea kwa masikitiko makubwa sana kwa suala la Sera ya Lishe kwa sababu, ni kitu ambacho kimeanza tangu mwaka 2017 mchakato ulishaanza. Tunapoongea suala la lishe, ni kitu mtambuka, ni sekta nyingi zinaguswa na ni kitu ambacho moja kwa moja kinaenda chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, linapokuwa linayumbishwa kupelekwa kwenye Wizara ya Afya, naona ni kitu ambacho siyo sawa. Kwa sababu, afya yenyewe *parse* tuna-*deal* na mambo ya

*prevention* na *treatment,* kuna mambo ya kulima, kuna mambo ya *advocacy,* na mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu naipokea kauli ya Mheshimiwa Waziri ya kwamba baada ya miezi sita tutakuwa na rasimu ya masuala ya hiyo Sera ya Lishe. Walishaanza wakafika hatua fulani, hatujajua ni kitu gani kiliwakwamisha, lakini tuwaombe watie jitihada kwa sababu, kuna kazi nyingine au kuna mambo mengine wajasiriamali wetu wanashindwa kufikia masoko mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, unapoongelea suala la…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ngoja. Mheshimiwa Neema ukisimama kwa hii sehemu ya pili, ni kwamba maelezo unakuwa ulishayatoa mwanzoni. Ukisimama mara ya pili ni unaeleza kama umeelewa yale aliyosema na unakubaliananayo au vipi. Yaani unasema sentensi moja au mbili, kwamba umekubali ama hujakubali yale ambayo ameyasema halafu tunaendelea na utaratibu. Haupati nafasi ya kuchangia tena.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nilitaka tu kusemea kitu alichokuwa ameongea kwamba, iitwe Sera ya Lishe na Usalama wa Chakula. Ukishaongea lishe, usalama wa chakula upo ndani yake, itakuwa na uwezo wa kuchakatwa. Kwa hiyo, nilikuwa najaribu kushauri hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu, nakubaliana na kauli ya Waziri. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, hawa ndio waliokuwa wanataka ufafanuzi. Labda tu Mheshimiwa Waziri kwa sababu umesema ndani ya miezi sita, nadhani ushiriki wa wadau uwe mpana zaidi ili muone kama

hivi vitu havihitaji sera tofauti. Kwa sababu nakumbuka huu mjadala umeshawahi kutokea hapa ndani wa lishe kama usalama wa chakula umo ndani. Sasa usalama wa chakula una utofauti na chakula kilicho salama na mambo kama haya.

Sasa kama ni lishe na unazungumzia na chakula kilicho salama, hilo ni suala lingine, lakini kama unazungumzia *food security,* nadhani ni tofauti kidogo na *nutrition.* Sasa *nutrition* inaweza kwenda na vyovyote vile, wewe umeelewa, mtaalamu. Si umenielewa! Si ndiyo Mheshimiwa! Sawa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hiyo ni ili tusichanganye mambo yote kwenye sera moja halafu tukaona tena kuna upungufu. Kwa hiyo, ni afadhali sera moja ishughulike na mambo yote yanayohusu hilo jambo. Kama kuna sababu, sera nyingine, lakini ukiyachanganya tena, tutaanza tena kurudi nyuma na kwenda mbele.

Waheshimiwa Wajumbe, hayo ndiyo majina niliyokuwa nayo hapa mbele yaliyokuwa yanahitaji ufafanuzi kwenye mambo ya kisera na mmeona wote ambao wamezileta hoja zao zimejibiwa na wamekubali ufafanuzi uliotolewa na Serikali. Kwa hiyo tunaendelea.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 15 – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management… ... ... … … … ..*Sh. 1,538,395,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit… …* Sh. 204,295,000
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring & Evaluation Unit… … ... ... … … … ... ... ... ... ...*Sh. 238,035,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit… … … … …* Sh. 218,440,000

Kifungu 1005 – *Information, Communication & Technology Unit… … … … ... ... ..*Sh. 183,764,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit… ... ... … … … ... ... ... ... ... ...*Sh. 211,710,000
Kifungu 2001 – *Mediation… … … … … … … …*Sh. 1,204,253,000
Kifungu 2002 – *Arbitration.. … … … … … … …* Sh. 1,168,147,000
Kifungu 2003 – *Dodoma Regional Office...… … …*Sh. 3,000,000
Kifungu 2004 – *Lindi Regional Office … … … … …* Sh. 3,000,000
Kifungu 2006 – *Ruvuma Regional Office... … … …* Sh. 6,000,000
Kifungu 2007 – *Kigoma Regional Office… … … …* Sh. 3,000,000
Kifungu 2008 – *Iringa Regional Office... … … … …* Sh. 3,600,000
Kifungu 2009 – *Njombe Regional Office… … … …* Sh. 3,000,000
Kifungu 2010 – *Geita Regional Office... … … … …* Sh. 3,000,000
Kifungu 2011 – *Mara Regional Office… … … … …* Sh. 3,600,000
Kifungu 2012 – *Singida Regional Office … … … …* Sh. 3,000,000
Kifungu 2013 – *Kagera Regional Office… … … …* Sh. 3,600,000
Kifungu 2014 – *Shinyanga Regional Office… … …* Sh. 3,325,000
Kifungu 2015 – *Katavi Regional Office...… … … …* Sh. 3,000,000
Kifungu 2016 – *Tabora Regional Office… … … …* Sh. 3,000,000
Kifungu 2017 – *Mbeya Regional Office… … … …* Sh. 6,000,000
Kifungu 2018 – *Arusha Regional Office… … … …* Sh. 13,150,000
Kifungu 2019 – *Mtwara Regional Office… … … …* Sh. 3,000,000
Kifungu 2020 – *Pwani Regional Office... … … … …*Sh. 6,600,000
Kifungu 2021 – *Tanga Regional Office... … … … …*Sh. 3,600,000
Kifungu 2022 – *Mwanza Regional Office...… … …* Sh. 6,000,000
Kifungu 2023 – *Songwe Regional Office... … … …* Sh. 3,000,000
Kifungu 2024 – *Manyara Regional Office… … …* Sh. 2,400,000
Kifungu 2025 – *Dar es Salaam Regional Office… … … … … … … … … ..*Sh. 117,142,000
Kifungu 2026 – *Rukwa Regional Office… … ... ... ...*Sh. 3,000,000
Kifungu 2028 – *Kilimanjaro Regional Office... … …* Sh. 3,000,000
Kifungu 5005 – *Morogoro Regional Office … … …*Sh. 3,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 27 – Msajili wa Vyama vya Siasa**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*… … … … … … … Sh. 960,112,687
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*… … Sh. 334,735,643
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring, Evaluation & Research Unit*… … … ... ... ... ... ..Sh. 262,926,849
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit* … … … … … Sh. 244,231,108
Kifungu 1005–*Procurement Management Unit*...Sh. 207,450,708
Kifungu 1006 – *Information & Communication Technology Unit*… … … … ... ... ..Sh. 530,654,817
Kifungu 1007 – *Communication and Civic Education Unit* … … … … … … ...Sh.181,965,391
Kifungu 1008 – *Reg & Monitoring of Political Parties Division*… … … … ... ... ... Sh. 789,974,786
Kifungu 1009 – *Election expenses and Grants Division*… … … ... ... ... .Sh. 18,119,083,699
Kifungu 1010 – *Political Parties Unit*...… … … …Sh. 1,586,662,000
Kifungu 1011 – *Zanzibar Office*...… … … … … …Sh. 351,989,312
Kifungu 1012 – *Legal Services Unit*..… … … … …Sh. 151,264,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu**

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Fungu hili Serikali imeleta *addendum*.

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*… … Sh. 8,922,901,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit* … Sh. 2,067,590,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*...… …Sh. 1,080,447,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*… … … … … Sh. 373,151,000
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*… … … … … … … … … … ...Sh. 298,345,000

Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit* … … … … … … … … … … … ..Sh. 490,505,000
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit* … … … … … Sh. 311,771,000
Kifungu 1008 – *Management Information System Unit* … … … … … … … ….Sh. 322,773,000
Kifungu 2001 – *Civil Affairs and Contingencies*… … … … … … Sh. 2,990,269,000
Kifungu 2002 – *National Festivals*..…. … … … … Sh. 818,627,000
Kifungu 3001 – *Parliamentary and Political Affairs*… … … … … … ... ... ... ... ...Sh. 933,464,000
Kifungu 4001 – *Private Sector Development & Economic Empowerment*… … ... ... ... ... .Sh. 0
Kifungu 5001 – *Coordination of Government Business*… … … … … … … … ...Sh. 3,148,303,000
Kifungu 5002 – *Performance, Monitoring & Evaluation Division*… … … ... ... Sh. 1,179,180,000
Kifungu 6001 – *Investment Development Division*... ..…. … Sh. 0
Kifungu 7001 – *Government Printer* … … … …Sh. 2,931,392,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 42 – Mfuko wa Ofisi ya Bunge**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division* … … …Sh. 13,449,548,000
Kifungu 1002 – *Library and Research Division* … Sh. 623,484,000
Kifungu 1003 – *Information and Communication Technology Unit*…. … … … … .Sh. 1,501,221,000
Kifungu 2001 – *Budget Division*... … … … … …Sh. 3,134,376,000
Kifungu 2002 – *Table Office Division*… … … Sh. 110,322,174,000
Kifungu 2003 – *Parliamentary Committees Division*… … … … … ... ... ... ...Sh. 15,476,688,000
Kifungu 2004 – *Hansard Unit*… … … … … … …Sh. 1,154,896,000
Kifungu 2005 – *Legal Services Division* … … … Sh. 2,934,280,000
Kifungu 3001 – *Private Office of The Speaker*… … … … … … … … Sh. 1,430,922,000

Kifungu 3002 – *Private Office of The Deputy Speaker… … … … … … … … ... ... .*Sh. 794,922,000
Kifungu 3003 – *Office of The Leader of Opposition… … …* Sh. 0
Kifungu 3004 – *Private Office of The Clerk… …*Sh. 1,272,504,000
Kifungu 3005 – *Finance and Accounts Unit...…* Sh. 942,920,000
Kifungu 3006 – *Communication and International Relations Unit… … … … … … ..*Sh. 4,698,622,000
Kifungu 3008 – *Internal Audit Unit … … … … …* Sh. 562,836,000
Kifungu 3009 – *Procurement Management Unit… … … … … … … … … … …*Sh. 810,050,000
Kifungu 3010 – *Defense and Security Unit …* Sh. 1,058,420,000
Kifungu 3012 – *Zanzibar Office … … … … … …*Sh. 291,014,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management…. …* Sh. 4,300,166,000
Kifungu 1002 – *Planning, Monitoring & Evaluation … … … … … … … …* Sh. 492,573,000
Kifungu 1003 – *Finance and Planning Unit … …*Sh. 593,541,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit … … … … …*Sh. 418,131,000
Kifungu 1005 – *Legal Services ... … … … … … …*Sh. 517,307,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management & Logistics Unit … … … … … ... ... .*Sh. 704,768,000
Kifungu 1007 – *Zanzibar Office … … … … … …*Sh. 310,470,000
Kifungu 2001 – *Election Management Division … … … … … … … … …* Sh. 607,512,000
Kifungu 2002 – *National Voters Registration & Information Communication Technology Division … … … …*Sh. 1,029,858,000
Kifungu 2003 – *Voters Education & Public Information Division … … … … ...*Sh. 956,233,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 65 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management* … … … … … ...Sh. 4,566,222,298
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit* … …Sh.505,473,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit* … … … Sh.752,434,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit* ... ... … … … … Sh.286,798,900
Kifungu 1005 - *Procurement Management Unit* … … … … … … … … … … ...Sh. 257,417,480
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit* … … … … … … … … … … …Sh.114,096,000
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology Unit*… … … … … … ...Sh.227,608,000
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit* ... ..… … … … Sh.212,148,000
Kifungu 2001 – *Labour* ... … … … … … … … … … Sh.6,192,776,296
Kifungu 2002 – *Employment Division* … … … … Sh. 727,709,000
Kifungu 2003 – *Registrar of Trade Unions* … … … Sh.197,810,920
Kifungu 2004 – *Arusha Regional Labour Office* … Sh.32,424,000
Kifungu 2005 – *Dodoma Regional Labour Office* … … … … … … … … … … .Sh. 32,424,000
Kifungu 2006 – *Geita Regional Labour Office* … …Sh.8,955,000
Kifungu 2007 – *Iringa Regional Labour Office* … … … … … … … … … … ..Sh.30,624,000
Kifungu 2008 – *Kagera Regional Labour Office* … … … … … … … … … … ..Sh.15,711,000
Kifungu 2009 - *Kigoma Regional Labour Office* … … … … … … … … … … ..Sh.22,467,000
Kifungu 2010 – *Kilimanjaro Regional Labour Office* … … … … … … … … … ... ..Sh.23,868,000
Kifungu 2011 - *Lindi Regional Labour Office* … … Sh.9,855,000
Kifungu 2012 – *Manyara Regional Labour Office* … … … … … … … … … … Sh.16,112,000
Kifungu 2013 – *Mara Regional Labour Office*… …Sh.17,061,000
Kifungu 2014 – *Mbeya Regional Labour Office* …Sh.48,136,000
Kifungu 2015 – *Morogoro Regional Labour* Office... … … … … … … ..Sh.23,668,000

Kifungu 2016 – *Mtwara Regional Labour Office* …Sh.25,468,000
Kifungu 2017 – *Mwanza Regional Labour Office*… … … … … … … ...Sh.69,804,000
Kifungu 2018 – *Njombe Regional Labour Office*....Sh.10,156,000
Kifungu 2019 – *Pwani Regional Labour Office*... …Sh.45,686,000
Kifungu 2020 – *Rukwa Regional Labour Office* ... Sh.16,912,000
Kifungu 2021 – *Katavi Regional Labour Office* … …Sh.8,556,000
Kifungu 2022 – *Ruvuma Regional Labour Office*…Sh.17,112,000
Kifungu 2023 – *Shinyanga Regional Labour Office*… … … … … … … ...Sh.23,627,000
Kifungu 2024 – *Simiyu Regional Labour Office* … …Sh.8,556,000
Kifungu 2025 - *Singida Regional Labour Office* …Sh.24,468,000
Kifungu 2026 – *Tabora Regional Labour Office* …Sh.31,224,000
Kifungu 2027 – *Tanga Regional Labour Office* … Sh.32,267,000
Kifungu 2028 – *Temeke Regional Labour Office*…Sh.46,936,000
Kifungu 2029 – *Kinondoni Regional Labour Office*… ... … … … … … ..Sh. 31,024,000
Kifungu 2030 – *Ilala Regional Labour Office* … …Sh.40,580,000
Kifungu 2031 – *Social Security Division* … … …Sh.573, 341,053
Kifungu 2032 – *Youth Development* … … … …Sh.1,568,122,072
Kifungu 2033 - *Employment Services Unit* … … …Sh.882,698,000
Kifungu 2034 – *Persons with Disability Unit* … …Sh.1,723,125,404
Kifungu 2035 – *Productivity Promotion Unit* … …Sh.419,048,577

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 91 – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management* … … … … … … Sh. 6,696,325,500
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit* … …Sh. 466,767,500
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit* … … … … … Sh. 337,795,500
Kifungu 1005 - *Legal Services Unit*… … … … … .Sh. 851,455,000
Kifungu 1006- *Procurement Management Unit*…Sh.287,715,000

Kifungu 1007- *Government Communication Unit… … … … … … … … … … … …* ...Sh. 375,170,000
Kifungu 2001- *Intelligence Division… … … … .*Sh. 1,599,802,000
Kifungu 3001- *Operations and Investigation Division… ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...*...Sh.1,982,830,000
Kifungu 4001 - *Prevention and Treatment Division… … … … … … … …* ..Sh. 1,518,607,500
Kifungu 5001- *Forensic and Inspection Division… … … … … … … … … …* ..Sh. 855,990,000
Kifungu 6001- *Zonal Offices… … … … … ... ... ...*Sh. 658,860,000

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 92 – Mamlaka ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania**

Kifungu 1001 – *Policy, Planning & Research* … Sh. 381,889,000
Kifungu 1002 – *Finance Administration & Research Mob… … … … … ...*Sh. 1,157,413,000
Kifungu 1003 – *Monitoring and Evaluation… …* Sh. 180,787,000
Kifungu 1004 – *Advocacy and Information Unit… … … … … ... .... ... .... ... ....*Sh. 310,004,000
Kifungu 1005 – *National Response … … … … ..*Sh. 748,606,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management... ...*Sh. 175,798,000
Kifungu 1007 – *Legal Services… … … … … ... ...*Sh. 163,314,000
Kifungu 1008 – *Management Information System… … … … … … … … …* Sh. 137,140,000
Kifungu 1009 – *Internal Audit Unit... ... ... ... ... ...* Sh. 182,021,000
Kifungu 1010 – *Special Programs Unit ... ... ... ...*Sh. 167,550,000
Kifungu 1011 – *Government Communication*....Sh. 66,695,000

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 15 – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi**

Kifungu 1005 – *Information Communication and Technology*... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 700,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 27 – Msajili wa Vyama vya Siasa**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 0
Kifungu 1011 – *Zanzibar* Office... ... ... ... ... ... ... ..Sh. 940,000,000

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 0
Kifungu 2001 - *Civil Affairs and* Contingencies... ... ... ... ... .Sh. 0
Kifungu 5001 - *Communication of Government Business*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 2,191,322,000
Kifungu 7001 - *Government Printer*... ... ... ... ... Sh. 1,880,000,000

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 42 – Mfuko wa Ofisi ya Bunge**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*... ... ... ... ... ... ... ..Sh. 2,700,000,000
Kifungu 1002 – *Budget Division*... ... ... ... ... ... ... ..Sh. 469,020,000
Kifungu 3004 – *Private Office of the Clerk*... ... Sh. 2,000,000,000

Kifungu 3006 – *Communication and International Relations*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 0

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

Kifungu 2001 – *Election Management Division* ... ... .... .... Sh. 0
Kifungu 2001 – *National Voters Registration and Information, Communication Technology*..Sh. 940,000,000

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 65 – Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*... .... ...Sh. 1,192,741,000
Kifungu 2001- Labour... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ..Sh. 100,000,000
Kifungu 2002 - *Employment Division*... ...... ... ...Sh. 5,520,720,000
Kifungu 2003 - *Registrar of Trade* Unions... ... ... ... Sh. 75,000,000
Kifungu 2031 - *Social Security Division*... ... ... ... ... Sh. 52,650,000
Kifungu 2032- *Youth Development*... ... ... ... ... Sh. 1,437,147,525
Kifungu 2033 -*Eemployment Services Unit*... ... Sh. 2,500,000,000
Kifungu 2034 - *Persons with Disability Unit*... ... .Sh. 3,871,455,875
Kifungu 2035 - *Productivity Promotion Unit*... ... ... ... ... ... ... Sh. 0

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 91- Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

Kifungu 4001- *Prevention and Treatment Division*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 8,775,172,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 92 – Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania**

Kifungu 1001 – *Policy, Planning and Research*... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 1,113,060,000
Kifungu 1002 – *Finance, Administration and Resource Mobilization*.. ... ... ... Sh. 2,421,630,000
Kifungu 1003 – *Monitoring and Evaluation*.. ... ...Sh. 627,459,000
Kifungu 1004 – *Advocacy and Information Unit*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 3,293,208,530
Kifungu 1005 – *National Response* ... ... ... ... ...Sh.10,795,006,470
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ..Sh. 155,000,000
Kifungu 1007 – *Legal Service Unit* ... ... ... ... ... ..Sh. 2,156,522,000
Kifungu 1008 – *Management Inform Systems* ... .Sh.344,379,000
Kifungu 1010 – *Special Programs Unit* ... ... ... ... ... Sh. 42,674,000
Kifungu 1011 - *Government Communication Unit*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 1,243,210,000

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba yake Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123 Kanuni ndogo ya 3(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la February mwaka 2023 na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake naomba sasa taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, kwa utaratibu wetu nitawahoji hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niseme ama nitamke rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 yamepitishwa rasmi na Bunge.

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Kwa hiyo nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, Waheshimiwa Mawaziri wawili mnaofanya kazi chini yake lakini pia Naibu Mawaziri wawili, Makatibu wakuu na Watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, nawapongeza sana kwa hatua hii ambayo tumefikia ya kupitisha makadirio ya mapato na matumizi, lakini pia nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuleta hapa bajeti ya Bunge ya na imepitishwa rasmi. Nakushukuru sana.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nitumie nafasi hii kuishukuru sana Kamati yetu ya Bunge ya Bajeti, Kamati yetu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inafanya kazi nzuri. Vilevile Kamati yetu ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambayo inashughulikia mambo ya *UKIMWI* pia na Kamati gani tena? Samahani Kamati ya Afya na Masuala ya *UKIMWI* lakini pia na Kamati ya Ustawi, kwa hiyo hizi ni Kamati mbili tofauti.

Kwa hiyo, niwashukuru sana kwa kuendelea kuisimamia Serikali yetu ninyi ambao mnasimamia Ofisi hii ya Waziri Mkuu, nawapongeza sana Kamati zetu zote kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuipitia bajeti hii; na sasa tumefikia hatua nzuri. Pia Wabunge wote ambao ni wajumbe wa Kamati hizo na wale ambao si wajumbe, wote mmeshiriki kwa pamoja humu Bungeni katika mjadala; na Waziri Mkuu ameeleza hapa wazi ni Wabunge wangapi ambao wamepata nafasi ya kuchangia kila mmoja wenu; yule aliyepeleka kwa maandishi na aliyezungumza mmetoa mchango mzuri. Bila shaka mmewasikia Mawaziri wakati wakihitimisha hoja hapa lakini pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba mapendekezo yenu mliyoyatoa na mawazo yenu mliyoyatoa katika mambo mbalimbali wataendelea kuyafanyia kazi, na yale ambayo yanahitaji ufafanuzi basi wataleta ufafanuzi kwa maandishi, kwa hiyo niwapongeze Wabunge wote kwa kazi nzuri.

Waheshimiwa Wabunge, na sasa tumehitimisha hii Bajeti ya Waziri Mkuu na sasa nilete matangazo mawili kwenu. Tangazo la kwanza ni la wageni. Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Hassan Kungu ambaye ni mpiga kura wake

kutoka Wilaya ya Tunduru Mkoa wa Ruvuma, Ndugu Fulko Abel Hyera karibu sana.

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Ally Juma Mohamed ambao ni familia yake kutoka Zanzibar, na hawa ni Ndugu Hisham Ally Juma ambaye ni mtoto wake, yupo pia Ndugu Walid Ally Juma ambaye pia ni mtoto wake, karibuni sana Bungeni.

Tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, anawatangazia Wabunge wote ambao wana hoja ya kuhusu Matrekta ya *URSUS* kwenye maeneo yao, anaomba mara baada ya kuhairisha shughuli za Bunge hapa muonane naye kama nilivyokuwa nimeagiza. Muonane naye kwenye ukumbi wa Msekwa D. Mara baada ya kutoka hapa Bungeni, Wabunge wote wanao husika wa hoya hiyo waonane na Mwenyekiti wa Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo.

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa hapa ujumbe na Mheshimiwa Mpina, nitampa nafasi ya dakika chache nimsikilize hoja yake, Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, wakati Katibu anasoma alikuwa anatumia neno laki katika kusoma kwake. Akifikia labda milioni ishirini laki mbili. Lakini kihasibu tunasema siyo laki tunasema kama inatimia laki mbili unasema ni milioni ni... sijui nitumie, nisome kwanza nani, ngoja nisome kwanza *figure* yenyewe.

Kwa mfano anaposema kumi na moja milioni, halafu anasema laki saba na moja, tunasema tu mia saba na moja elfu ndiyo *language* ya kiuhasibu ambayo ndiyo tunayotumia badala ya neno laki kwa sababu laki hili...

**SPIKA:** Sawa, sasa hicho ni kihasibu na Kiswahili inasomekaje? Maana humu ndani tupo ambao si wahasibu. Yaani tuelekeze vizuri ili twende vizuri maana ndiyo tumeanza sasa hivi bajeti, Kiswahili inasomwaje, ukimuacha yule ambaye ni Mhasibu, yule ambaye si Mhasibu anasoma tu namba kawaida anasomaje?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema anasoma kama ni laki mbili na Sabini na nne anasoma tu mia mbili sabini na nne elfu.

**SPIKA:** Akisema laki ni Kiswahili au si Kiswahili? Ndilo swali langu, yaani akisema laki ni Kiswahili au si Kiswahili au sio lugha ya hesabu yaani hesabu katika lugha yake haitambui neno laki au ni uhasibu ndio hautambui neno laki?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kihesabu na kihasibu hatuitambui hili neno laki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge humu ndani leo tulikuwa tunaelekezwa kuhusu Kiswahili na mimi hapa nikitazama kwenye Kamusi inaonekana neno laki na imeeleza hapo laki inatumikaji, kwenye Kiswahili kabisa. Sasa wale Wahasibu na Wataalam wa Hesabu nadhani itabidi ninyi ambao ni wataalamu wa Hesabu mnaweza kuamua kutumia lugha yenu ya Kitaalam lakini kwa maana ya Kiswahili hii ni lugha ya Kiswahili na ni Kiswahili fasaha kabisa kuitwa laki. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabune kwa hivyo alichokisoma Katibu hapo wakati tupo kwenye Kamati ya Matumizi kwa kutumia neno laki alikuwa sahihi na kwa hivyo hesabu zimesomwa sawasawa, kwa maana ya matumizi ya neno laki. Kwa hivyo katika kipindi hiki ambacho tutakuwa tukishughulika na namba matumizi ya neno laki, matumizi ya elfu pia yanaruhusiwa, isipokuwa Waheshimiwa Mawaziri mnapoleta hoja hapa kuna watu ambao huwa wanakuwa wanazizidisha zile sifuri kwa kusema hivi; ukianza na neno laki

kule mbele hautakiwi kusema neno elfu kwa sababu maana yake ameziongeza tena nyingine. Hayo tu ndiyo matumizi sahihi ya neno laki.

Ukianzia pale kwenye laki unasema laki halafu unasoma zile tarakimu umemaliza usiseme kule mbele. Ili utumie neno elfu lazima utumie lugha aliyosema Mheshimiwa Mpina. Kwa hiyo huwezi kutumia neno laki halafu mwishoni tena ukasema elfu kwa sababu utakuwa umeongeza kiasi cha sifuri kule mbele, na ndio maana kuna mwinginw hataki kusema Bilioni atasema Milioni kadhaa halafu kule mbele atakuja kusema hayo ma elfu yake. Nadhani tumeelewana vizuri. Kwa hiyo matumizi ya neno elfu mbele ni sawa na matumizi ya neno lake huku mwanzoni bila kusema elfu kule mbele pia ni sawa. Kwa hiyo bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa kwa namna ilivyosomwa kwenye Kamati ya Matumizi iko sawasawa na vifungu vimepitishwa sawasawa.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya kuyasema hayo ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa 03:00 Asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 11.40 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 14 Aprili, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*